# UFUNDISHAJI WA USHAIRI KWA KUTUMIA TAMTHILIA KATIKA SHULE ZA UPILI NCHINI KENYA: UCHUNGUZI KIFANI WA KAUNTI NDOGO YA TESO KASKAZINI

**Hillary Mauka Mukoya**

**Tasnifu Hii Imewasilishwa Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili Katika Elimu ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Cha Kibabii.**

**NOVEMBA, 2019**

## UNGAMO NA IDHINI

### UNGAMO LA MTAHINIWA

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kingine chochote.

**Hillary Mauka Mukoya**

**(M.ED/KIS/008/14)**

Sahihi________________________ Tarehe____________________

### IDHINI YA WASIMAMIZI

Tasnifu hii imewasilishwa kwa ajili ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na chuo.

**Dkt. Misiko Wasike,**

Sahihi__________________________ Tarehe__________________

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,

Chuo Kikuu cha Kibabii.

**Dkt. Deborah Nanyama Amukowa,**

Sahihi__________________________ Tarehe__________________

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,

Chuo Kikuu cha Maseno.

**Dkt. Edwin Masinde,**

Sahihi__________________________ Tarehe__________________

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,

Chuo Kikuu cha Kenyatta.

## IKIRARI NA HATI MILIKI

Mimi, Hillary Mauka Mukoya ninathibitisha kwamba, tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe. Tasnifu hii haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika chuo chochote kwa ajili ya shahada kama hii au nyingine yoyote.

Tasnifu hii ya shahada ya Uzamili katika Elimu ya Kiswahili ni kazi inayolindwa kwa mujibu wa makubaliano ya mswada wa kisheria wa Berne, kifungu cha hati miliki cha mwaka 1999 na sheria nyingine za kitaifa na kimataifa, kwa niaba ya mwanataaluma. Kazi hii hairuhusiwi kutolewa kwa namna yoyote ile, yote au sehemu, isipokuwa kwa matumizi ya kitaaluma ya utafiti, kujisomea na kurejelea kwa kibali cha maandishi kutoka kwa Mkurugenzi wa Masomo ya Uzamili kwa niaba ya mwandishi na Chuo Kikuu cha Kibabii, Kenya.

# TABARUKU

Nawatabarukia tasnifu hii wazazi wangu wapendwa Gabriel Mauka Mukoya na Rose Kerubo Nyasarura kwa mapenzi yao ya dhati.

# SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia neema katika kipindi chote cha masomo yangu ya uzamili. Nisingefika hapa nilikofikia pasi na nguvu, uwezo na afya njema aliyonijalia. Hakika utukufu na heshima ni kwake Mwenyezi Mungu aliye muweza na mumiliki wa yote. Natoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu wa kazi hii Dkt. Misiko Wasike, Dkt. Deborah Nanyama Amukowa na Dkt. Edwin Masinde kwa kutumia muda wao kuniongoza kwa busara, ukakamavu na kujitolea. Ushauri wao ulinifaa zaidi kwa kuandika kazi hii. Nawashukuru wahadhiri wangu Dkt. Fred Simiyu Wanjala, Dkt. Carren Nyandiba, Dkt. Nilson Opande, Mwalimu Eric Wamalwa, na wengine wote katika idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Kibabii kwa kunitia hamasa nilipokuwa nikiandika kazi hii. Sitowasahau Dkt. Juma Injendi na Bi. Gladys Kinara kwa kunipa mwelekeo mara ya kwanza chuoni Kibabii nilipokuwa katika pilikapilika za kuanza kufanya shahada hii ya uzamili. Namshukuru babangu mpendwa Gabriel Mauka Mukoya pamoja na mamangu mpendwa Rose Kerubo Nyasarura kwa mapenzi yao ya dhati. Ahsante sana kwa kujitolea kwenu katika hali zote kunielimisha. Shukrani za dhati ziwaendee ndugu zangu kwa kunifaa kwa kila jambo.

Namshukuru mke wangu kipenzi Bi. Janet Nasimiyu kwa kunitia moyo nilipokuwa nikishughulikia kazi hii. Shukrani zaidi ni kwa binti yangu mpendwa Evangeline Kemunto; haikuwa rahisi kutimiza majukumu yangu ya kuwa mzazi na kuishughulikia kazi hii pasi na kumpunja wakati niliohitajika kuwa naye. Ahsante sana kwa kunivumilia. Namshukuru Bi. Elizabeth Nasimiyu Siundu kwa kunihimiza mara kwa mara. Nawashukuru wanafunzi wenzangu Martin Lutta, David Kibiti, Anne Nabutola, Rose Abai, Stephen Ndinyo, Benard Wangwa, Melly Kipchirchir, Elizabeth Soita, Inviolata Simbi, Emily Magambo na Martha Wafula kwa kunitia moyo mara kwa mara hasa nilipohisi kulemewa. Natoa shukrani za dhati kwa walimu wenzangu katika Shule ya Upili ya Wasichana ya Askofu Sulumeti-Chelelemuk kuanzia 2015 hadi sasa kwa kunifaa nilipokuwa nikishughulikia kazi hii. Ahsanteni sana walimu. Mwisho nawashukuru watafitiwa wangu kwa kukubali niwasaili na hivyo basi, kufanikisha uandishi wa tasnifu hii. Mwisho kabisa nawashukuru wengine wote ambao walichangia kwa njia moja au nyingine katika ufanisi wa kazi hii.

# IKISIRI

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu utanzu mmoja kutumika kuwasilisha mawazo katika utanzu mwingine. Mbinu ya mwelekeo mseto imetafitiwa na wataalam mbalimbali kuhusu isimu kutumika kufundisha fasihi na fasihi kutumika kufundisha isimu. Hata hivyo, mtafiti hajakumbana na utafiti unaohusu utanzu mmoja wa fasihi kutumika kufundisha utanzu mwingine wa fasihi, hasa tamthilia kufundisha ushairi. Kumbe dhana ya usetaji inaweza kutumika katika ufundishaji wa tanzu za fasihi. Kwa hivyo, kuna haja ya kufanya utafiti kuhusu ufundishaji wa ushairi kwa kutumia tamthilia. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza namna tamthilia inavyotumika kufundisha ushairi katika shule za upili zilizoko Kaunti Ndogo ya Teso Kaskazini, Busia Kenya. Malengo mahususi ya utafiti yalikuwa: kuchunguza namna ushairi unavyofundishwa katika shule za upili, kupambanua namna tamthilia inavyoweza kutumika kufundisha ushairi na kueleza mchango wa matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa ushairi. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya utanzu ambayo iliasisiwa na Boas (1940) na kuendelezwa naye Bakhtin (1981). Nadharia hii ina mihimili ifuatayo: Mhimili wa kwanza unaoshikilia kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi sana; mhimili wa pili unaeleza kuwa, matumizi ya utanzu mwingine huwafanya wasomaji au wapokezi kuwa na ilhamu zaidi kuliko kuwapa kila wanachotarajia na mhimili wa tatu unashikilia kuwa, tanzu mbili zilizozoeleka zitumike kwa pamoja kwa sababu ya sifa zenye uhusiano mkubwa. Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo. Sampuli ya utabakishaji wa kimakusudi ilitumika kuchagua shule za upili tisa (9) zilizowakilisha asilimia thelathini (30%) ya shule zilizo katika Kaunti Ndogo ya Teso Kaskazini iliyo na jumla ya shule thelathini (30). Kwa upande mwingine, sampuli ya kimakusudi ilitumika kuchagua mwalimu mmoja kutoka katika kila shule aliyeshiriki katika utafiti huu. Mbinu za ukusanyaji data zilizotumika ni usaili na uchunzaji. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, vipengee vya mtindo, muundo na maudhui katika ushairi vilifundishwa kwa kutumia mbinu tofautitofauti za ufundishaji. Aidha, ilibainika kuwa, tamthilia ya *Kifo Kisimani*, *Mstahiki Meya* na *Kigogo* zilikuwa katika nafasi nzuri ya kufundishia mtindo, muundo na maudhui kwa sababu zilikuwa na bahari mbalimbali za ushairi. Mchango wa matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa ushairi ulionyeshwa; utafiti ulibaini kuwa, ufundishaji wa tamathali za usemi ulifanywa kwa urahisi, muundo wa ushairi ulifafanuliwa vizuri, wanafunzi walielewa maudhui kwa urahisi, walimu walikamilisha silabasi mapema, wanafunzi walichangamkia somo, ilhamu ya kutafiti iliibuliwa miongoni mwa wanafunzi na wanafunzi walimakinika darasani. Utafiti huu unapendekeza kuwa, walimu watilie maanani mbinu mahususi za ufundishaji wanapofundisha vipengee vya ushairi kama vile mtindo, muundo na maudhui ili kuhakikisha kwamba, wanafunzi wanafurahia utanzu wa ushairi. Vilevile, unapendekeza kuwa, usetaji katika ufundishaji na ujifunzaji uweze kutiliwa maanani na walimu wanapofunza ushairi wa Kiswahili kwa kusudi la kuondoa uchovu miongoni mwa wanafunzi. Aidha, unapendekeza walimu waboreshe mwelekeo wa ufundishaji mseto kusudi mada zinazofundishwa zieleweke bora zaidi. Pia unapendekeza kwamba, walimu wazingatie mchango wa matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa ushairi. Utafiti huu utawasaidia walimu wa shule za upili kuboresha zaidi ufundishaji wa ushairi kwa kuzingatia mbinu mahususi za ufundishaji wa ushairi. Utafiti huu pia utabainisha mchango wa kutumia tamthilia katika ufundishaji wa ushairi na hivyo basi, kufaa asasi zinazowaandaa walimu katika matumizi ya mbinu ya mwelekeo mseto katika ufundishaji wa fasihi.

**ABSTRACT**

Many studies have been done concerning one genre being used to present ideas in another genre. The integrated approach method has been studied by various scholars concerning linguistics being used to teach literature and literature being used to teach linguistics. However, the researcher has not come across a study that concerns one genre of literature being used to teach another genre of literature, especially a play to teach poetry. So the integrated approach concept can be used in teaching of literature genres. Therefore, there is need of doing research about teaching of poetry using a play. The main objective of this research was to analyse how a play is used in teaching of poetry in secondary schools that are found in Teso North Sub County, Busia Kenya. The specific objectives of this research were: to analyse how poetry is taught in secondary schools, to clarify how a play can be used to teach poetry and to explain the role of usage of a play in teaching of poetry. The research was guided by the genre theory that was propounded by Boas (1940) and advanced by Bakhtin (1981). This theory has the following tenets: The first tenet which holds that genre emerges with the structure of a certain work of literature and therefore makes such a work to be easily understood; the second tenet explains that the usage of a genre in another genre makes the readers or the receivers to have more interest than giving them everything they expect and the third tenet holds that it is important for the two genres that are common in the society to be used together because of features that are closely related. This study adopted the descriptive research design. Stratified sampling was used to select nine (9) secondary schools which represent thirty percent (30%) of the thirty (30) schools in Teso North Sub County. On the other hand, purposive sampling was used to select one Kiswahili teacher from every school to be involved in this research. The techniques of data collection were interview and observation. The data collected was analysed and presented by considering the objectives of this study. The research findings showed that aspects of the structure, form and the themes in poetry were taught using various methods of teaching. It was also found out that the three Swahili plays that is, *Kifo Kisimani*, *Mstahiki Meya* and *Kigogo* were well placed in teaching of structure, form and the themes because they had various genres of poetry. The role of usage of plays in teaching of poetry came out; the study found out that it was easier to teach stylistic devices, the structure of poetry was well elaborated, learners easily understood the themes, teachers completed the syllabus early, learners liked the lessons, the interest of researching among the learners arose and the learners became keen during lessons. This study recommends that teachers should consider specific methods of teaching while teaching poetry aspects like structure, form and the themes so as to ensure that learners like the poetry genre. It also recommends that integration in teaching and learning should be considered by teachers when teaching Kiswahili poetry for the purposes of doing away with boredom among learners. The study also recommends that teachers should better the approach of integrated method of teaching for the purposes of ensuring that the topics taught are more understood. It also recommends that, teachers should consider the role of usage of a play in teaching of poetry. This study will help secondary school teachers better their teaching more in poetry by considering specific methods of teaching poetry. This study will also distinguish the contributions of the usage of a play in teaching of poetry and will therefore benefit institutions that prepare teachers in the usage of an integrated approach method in teaching of literature.

## ORODHA YA VIFUPISHO

**h.t** haijawekewa tarehe

**k.h.j.** Keshatajwa

**uk** Ukurasa

## FASILI YA ISTILAHI ZILIZOTUMIKA

**Maudhui** Mawazo makuu yanayojitokeza katika kazi ya ushairi.

**Mchango** Umuhimu au athari inayobainika tamthilia inapotumika kufundisha ushairi.

**Mtindo** Mbinu za uandishi na tamathali za usemi namna zilivyotumiwa na mtunzi wa ushairi.

**Muundo** Mpangilio maalum wa kazi fulani ya ushairi kwa mfano mizani, vina, mishororo, vipande, vibwagizo, vimalizio na beti ni vipengee.

**Nadharia** Mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kutekeleza jambo fulani.

**Tamthilia** Utungo wa kisanaa ambao huweka wazo fulani katika matendo na mazungumzo na aghalabu huigizwa.

**Ufundishaji** Namna ya kuelekeza mtu jambo ili afahamu.

**Usetaji** Mchakato wa ufundishaji unaohusu kufungamanisha mada mbili au zaidi zinazohusiana katika kipindi cha mafunzo ili zichangiane na kuongezana nguvu.

**Ushairi** Sanaa ya utunzi wa mashairi, tenzi, ngonjera na nyimbo.

## ORODHA YA MAJEDWALI


| | | |
|---|---|---|
| Jedwali 4.2.1.1 | Namna mtindo wa ushairi unavyofundishwa katika shule za upili | uk. 58 |
| Jedwali 4.2.2.1 | Namna muundo wa ushairi unavyofundishwa katika shule za upili | uk. 66 |
| Jedwali 4.2.3.1 | Namna maudhui katika ushairi yanavyofundishwa katika shule za upili | uk. 74 |
| Jedwali 4.3.1.1 | Namna tamthilia inavyoweza kufundisha mtindo katika ushairi | uk. 81 |
| Jedwali 4.3.2.1 | Namna tamthilia inavyoweza kufundisha muundo katika ushairi | uk. 86 |
| Jedwali 4.3.3.1 | Namna tamthilia inavyoweza kufundisha maudhui katika ushairi | uk. 92 |
| Jedwali 4.4.1 | Mchango wa tamthilia katika ufundishaji wa ushairi | uk. 98 |

**YALIYOMO**

**UNGAMO NA IDHINI** ........ ii

**IKIRARI NA HATI MILIKI** ........ iii

**TABARUKU** ........ iv

**SHUKRANI** ........ v

**IKISIRI** ........ vi

**ABSTRACT** ........ vii

**ORODHA YA VIFUPISHO** ........ viii

**FASILI YA ISTILAHI ZILIZOTUMIKA** ........ ix

**ORODHA YA MAJEDWALI** ........ x

**YALIYOMO** ........ xi

**SURA YA KWANZA: MSINGI WA UTAFITI** ........ 1

1.1 Utangulizi ........ 1

1.2 Usuli wa Mada ........ 1

1.3 Suala la Utafiti ........ 3

1.4 Malengo ya Utafiti ........ 4

1.4.1 Maswali ya Utafiti ........ 4

1.5 Umuhimu wa Utafiti ........ 4

1.6 Sababu za Kuchagua Mada ........ 5

1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti ........ 5

1.8 Misingi ya Kinadharia ........ 6

1.9 Hitimisho ........ 8

**SURA YA PILI: UHAKIKI WA MAANDISHI ........ 10**

2.1 Utangulizi ........ 10

2.2 Ufundishaji Mseto ........ 10

2.3 Maelezo Kuhusu Ushairi, Mtindo, Muundo, Maudhui na Mbinu za Ufundishaji ........ 18

2.4 Namna Ushairi Unavyofundishwa Katika Shule za Upili ........ 22

2.5 Namna Tamthilia Inavyoweza Kutumika Kufundisha Ushairi ........ 27

2.6 Mchango wa Tamthilia Katika Ufundishaji wa Ushairi ........ 37

2.7 Hitimisho ........ 41

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ........ 43**

3.1 Utangulizi ........ 43

3.2 Muundo wa Utafiti ........ 43

3.3 Eneo la Utafiti ........ 44

3.4 Sampuli na Usampulishaji ........ 44

3.4.1 Umma Lengwa ........ 45

3.4.2 Sampuli ........ 45

3.4.3 Usampulishaji ........ 45

3.5 Mbinu za Kukusanya Data ........ 46

3.5.1 Utafiti Maktabani ........ 47

3.5.2 Utafiti Nyanjani ........ 47
3.5.2.1 Usaili ........ 48
3.5.2.2 Uchunzaji ........ 48
3.6 Vifaa vya Ukusanyaji Data ........ 49
3.6.1. Dodoso ........ 49
3.6.2 Mwongozo wa Kuchunza Vipindi ........ 49
3.6.3 Kinasa Sauti ........ 50
3.7 Utafiti Mwigo ........ 50
3.8 Uwasilishaji na Uchanganuzi wa Data ........ 51
3.9 Uhalali na Uthabiti wa Vifaa ........ 51
3.9.1 Uhalali wa Vifaa ........ 51
3.9.2 Uthabiti wa Vifaa ........ 52
3.10 Maadili Katika Utafiti ........ 53
3.11 Changamoto za Utafiti ........ 55
3.12 Hitimisho ........ 55
**SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA ........ 57**
4.1 Utangulizi ........ 57
4.2 Namna Ushairi Unavyofundishwa Katika Shule za Upili ........ 58
4.2.1 Mtindo ........ 58
4.2.2 Muundo ........ 66

4.2.3 Maudhui ........ 74
4.3 Namna Tamthilia Inavyoweza Kutumika Kufundisha Ushairi ........ 81
4.3.1 Mtindo ........ 81
4.3.2 Muundo ........ 86
4.3.3 Maudhui ........ 92
4.4 Mchango wa Matumizi ya Tamthilia Katika Ufundishaji wa Ushairi ........ 97
4.5 Hitimisho ........ 105
**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 107**
5.1 Utangulizi ........ 107
5.2 Muhtasari wa Tasnifu ........ 107
5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ........ 109
5.3.1 Namna Ushairi Unavyofundishwa Katika Shule za Upili ........ 109
5.3.2 Namna Tamthilia Inavyoweza Kutumika Kufundisha Ushairi ........ 110
5.3.3 Mchango wa Matumizi ya Tamthilia Katika Ufundishaji wa Ushairi ........ 110
5.4 Hitimisho ........ 111
5.5 Mapendekezo ........ 112
5.6 Tafiti za Baadaye ........ 112
**MAREJELEO ........ 114**
**VIAMBATISHO ........ 119**
Kiambatisho 1: Mwongozo wa Maswali (Dodoso) ........ 119

Kiambatisho 2: Mwongozo wa Kuchunza Vipindi ........ 120

Kiambatisho 3: Orodha ya Shule ........ 121

Kiambatisho 4: Ramani ya Utafiti ........ 123

Kiambatisho 5: Ratiba ya kazi ........ 124

Kiambatisho 6: Maazimio ya Kazi ........ 125

Kiambatisho 7: Maazimio ya Kazi ........ 126

Kiambatisho 8: Maandalizi ya Somo ........ 127

Kiambatisho 9: Maandalizi ya Somo ........ 128

Kiambatisho 10: Maandalizi ya Somo ........ 129

Kiambatisho 11: Maandalizi ya Somo ........ 130

Kiambatisho 12: Hifadhi ya Kazi ........ 131

Kiambatisho 13: Hifadhi ya Kazi ........ 132

Kiambatisho 14: Hifadhi ya Kazi ........ 133

Kiambatisho 15: Barua ya Idhini Kutoka SGS ........ 134

Kiambatisho 16: Barua ya Idhini Kutoka NACOSTI ........ 135

Kiambatisho 17: Kibali cha Utafiti Kutoka NACOSTI ........ 136

Kiambatisho 18: Barua ya Idhini Kutoka kwa Kamishna wa Kaunti ya Busia ........ 137

Kiambatisho 19: Barua ya Idhini Kutoka kwa Mkurugenzi wa Elimu katika Kaunti ya Busia ........ 138

# SURA YA KWANZA

# MSINGI WA UTAFITI

## 1.1 Utangulizi

Sura hii inahusu usuli wa utafiti, suala la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti na umuhimu wa utafiti. Vilevile, imeangazia upeo na mipaka ya utafiti, sababu za kuchagua mada na nadharia ya utanzu ambayo iliongoza utafiti.

## 1.2 Usuli wa Mada

Kiswahili ni somo la lazima katika shule za msingi na za upili nchini Kenya. Baada ya miaka minne ya elimu katika shule ya upili, mwanafunzi hutahiniwa katika somo hili ambalo huwa limegawika katika karatasi tatu; 102/1 (insha), 102/2 (lugha) na 102/3 (fasihi). Karatasi ya 102/3 huwa ni ya fasihi andishi na fasihi simulizi. Fasihi andishi huwa na sehemu zifuatazo: riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi. Ushairi huwa na mashairi ya arudhi na huru.

Wataalamu mbalimbali wameelezea kwa kina maana ya tamthilia na ushairi. Mathalani Haji, Muhammed, Hamad na Omar (1981), wanasema kuwa, tamthilia ni utungo ulioandikwa au usioandikwa ambao unalieleza na kuliweka wazo linalotendeka mbele ya hadhira. Kulingana na Wafula (2003), tamthilia ni moja kati ya tanzu kubwa na muhimu za fasihi, na si rahisi kuonyesha tofauti zilizopo kati ya tamthilia na tanzu nyingine za fasihi kwa sababu tanzu hizi huingiliana.

Kulingana na Massamba (1983), ushairi ni sanaa ya vina inayopambanuliwa kama nyimbo, mashairi na tenzi. Anazidi kueleza kuwa, ushairi una ufasaha wa maneno machache au muhtasari. Vilevile, anasema kuwa, sanaa ya ushairi ni chombo cha kubebea maudhui, yaani chombo ambacho bila ya kuwepo, wazo la ushairi huwa halipo tena.

Masebo na Nyangwine (2010) wanasema kuwa, tume ya Ominde ilipendekeza kuwe na ufundishaji wa Kiswahili kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu nchini Kenya. Wanaendelea kusema kuwa, Tume ya Mackay ya mwaka wa 1982 ilisisitiza kuwa, Kiswahili kifundishwe kama somo la lazima nchini katika shule zote za upili nchini Kenya. Kutokanana na pendekezo la Mackay 1982, masomo ya fasihi yalifunzwa.

Iyaya, Kobia na Luganda (2016) wamechunguza mbinu zinazotumiwa na walimu wa shule za upili nchini Kenya kufundishia somo la ushairi. Kulingana nao, inabainika kuwa, walimu huwa hawana nyenzo za kutosha wanapofundisha somo la ushairi. Hivyo basi, kuwepo kwa nyenzo zisizotosha katika ufundishaji wa somo la ushairi ni changamoto kwa walimu wanaofundisha somo la ushairi.

Matumizi ya utanzu kufundisha utanzu mwingine ni miongoni mwa mbinu za kisasa za kufundisha. Taasisi ya Elimu ya Kenya (2006) inapendekeza mbinu ya mwelekeo mseto wa ufundishaji wa somo la Kiswahili itumike katika shule za upili. Hii ina maana kuwa masomo ya lugha na fasihi yajumuishwe kwa pamoja ili yachangiane. Taasisi ya Elimu ya Kenya (k.h.j.) inaendelea kusema kuwa, vipindi vya lugha huwa vikavu na hivyo basi huwasinya wanafunzi ambao baadaye huvichukia lakini kwa upande mwingine wanafunzi huvipenda vipindi vya fasihi. Kwa hivyo pana haja ya kufundisha ushairi kwa kutumia tamthilia ili kupata uhai na mvuto katika somo la Kiswahili kwa ujumla.

Utafiti huu ulishirikisha mbinu ya mwelekeo mseto kwa sababu mbinu hii ina nafasi katika ufundishaji wa tanzu za fasihi. Mathalani tanzu za fasihi andishi zinaweza kufundishwa kwa

pamoja kwa kuzingatia sifa zinazofanana kwa mfano mtindo, muundo na maudhui katika tamthilia na ushairi. Hivyo basi, mwalimu anaweza kutumia utanzu kama vile tamthilia kufundishia vipengele kama vile mtindo, muundo na maudhui katika ushairi.

Maitaria (2012) anatathmini matumizi ya methali katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Ameonyesha kuwa, methali kama kipera kimojawapo cha fasihi simulizi ina nafasi katika utunzi wa ushairi; methali imetumika katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili.

Tamthilia na ushairi ni tanzu za fasihi ambazo zinafundishwa katika shule za upili kwa kutumia mbinu kadha wa kadha, hata hivyo Taasisi ya Elimu ya Kenya (k.h.j.) inapendekeza mbinu ya mwelekeo mseto itumike kufundishia masomo ya Kiswahili. Kwa hivyo, tamthilia kama utanzu mmojawapo wa fasihi andishi una nafasi katika kufundishia utanzu mwingine kama vile ushairi.

**1.3 Suala la Utafiti**

Kuna mbinu nyingi za kisasa za kufundisha ushairi katika shule za upili. Taasisi ya Elimu ya Kenya inapendekeza kuwa, mbinu ya mwelekeo mseto itumike katika ufundishaji wa somo la Kiswahili mathalani masomo ya lugha na fasihi yafundishwe kwa pamoja ili wanafunzi wayachangamkie. Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu utanzu mmoja kutumika kuwasilisha mawazo katika utanzu mwingine. Mbinu ya mwelekeo mseto imetafitiwa na wataalam mbalimbali kuhusu isimu kutumika kufundisha fasihi na fasihi kutumika kufundisha isimu. Hata hivyo, mtafiti hajakumbana na utafiti unaohusu utanzu mmoja wa fasihi kutumika kufundisha utanzu mwingine wa fasihi, hasa tamthilia kufundisha ushairi. Kumbe dhana ya usetaji inaweza kutumika katika ufundishaji wa tanzu za fasihi. Kwa hivyo, kuna haja ya kufanya utafiti kuhusu ufundishaji wa ushairi kwa

kutumia tamthilia. Utafiti huu ulichunguza ufundishaji wa ushairi katika shule za upili kwa kutumia tamthilia.

### 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza namna tamthilia inavyotumika kufundisha ushairi katika shule za upili za Kaunti Ndogo ya Teso Kaskazini, Busia Kenya. Utafiti hususan ulilenga:

i. Kuchunguza namna ushairi unavyofundishwa katika shule za upili.
ii. Kupambanua namna tamthilia inavyoweza kutumika kufundisha ushairi.
iii. Kueleza mchango wa matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa ushairi.

#### 1.4.1 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kujibu maswali yafuatayo;

i. Je, ushairi unafundishwa vipi katika shule za upili?
ii. Tamthilia inawezaje kutumika kufundisha ushairi?
iii. Mchango wa matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa ushairi ni upi?

### 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ambao unahusu matumizi ya tamthilia katika kufundisha ushairi utakuwa na manufaa kwa njia mbalimbali: Utawasaidia walimu wa shule za upili kuboresha zaidi ufundishaji wa ushairi. Vilevile, utatoa mwelekeo mpya katika ufundishaji wa ushairi. Aidha, utatoa mbinu ibuka katika ufundishaji wa ushairi. Ni utafiti ambao utakuwa wa manufaa kwa asasi zinazowaandaa walimu kwa kuwa utachangia katika kuboresha zaidi maandalizi yao kuhusu mwelekeo mseto wa ufundishaji wa fasihi. Licha ya hayo, utafiti huu utawafaa waandishi wa vitabu kwa kuwa utadhihirisha namna utanzu mmoja wa fasihi unavyofanikisha ufunzaji na ujifunzaji wa utanzu mwingine: matumizi ya utanzu mmoja katika kufundisha utanzu mwingine kando na mbinu za

ufundishaji zilizozoeleka. Kwa upande wa wanafunzi, utafiti huu utazua ilhamu yao ya kuchangamkia ushairi kwa kuwa ufundishaji wa tanzu mbili za fasihi utatendeka kwa pamoja na hivyo basi kuwa na ujifunzaji bora wa ushairi.

### 1.6 Sababu za Kuchagua Mada

Kuna sababu kadhaa zilizochangia katika uteuzi wa mada hii ya utafiti. Sababu hizi ni: Kiswahili ni somo la lazima katika shule za upili nchini Kenya ambalo huwa na fasihi iliyo na tanzu za ushairi na tamthilia ambazo hufundishwa na kutahiniwa. Sababu ya pili ni kuwa, Wizara ya Elimu ya Kenya inapendekeza matumizi ya mbinu ya mwelekeo mseto katika ufundishaji wa somo la Kiswahili. Sababu ya tatu ni kuwa, matumizi ya utanzu mmoja kufundisha utanzu mwingine ni miongoni mwa mbinu ibuka za kufundisha ambazo zinachangamkiwa katika shule za upili. Sababu ya nne ni kuwa, kuna haja ya kutafiti mbinu zaidi za kufundisha ushairi ili kuboresha zaidi ufundishaji miongoni mwa walimu na hivyo basi, kuwasaidia wanafunzi kuboresha zaidi ujifunzaji wao wa ushairi katika shule za upili nchini Kenya. Sababu ya tano ni kuwa, juhudi za kutunga, kuhakiki na kufundisha ushairi hazina kikomo.

### 1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijifunga katika sifa zinazobainika katika tamthilia na ushairi na hivyo basi, kuwa mwafaka katika kufundishia ushairi. Sifa hizo ni: mtindo, muundo na maudhui. Utafiti ulichunguza namna ushairi unavyofundishwa katika shule za upili kwa kuzingatia mtindo, muundo na maudhui kwa kutumia mhimili wa nadharia ya utanzu uelezao kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi ya fasihi. Utafiti huu pia ulipambanua namna tamthilia inavyoweza kutumika kufundisha mtindo, muundo na maudhui katika ushairi kwa kutumia mhimili uelezao kuwa, tanzu mbili zilizozoeleka zitumike kwa pamoja kwa sababu ya sifa zenye uhusiano mkubwa. Aidha, utafiti huu ulieleza mchango wa matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa ushairi kwa kuzingatia mtindo, muundo

na maudhui kwa kutumia mhimili uelezao kuwa, matumizi ya utanzu mwingine huwafanya wapokezi au wasomaji kuwa na ilhamu.

Utafiti huu ulirejelea tamthilia tatu ambazo ni: *Kifo Kisimani* (Mberia, 2001), *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na *Kigogo* (Kea, 2016). Kidato cha tatu kilihusishwa katika utafiti huu. Eneo la utafiti huu ni Teso Kaskazini.

**1.8 Misingi ya Kinadharia**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya utanzu. Kulingana na Wanyela (2007), nadharia ya utanzu iliasisiwa na Boas (1940). Nadharia hii iliendelezwa naye Bakhtin (1981). Nadharia hii ilitumiwa katika anthropolojia wakati wa Boas katika kuchunguza lugha asilia ya Marekani. Wanasayansi jamii na wanamiundo waliitumia hii nadharia baadaye. Vilevile, ilitumiwa katika enthrografia ya mazungumzo. Nadharia ya utanzu ni kama kundi, aina, namna au mtindo wa utendaji wenye kuwasiliana ambao huelezwa, huainishwa na kujulikana kuwa ni mali ya kundi husika. Hii inatokana na sifa bainifu za umbo lake na mbinu zilizotumiwa katika kujengwa au kuendelezwa kwake kulingana na warasimi kama vile Plato, Aristotle na Horace. Wakati wa wanafalsafa kama vile Plato, Aristole na Horace kulikuwa na tanzu tatu pekee ambazo ni: shairi la hisia, drama na utendi. Wanyela (k.h.j.) anasema kuwa, tanzu hufungamana wala si tenge; hii ina maana kuwa, tanzu hujumuisha mitindo mbalimbali na huingiliana kwa kiasi kikubwa.

Bakhtin (k.h.j.) anaeleza kwamba, mgawanyo wa mbinu na lugha kutoka kwa suala la utanzu umekuwa na jukumu kubwa katika hali ambapo mtu binafsi na kipindi hufungamanishwa na mtindo na hivyo basi, kuwa na umuhimu ikilinganishwa na toni ambayo hupuuzwa. Anaongezea kwamba, katika tanzu za mashairi, ufahamu wa kisanii, unaoeleweka kama umoja wa waandishi wote wa semantiki na uelezaji wa nia hubainika katika lugha yenyewe.

Naye Matundura (2015) anasema kuwa, nadharia ya utanzu ni utaratibu wa kuainisha fasihi katika misingi ya aina mbalimbali kwa kuegemea miundo na maumbo. Umbo ni sifa za nje zinazoipa kazi ya fasihi sura za kutambulika (matendo, maonyesho, vina na mizani) ilhali muundo ni jumla ya uhusiano unaokuwepo kati ya vijisehemu mbalimbali vinavyounda kitu kamili au kwa jumla.

Matundura (k.h.j.) anasema kuwa, nadharia ya utanzu ina misingi yake katika kipindi cha urasimi ambapo fasihi ya Ugiriki na Urumi ilifana. Anatoa mfano wa *Poetics* ambapo Aristotle anaeleza maana na sifa za tamthilia ya kitanzu. Hivyo basi, nadharia ya utanzu katika kipindi cha urasimi ililenga kuwekea tanzu mipaka. Hii ni tofauti na nadharia ya kipindi hiki ambayo mara nyingi ni ya kimaelezo tu; inaelezea tanzu zilizopo na sifa zao bila kuziwekea sheria zozote na mipaka yoyote. Ni nadharia ambayo inatambua kuwa, kazi za kifasihi zinazotambulika zinaweza kuchanganywa na vilevile, zinaweza kuzaa tanzu mpya; umahuluti wa tanzu.

Matundura (k.h.j.) anaelezea kuwa, thamani kuu ya nadharia ya utanzu haitokani na suala la uainishaji bali inatuwezesha tu kueleza jinsi ya kuweka kazi fulani katika tanzu mahususi ili kuweza kuifasiri na kuishughulikia. Hii ina maana kuwa, badala ya kusisitiza upekee wa kila utanzu, nadharia ya utanzu ya kisasa inaangalia sifa za jumla za kila utanzu, kunga zake na lengo lake la kifasihi.

Wanyela (k.h.j.) anasema kuwa, hakuna migao maalum ya kutenganisha visasili na ngano kwa kuwa tanzu hizi mbili zinaingiliana. Hivyo basi, tofauti iliyopo hudhihirika katika fikira za wanajamii. Utanzu kama mfumo maalum wa matini ambao huleta pamoja watunzi, wapokezi, mada na njia ya kuwasilisha kulingana na shughuli fulani humtawala na kumwongoza mtunzi kwa matarajio ya wapokezi kulingana na ujuzi wa watunzi wa utanzu husika. Matarajio na sheria za utanzu husika hufahamika miongoni mwa wapokezi na watunzi wa utanzu husika. Kwa hivyo anayesoma tanzu husika anafaa awe na uwezo wa kutambua kanuni zinazowajibikia utanzu mmoja

na mwingine ili aweze kutofautisha tanzu hizo. Nadharia ya utanzu ina mihimili ifuatayo ambayo imetumiwa katika utafiti huu:

Mhimili wa kwanza unashikilia kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi sana. Mhimili huu uliwezesha utafiti huu kubainisha namna ya kufundisha ushairi katika shule za upili nchini Kenya; utafiti uliweza kubainisha vipengee vya ushairi kama vile mtindo, muundo na maudhui namna vinavyofundishwa katika shule za upili kwa kuzingatia mhimili huu.

Mhimili wa pili unashikilia kuwa, tanzu mbili zilizozoeleka zitumike kwa pamoja kwa sababu ya sifa zenye uhusiano mkubwa. Mhimili huu ulifaa utafiti huu kwa sababu uliwezesha kuonyesha namna tamthilia inavyotumika katika kufundisha ushairi. Tamthilia kama mbinu ya kufundishia ni utanzu ambao unafundishwa katika shule za upili nchini Kenya na umezoeleka miongoni mwa wanafunzi, kwa hivyo ni utanzu ambao ulikuwa na nafasi ya kutumika kufundishia utanzu wa ushairi ambao pia umezoeleka kutumika miongoni mwa wanafunzi.

Mhimili wa tatu unaeleza kuwa, matumizi ya utanzu mwingine huwafanya wasomaji au wapokezi kuwa na ilhamu zaidi kuliko kuwapa kila wanachotarajia. Vilevile, hutia taharuki na hivyo basi, kusaidia katika kufahamu makala. Mhimili huu uliwezesha utafiti kuonyesha namna tamthilia ilivyochangia kufundisha ushairi katika shule za upili nchini Kenya. Wanafunzi waliofundishwa ushairi kwa kutumia tamthilia walikuwa na ilhamu ya kutaka kuchambua zaidi ushairi.

### 1.9 Hitimisho

Sura hii imeangazia msingi wa utafiti kwa kuweka wazi kuwa, ushairi ni utanzu ambao unafundishwa kwa kutumia mbinu kadha wa kadha. Mbinu hizi ni kama vile maelezo, kuuliza na kujibu maswali, majadiliano, mhadhara, maigizo, kazimradi, utumiaji wa kanda au santuri na

kinuruweo. Mbinu ya mwelekeo mseto inapendekezwa itumiwe katika ufundishaji wa somo la Kiswahili. Suala la utafiti huu ni kuwa, japo mbinu ya mwelekeo mseto imezingatiwa pakubwa na wataalam mbalimbali, tafiti chache zimefanywa kuhusiana na mwingiliano kati ya ushairi na tamthilia, kwa hivyo utafiti huu ulichunguza mchango wa matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa ushairi.

Aidha, malengo ya utafiti huu ni: kuchunguza namna ushairi unavyofundishwa katika shule za upili, kupambanua namna tamthilia inavyoweza kutumika kufundisha ushairi na kueleza mchango wa matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa ushairi. Umuhimu wa utafiti huu ni kuwa, utawasaidia walimu wa shule za upili kuboresha zaidi ufundishaji wa ushairi, utatoa mwelekeo mpya katika ufundishaji wa ushairi, utatoa mbinu ibuka katika ufundishaji wa ushairi, utatoa mchango katika taaluma ya elimu na lugha kwa kuongezea mbinu moja zaidi ya kufundisha, utakuwa wa manufaa kwa asasi zinazowaandaa walimu, utawafaa waandishi wa vitabu kwa kuwa utadhihirisha namna utanzu mmoja wa fasihi unavyofanikisha ufunzaji na ujifunzaji wa utanzu mwingine na utazua ilhamu ya wanafunzi katika ujifunzaji wa ushairi.

Vilevile, utafiti huu uliongozwa na nadharia ya utanzu ambayo iliasisiwa na Boas ambayo ina mihimili ifuatayo: tanzu huibua muundo wa kazi ya fasihi; matumizi ya utanzu mwingine huwafanya wapokezi au wasomaji kuwa na ilhamu na tanzu mbili zilizozoeleka zitumike kwa pamoja kwa sababu ya sifa zenye uhusiano mkubwa. Sura ya pili imeshughulikia uhakiki wa maandishi. Uhakiki huo umefanywa kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti.

# SURA YA PILI

# UHAKIKI WA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inahusu tahakiki ya maandishi. Tahakiki imefanywa kwa kurejelea malengo mahususi ya utafiti huu. Utafiti huu umewarejelea wasomi mbalimbali ambao wana mawazo tofautitofauti kuhusiana na ufundishaji wa tanzu za ushairi na tamthilia. Tahakiki kuhusu ufundishaji mseto umeshughulikiwa katika sura hii. Utafiti huu pia, umetoa maelezo kuhusu ushairi, mtindo, muundo, maudhui na mbinu za ufundishaji. Vilevile, utafiti huu umehakiki maandishi kuhusiana na namna ushairi unavyofundishwa katika shule za upili. Utafiti pia umehakiki maandishi kuhusiana na namna tamthilia inavyoweza kutumika kufundisha ushairi, na jinsi tamthilia inavyochangia katika ufundishaji wa ushairi.

## 2.2 Ufundishaji Mseto

Mwelekeo mseto ni mchakato wa ufundishaji ambao unahusu kuunganisha, kufungamanisha au kuchanganya maudhui ya masomo, mada mbili au zaidi zinazohusiana katika kipindi fulani cha mafunzo ili zichangiane na kuongezana nguvu katika matumizi ya mbinu shirikishi za ufundishaji (Opunde, h.t.). Katika karne ya 20, mbinu hii ilishabikiwa pakubwa sana na wanafalsafa kama vile Dewey na Kilpatrick (Kaur, 2019). Anaendelea kueleza kuwa, wazo la usetaji ni la kimapinduzi kwa sababu linahitaji mabadiliko makubwa katika mfumo wa elimu ya kijadi na migongano inayosababishwa na mabadiliko hayo.

Suter na Busienei (2013) walichunguza changamoto za ufundishaji na ujifundishaji wa fasihi simulizi kwa mujibu wa silabasi mpya ya mwaka wa 2002. Matokeo ya utafiti wao yalionyesha kuwa, kabla ya mwaka wa 2006, walimu hawakutilia maanani sana somo la fasihi simulizi kwa

sababu halikuwa likitahiniwa. Kulingana na wataalam hawa, walimu wa fasihi simulizi wanafaa kufanya somo la fasihi simulizi kuwa la kuvutia kwa kuhusisha mbinu bora za mawasiliano kama vile uigaji, vikundi vya majadiliano na maigizo. Wanazidi kueleza kuwa, mitagusano kati ya wanafunzi wakati wa ujifundishaji imezingatiwa kama mbinu bora ya kuwawezesha wanafunzi kuwa na umilisi wa lugha.

Kulingana na Suter na Busienei (k.h.j.), maigizo ni mbinu bora zaidi ya ufundishaji stadi simulizi kwa sababu huruhusu wanafunzi kuchangia kisimulizi katika somo. Maigizo huwaruhusu wanafunzi kutumia maneno yao katika usimulizi kwa kuhadithia, kucheza, kuimba na kutumia ipasavyo hadithi zilizorekodiwa. Wanapendekeza walimu wa Kiswahili watumie vikundi vya majadiliano wakati wanawaelekeza wanafunzi wao kujifundisha fasihi simulizi. Kulingana nao, hiyo ndiyo mbinu bora zaidi ya ufundishaji wa fasihi simulizi.

Suter na Busienei (k.h.j.) wanaongezea kusema kuwa, mwalimu wa somo la Kiswahili anastahili kuwafundisha wanafunzi wake mikakati ya ujifundishaji bora. Kulingana nao, mikakati ya ujifundishaji bora ni mbinu ambayo hulenga ufundishaji wa wanafunzi kaida za ufundishaji na ujifundishaji uliofaulu na hivyo basi, kuwezesha ukuzaji wa mikakati ya ufundishaji na ujifundishaji huo. Kwa hivyo, maoni yao ni kuwa, walimu wa fasihi simulizi wanafaa kuwasaidia wanafunzi wao kukuza mikakati yao binafsi katika ujifundishaji wao maishani; hili ni lazima litendeke wanapokuwa darasani. Vilevile, wataalam hawa wanapendekeza kuwa, walimu wa fasihi simulizi wanafaa kuwawezesha wanafunzi wao kujitegemea wakati wanapojifundisha somo la fasihi simulizi. Utafiti wao Suter na Busienei (k.h.j.) umefanana na huu kwa sababu tafiti zote mbili zinahusu namna ya kufundisha fasihi ya Kiswahili. Tofauti iliyopo ni kuwa, utafiti wao unazungumzia vifaa na mbinu za kufundishia somo la fasihi simulizi. Utafiti huu unahusu jinsi ya

kufundisha fasihi andishi hususan ushairi katika shule za upili. Aidha, utafiti huu unahusu jinsi ya kutumia tamthilia kama mbinu ya ufundishaji wa ushairi.

Omollo, Wanami na Kandagor (2017) walichunguza mitazamo ya walimu katika ufundishaji wao wa Kiswahili kwa kutumia TEHAMA. Katika utafiti wao, waligundua kuwa, baadhi ya walimu walikuwa na mitazamo hasi kuhusiana na ufundishaji wao wa Kiswahili kwa kutumia TEHAMA. Aidha, utafiti wao uligundua kuwa, walimu wengi walikuwa na mitazamo chanya kuhusiana na jinsi ya kufundisha Kiswahili kwa kutumia TEHAMA ikilinganishwa na walimu wa Kiswahili waliokuwa na mitazamo hasi. Hata hivyo, utafiti wao ulionyesha kuwa, uhusishaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa somo la Kiswahili haukuwa wa kimatendo darasani katika vyuo hivyo.

Omollo, Wanami na Kandagor (k.h.j.) wanapendekeza kuwa, Taasisi ya Ukuzaji Mitalaa nchini Kenya iratibu semina kuhusiana na ufundishaji mseto. Wanasema kuwa, semina hiyo idhihirishe namna TEHAMA inavyoweza kutumiwa kufundisha Kiswahili na hivyo basi iwe lazima kwa walimu wa Kiswahili vyuoni kutumia TEHAMA wanapofundisha Kiswahili. Wanaongezea kuwa, wale waotumia TEHAMA katika ufundishaji wa somo la Kiswahili wamotishwe. Utafiti wao Omollo, Wanami na Kandagor (k.h.j.) ni sawa na huu kwa kuwa tafiti zote mbili zinahusu usetaji katika ufundishaji wa Kiswahili. Tofauti ya utafiti wao na utafiti huu ni kuwa, utafiti wao unahusu jinsi TEHAMA inavyotumiwa katika kufundishia somo la Kiswahili kwa jumla. Hata hivyo, utafiti huu unahusu jinsi ya kutumia tamthilia kama utanzu mmojawapo wa fasihi kufundishia ushairi.

Molenje (2018) alichunguza changamoto zinazokabili ufundishaji wa silabasi mpya. Alichunza matokeo yaliyoshuka ikilinganishwa na miaka ya awali kwa kurejelea ripoti ya Baraza la Mitihani la Kitaifa nchini Kenya. Utafiti wake ulionyesha kuwa, hakuna mwalimu aliyepokea mafunzo kuhusiana na namna ya kufundisha silabasi mpya kabla ya kuitekeleza silabasi hiyo. Hii ni changamoto katika ufundishaji wa Kiswahili. Vilevile, utafiti wake ulionyesha kuwa, walimu wa

Kiswahili waliohitimu vizuri hawakuweza kuandaa masomo ya Kiswahili vilivyo na hivyo basi, kutathmini wanafunzi wao ipasavyo kwa sababu muda waliotengewa kufundisha silabasi mpya ya Kiswahili haukutosha. Mapendekezo ya mtafiti huyu ni kuwa, kozi mahususi zizinduliwe vyuoni kwa ajili ya kufundisha walimu wa Kiswahili namna ya kufundisha kwa kuzingatia usetaji.

Molenje (k.h.j.) anaendelea kueleza kuwa, mafundisho ya mara kwa mara kwa walimu yatiliwe maanani ili walimu waweze kuwa na maarifa ya kutumia mbinu mwafaka katika ufundishaji wao. Vilevile, anapendekeza kuwa, Idara ya Ukaguzi na Uhakikishaji wa Viwango Bora vya Elimu katika Wizara ya Elimu iwe ikikagua walimu wa Kiswahili mara kwa mara kwa ajili ya kuhakikisha kuwa, walimu wanatekeleza silabasi mpya ya Kiswahili vilivyo. Utafiti wake Molenje (k.h.j.) ni sawa na utafiti huu kwa kuwa tafiti zote zinahusu ufundishaji wa somo la Kswahili. Tofauti ni kuwa, utafiti wake unahusu changamoto zinazowakabili walimu wanaofaa kutekeleza silabasi ya Kiswahili iliyodurusiwa kwa jumla. Utafiti huu unahusu namna ya kufundisha ushairi kwa kutumia mbinu mahususi za ufundishaji.

Cheruto na Orodho (2016) walichunguza namna walimu walivyojiandaa kufundisha Kiswahili kwa kutumia mbinu ya ufundishaji mseto. Matokeo ya utafiti wao yalionyesha kuwa, walimu wengi wa Kiswahili hawakuwa na umilisi wa kutumia mbinu ya ufundishaji mseto katika kufundisha somo la Kiswahili na kuwa nyenzo zilizohitajika katika kufundisha kwa kutumia mbinu ya usetaji hazikupatikana kwa urahisi. Vilevile, matokeo ya utafiti wao yalionyesha kuwa, walimu hawakuwa na tatizo la kufundisha somo la lugha na fasihi. Matokeo yao pia yalionyesha kuwa, maandalizi ya mapema kwa walimu wa Kiswahili kuhusiana na ufundishaji mseto yangefaa sana. Matokeo yao vilevile, yalionyesha kuwa, maandalizi ya mapema kwa walimu yalihusu tu mbinu za ufundishaji wa Kiswahili kwa jumla, hivyo basi, walimu waliondaliwa walitumia tu mbinu hizo za ufundishaji katika kuandaa maandalizi ya masomo, maazimio ya kazi na jinsi ya

kutumia nyenzo lakini wengi wao hawakuandaliwa jinsi ya kutumia mwelekeo mseto katika ufundishaji wa somo la Kiswahili.

Kulingana na Cheruto na Orodho (k.h.j.) mbinu ya mwelekeo mseto ni mpya na changamano kwa walimu wa Kiswahili na ukweli uliopo ni kuwa, walimu wengi wa Kiswahili hawakujua namna ya kutekeleza mapendekezo ya silabasi iliyodurusiwa ya mwaka wa 2002. Mapendekezo yao ni kuwa, walimu wa Kiswahili waandaliwe vilivyo kuhusiana na matumizi ya mbinu ya ufundishaji mseto katika maandalizi yao ya mapema. Tafiti zote zinahusu usetaji katika ufundishaji wa somo la Kiswahili. Kinyume cha utafiti wao, utafiti huu unahusu ufundishaji wa utanzu wa ushairi kwa kutumia tamthilia za Kiswahili.

Gilakjani (2017) alichunguza namna teknolojia ilivyobadilisha njia za watu za kutafuta habari, kufanya utafiti na kuwasiliana na wengine kote ulimwenguni. Anasema kuwa, teknolojia imeondoa vizingiti vya kimasafa na hivyo basi, imefanya elimu ya vyuo vikuu kumfikia yeyote yule kwa uthabiti. Anahoji kuwa, usetaji wa kiteknolojia unatumiwa kwa wingi katika uelekezaji kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifundishaji. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kuwa, wanafunzi humotishwa sana kusoma lugha ya Kiingereza teknolojia inapotumika katika ujifundishaji na ufundishaji. Anaongezea kuwa, wanafunzi hujifunza kupata habari yoyote ile kupitia kwa teknolojia; mwanafunzi hupata habari zaidi kuhusiana na silabasi hasa ikizingatiwa kuwa, baadhi ya habari huenda isiwe katika vitabu vya kiada vilivyopendekezwa.

Utafiti wake Gilakjani (k.h.j.) ulidhihirisha kwamba, teknolojia ilikuza ujifundishaji kwa sababu ni kifaa kinachotoa usaidizi katika ujenzi wa maarifa kwa kuashiria maoni ya wanafunzi, uelewa wao na imani zao na kuzalisha maarifa yaliyopangwa kimsingi na wanafunzi. Mtafiti huyu aligundua kwamba, walimu walikuwa na jukumu kuu la kutumia teknolojia madarasani na hivyo basi, ni muhimu kuzingatia sana walimu katika jukumu la kutekeleza ufundishaji na ujifundishaji

kwa kutumia teknolojia. Anasema kuwa, majukumu ya wanafunzi hubadilika iwapo kuna matumizi ya teknoljia madarasani mwao; yaani majukumu ya ujifundishaji hubadilika kutoka kwa ujifundishaji tuli hadi ujifundishaji tendi kwa kutumia usetaji wa teknolojia.

Gilakjani (k.h.j,) anaongezea kuwa, vipindi hubadilika kutoka mwelekeo wa ufundishaji wa mwalimu hadi ujifundishaji wa wanafunzi. Mapendekezo yake ni kuwa, walimu wabuni maandalizi ya masomo kwa kuzingatia usetaji wa teknolojia na kuwa, vifaa hivyo vinafaa kusisitiza ufundishaji na ujifundishaji wala si kuegemea masuala ya teknolojia tu. Utafiti wake Gilakjani (k.h.j.) ni tofauti na huu kwa kuwa unahusu ufundishaji na ujifundishaji wa fasihi ya Kiingereza kwa kutumia teknolojia ilhali utafiti huu unahusu ufundishaji wa ushairi katika shule za upili hasa kwa kutumia tamthilia.

Yimwilai (2015) ameonyesha uthabiti wa mwelekeo mseto kama mbinu ya ufundishaji. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kuwa, mwelekeo mseto ilikuwa mbinu mwafaka katika ufundishaji wa somo la Kiingereza kama lugha ya kigeni. Matokeo ya utafiti wake yalionyeshwa kwa kuzingatia kufaulu kwa wanafunzi katika somo la Kiingereza kama lugha ya kigeni kwa kulinganisha mbinu zilizozoeleka na mbinu ya mwelekeo mseto. Mbinu ya mwelekeo mseto ilifaulu katika ukuzaji wa stadi zao za kuhakiki mambo. Matokeo ya utafiti wao pia yalionyesha kuwa, mbinu ya mwelekeo mseto ilifaulu katika kubadilisha mitazamo ya wanafunzi katika usomaji wa fasihi. Utafiti wake Yimwilai (k.h.j.) umelingana na utafiti huu kwa sababu tafiti zote mbili zinahusu ufundishaji mseto. Tofauti kati ya utafiti wake Yimwilai na utafiti huu ni kuwa, utafiti wake unahusu ufundishaji mseto katika fasihi ya Kiingereza ilhali utafiti huu unahusu ufundishaji wa ushairi kwa kutumia tamthilia za Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya.

Vannak (h.t) anasema kuwa, mwelekeo wa lugha kimsingi ni mwelekeo bora kwa sababu unahusu usetaji wa lugha na fasihi darasani na ni mwelekeo ambao utawasaidia wanafunzi kufikia lengo

kuu ambalo ni kuboresha maarifa na umilisi wao katika Kiingereza. Anazidi kueleza kuwa, matumizi ya mwelekeo mseto ni muhimu kwa sababu wanafunzi huangazia zaidi kufahamu fasihi. Kupitia kwa fasihi, wanafunzi hujifunza mengi kuhusiana na lugha ya Kiingereza hasa kwa kuzingatia tamathali za usemi. Tamathali za usemi ni muhimu katika ufundishaji na ujifundishaji wa fasihi katika somo la Kiingereza. Hii ni kwa sababu tamathali ni tawi la isimu ambalo linahusiana na sifa teule katika matumizi ya lugha hasa kwa kuzingatia sauti, umbo ama msamiati, zilizoundwa na watu tofautitofauti ama vikundi vya kijamii katika miktadha tofautitofauti. Mtafiti huyu anasema kuwa, tamathali za usemi zina ubora wa kutolea mifano maumbo fulani ya kiisimu katika kufanya kazi ya kupitisha ujumbe mahususi.

Utafiti wake Vannak (k.h.j.) umefanana na utafiti huu kwa sababu tafiti zote mbili zinahusu ufundishaji kwa kuzingatia mbinu ya mwelekeo mseto. Tafiti hizi zinatofautiana kwa sababu utafiti wake Vannak unahusu usetaji wa lugha na fasihi ya Kiingereza ilhali utafiti huu unahusu ufundishaji wa ushairi kwa kutumia tamthilia za Kiswahili.

Chepkemoi na Wanyonyi (2017) walichunguza matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa tamthilia za Kiswahili kama njia mojawapo ya kupalilia ilhamu na mtazamo chanya kuhusu tamthilia katika miaka ya mapema ya wanafunzi. Matokeo ya utafiti wao yalionyesha kuwa, walimu wa tamthilia za Kiswahili hawajakumbatia vilivyo usetaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa tamthilia za Kiswahili. Vilevile, matokeo ya utafiti wao yalionyesha kuwa, asilimia 100% ya walimu wanaofundisha tamthilia za Kiswahili, kwa njia moja au nyigine walipata mafunzo ya TEHAMA lakini kwa sababu ya kutotaka kukumbatia mabadiliko, ni nadra wao kutumia TEHAMA katika ufundishaji wa tamthilia za Kiswahili madarasani.

Chepkemoi na Wanyonyi (k.h.j.) wanapendekeza kuwa, walimu wafundishao tamthilia za Kiswahili wakumbatie matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wao kwa sababu ufundishaji na

ujifundishaji utaimarika wakifanya hivyo. Utafiti wao Chepkemoi na Wanyonyi (k.h.j.) umeshabihiana na utafiti huu kwa maana tafiti zote mbili zinahusu usetaji katika ufundishaji wa somo la Kiswahili. Tofauti inayodhihirika ni kuwa, utafiti wao Chepkemoi na Wanyonyi unahusu usetaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa somo la Kiswahili kwa jumla. Kwa upande mwingine utafiti huu unahusu ufundishaji wa ushairi kwa kutumia tamthilia kama mbinu ya ufundishaji.

Chepkemboi, Chemwei na Awino (2018) walichunguza changamoto zinazokabili utekelezaji wa ufundishaji mseto wa fasihi simulizi. Matokeo ya utafiti wao yalidhihirisha kuwa, utekelezaji wa ufundishaji mseto wa fasihi simulizi ulitegemea mitazamo ya wanafunzi, hivyo basi, kufaulu kwa wanafunzi kulitegemea mitazamo yao chanya. Aidha, matokeo yao yalionyesha kuwa, kulikuwa na uhusiano chanya kati ya mikakati ya uelekezaji na utekelezaji wa silabasi ya fasihi simulizi katika shule za sekondari. Kwa hivyo, kulingana nao mikakati ya uelekezaji ni muhimu katika utekelezaji wa fasihi simulizi. Maoni yao ni kuwa, umilisi wa lugha ni muhimu sana katika ufundishaji wa fasihi simulizi. Utafiti wao Chepkemboi, Chemwei na Awino (k.h.j.) umefanana na huu kwa sababu tafiti hizi mbili zinahusiana na ufundishaji mseto kama mbinu ya kufundishia. Tofauti ni kuwa, utafiti wao unahusiana na umilisi wa lugha katika ufundishaji wa fasihi simulizi ikilinganishwa na utafiti huu ambao unahusu matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa ushairi.

Achillah (2010) alichunguza iwapo walimu walikuwa tayari kutumia mbinu ya mwelekeo wa usetaji katika kufundishia msamiati; alibainisha mazoezi ya kimuktadha yaliyotumiwa katika ufundishaji pamoja na changamoto zilizojiri kutokana na mbinu ya kimuktadha. Anaendelea kueleza kuwa, kuna mbinu nyingi za ufundishaji ambazo mwalimu hustahili kuzitumia na hivyo basi, mwalimu huamua ni mbinu ipi itakayowafaa wanafunzi wake na baadaye kutathmini ufaafu wa mbinu hiyo.

Achillah (k.h.j.) anaongezea kwa kusema kuwa, kila mbinu huwa inafaa na hivyo basi, ni jukumu lake mwalimu kuteua mbinu itakayomwezesha kuyafikia malengo ya somo lake. Vilevile, anazidi kueleza kuwa, mbinu za ufundishaji huingiliana na kutegemeana; anashauri walimu kutotegemea mbinu moja tu wanapokuwa wanafundisha. Aidha, anasema kuwa, mbinu faafu hufanya ufundishaji kuwa rahisi na hivyo basi, kuwafanya wanafunzi kuelewa dhana kwa urahisi. Utafiti wake Achillah umelingana na utafiti huu kwa sababu tafiti zote mbili zimeshughulikia mbinu ya ufundishaji lakini kinyume cha utafiti wake Achillah ni kwamba, utafiti huu umeaangazia tamthilia kama mbinu ya ufundishaji wa ushairi.

### 2.3 Maelezo Kuhusu Ushairi, Mtindo, Muundo, Maudhui na Mbinu za Ufundishaji

Sehemu hii ilishughulikia ufafanuzi wa dhana muhimu zilizorejelewa mara kwa mara katika utafiti huu. Dhana hizi zilielezwa kwa mujibu wa wataalam tofautitofauti kama ifuatavyo

Njogu na Chimera (2011) wanaeleza kuwa, ushairi ni sanaa ya lugha inayoeleza jambo au wazo kwa njia ya mkato na kwa namna inayoteka hisia za msomaji au msikilizaji. Maneno ya msikilizaji huteuliwa kimakusudi ili yalete taswira maalumu akilini mwa msomaji au msikilizaji; maneno hayo hupangwa ili yatoe mdundo fulani shairi linapoimbwa, linapoghaniwa au linaposemwa.

Ushairi una historia ndefu. Shitemi (2010) anaelezea historia ya ushairi wa Kiswahili kwa kusema kuwa, historia ya ushairi wa Kiswahili ni kongwe kadri ilivyo fasihi simulizi na historia ya jamii ya Waswahili. Ameainisha historia ya ushairi wa Kiswahili katika awamu nne maalum. Awamu hizi ni: kipindi cha urasmi mkongwe, kipindi cha utasa, kipindi cha urasmi mpya na kipindi mamboleo au cha sasa. Hii ina maana kuwa, iwapo kuna mabadiliko katika ukuaji wa ushairi wa Kiswahili, kuna mabadiliko katika ufundishaji na ujifunzaji wa ushairi.

Ushairi katika shule za upili hufundishwa kwa kuzingatia vipengee kama vile mtindo, muundo na maudhui. Hakuna njia moja ya kueleza neno mtindo lakini kwa jumla mtindo unaweza kuelezwa kama tabia ya utungaji inayopambanua mtunzi mmoja na mwingine (Wamitila, 2002). Anaendelea kueleza kwamba, katika ushairi msomaji anapaswa kufahamu masuala yafuatayo: afahamu iwapo mtunzi ametumia maneno magumu, lahaja, maneno ya kale na sababu ya kumfanya kutumia maneno hayo. Anaongezea kuwa, msomaji pia anapaswa kufahamu maudhui yalioyoendelezwa na maneno ya kale. Vilevile, msomaji anashauriwa kuchunguza iwapo mwandishi amechanganya ndimi, ametumia methali na iwapo amechanganya ndimi, aonyeshe uhusiano wa kuchanganya ndimi na maudhui yake.

Wamitila (k.h.j.) anaendelea kuongezea kuwa, msomaji anapaswa kujua jinsi mishororo ilivyopangwa na kuchunguza iwapo kuna takriri (vibwagizo) na pia kujua jambo ambalo takriri hizo zinasisitiza. Msomaji pia anapaswa kujua kile kinachosemwa kuhusiana na kwapi na miloto ya shairi hilo na kuchunguza jinsi mtunzi alivyoumba utungo wake. Anazidi kueleza kuwa, msomaji anapaswa kujua namna mtunzi alivyoanzisha hoja zake, alivyoendeleza hoja zingine na alivyomalizia hoja zake.

Mlaga (2017) anasema kuwa, mtindo ni dhana inayorejelea upekee wa kazi yenyewe ama ni upekee wa mwandishi ambao unajitokeza katika kazi ya fasihi. Hii ina maana kuwa, upekee huo humtofautisha msanii wa kazi fulani na wasanii wengine. Anazidi kueleza kuwa, mtindo huweza kugawanyika katika mtindo unaoonyesha upekee kabisa wa mtu binafsi na mtindo unaoonyesha kundi fulani au namna fulani ya kuandika utanzu fulani wa fasihi. Anaongezea kwa kusema kuwa, mtindo hubainishwa kwa vipengele kama vile matumizi ya lugha (kwa mfano tamathali za usemi), usimulizi na mbinu mbalimbali za uandishi.

Kuna miundo mingi katika ushairi wa Kiswahili (Wamitila, k.h.j.). Anaendelea kueleza kuwa, vipengee vinavyotumika katika muundo ni kama vile mishororo, mizani na vina. Vilevile, anaongezea kwamba, urefu wa mishororo hutegemea idadi ya mizani na mtiririko wa mawazo iwapo shairi ni huru. Vilevile, anasema kwamba, urefu wa beti hutegemea idadi ya mistari katika kila shairi.

Wamitila, (k.h.j.) anazidi kushauri kuwa, ni muhimu kufahamu aina ya tungo, mathalani, pindu, tarbia au takhmisa. Anazidi kushauri kuwa, ni vyema kutazama idadi ya mishororo, mizani na vipande katika ubeti wa shairi. Vilevile, anasema kuwa, ni vizuri kuchunguza ruwaza (mpangilio) ambao mshairi aliutumia. Aidha, anasema kwamba, ni muhimu kuonyesha namna muundo uliotumika ulivyoingiliana na mtiririko na maana ya ushairi.

Mlaga (k.h.j.) anaeleza kuwa, kuna upekee wa muundo katika ushairi wa Kiswahili. Upekee huo ni kuwa, kila ubeti huundwa kwa mishororo kadhaa ambapo kila mshororo huwa na maana iliyokamilika kuhusiana na ubeti husika. Anazidi kuelezea kuwa, ubeti na mishororo ni vipengee muhimu katika muundo wa ushairi. Anaongezea kuwa, shairi huweza kuwa na muundo wa tamonitha, tathinia, tarbia na sabilia. Vilevile, anasema kwamba, shairi linaweza kuwa na mchanganyo wa miundo mbalimbali.

Masuala makuu ya utungo ni dhamira, lengo na shabaha (Wamitila, k.h.j.). Anaendelea kusema kwamba, masuala hayo yanapounganishwa na mtazamo wa mtunzi na kuhusishwa na muktadha, maudhui hupatikana. Vilevile, anaeleza kwamba, kwa jumla, maudhui ni mawazo ya mtunzi kwa mkabala na muktadha fulani.

Mlaga (k.h.j.) anasema kuwa, maudhui ni jumla ya mambo yote yaliyomsukuma msanii wa kazi fasihi kusana kazi yake husika. Anaorodhesha vipengele vya maudhui kama ifuatavyo: dhamira,

ujumbe, migogoro, falsafa, itikadi, msimamo na mtazamo. Anahitimisha kuwa, vipengee hivyo ndivyo huwa vinaunda jumla ya mambo ambayo huwa yanamsukuma msanii wa kazi fulani ya fasihi kusana kazi yake.

Wakati huo huo, mwalimu wa Kiswahili amependekezewa mbinu kadha wa kadha za ufundishaji wa Kiswahili. Somo la fasihi na hasa ushairi lina mbinu nyingi za kisasa za ufundishaji. Kwa mujibu wa Wanjala na Kavoi (2013) mbinu hizi ni kama vile maelezo, kuuliza na kujibu maswali, majadiliano, mhadhara, maigizo, kazimradi, utumiaji wa kanda au santuri na kinuruweo. Wanaeleza kuwa, maelezo ni mbinu ambayo hutumiwa kufafanua maneno yenye maana zaidi ya moja. Kuuliza na kujibu maswali ni mbinu ambayo inatumiwa na mwalimu kuuliza mwanafunzi swali kuhusiana na mada anayofundisha kisha mwanafunzi huyo hutarajiwa kujibu.

Wanjala na Kavoi (k.h.j.) wanaendelea kusema kwamba, majadiliano ni mbinu ambayo hutumiwa na mwalimu katika uchambuzi wa vipengele mbalimbali vya maudhui na fani katika fasihi. Mhadhara ni mbinu ambayo humfanya mwanafunzi kuwa mpokezi na msikilizaji katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji na ni nzuri kwa kufundishia fasihi. Maigizo ni mbinu ya ufundishaji ambayo mwalimu anaweza kutumia kufundishia masomo ya fasihi kwa kuwa mwalimu anaweza kuigiza hali mbalimbali zinazojitokeza katika makala ya fasihi; mwalimu anafaa kuwaeleza wanafunzi malengo ya uigizaji kabla ya kuwaruhusu kuigiza.

Wanjala na Kavoi (k.h.j.) wanafafanua kwamba, kazimradi ni mbinu ambayo mwalimu huitumia kwa ajili ya kumshirikisha mwanafunzi moja kwa moja kwa kumpa kazi ya kufanya na baadaye mwanafunzi huyo kutarajiwa kuiwasilisha kazi hiyo kwa mwalimu au darasani. Utumiaji wa kanda au santuri ni mbinu ambayo mwalimu hutumia kuandaa somo lake la fasihi kwa mfano ushairi na

kulipeperusha hewani kwa kutumia mitambo ya kielektroniki kwa wanafunzi wake. Kinuruweo ni mbinu ambayo hutumiwa pamoja na kipakatakilishi katika kufundishia masomo ya fasihi yaliyoandaliwa kwa kuyarusha ukutani kwa ajili ya kusomwa na wanafunzi.

### 2.4 Namna Ushairi Unavyofundishwa Katika Shule za Upili

Sehemu hii inahusu maandishi ya ushairi jinsi yalivyohakikiwa na wataalam mbalimbali na jinsi ambavyo uhakiki huo ulivyohusiana na utafiti huu. Uhakiki huo wa maandishi ni kama ufuatao:

Iyaya, Kobia na Luganda (k.h.j.) wamechunguza mbinu zinazotumiwa na walimu wa shule za upili nchini Kenya katika kufundisha. Mbinu hizo ni kama vile kutumia darasa zima, mbinu ya kidrama, kazimradi, mwalimu kumsaidia mwanafunzi mmoja, wageni waalikwa, mbinu nyanjani na kutumia mashindano. Matokeo ya utafiti wao yalionyesha kuwa, walimu wanaofundisha ushairi walikuwa wamefuzu vyema sana, hivyo basi, kuwa na ujuzi wa mielekeo bora katika taaluma ya ufundishaji. Vilevile, matokeo ya utafiti wao yalionyesha kuwa, walimu wengi hawakutumia mbinu zilizohitilafiana kufundisha ushairi wa Kiswahili katika shule za upili; nyenzo za kufundishia ushairi wa Kiswahili hazikuwepo na hivyo basi, hazikupatikana kwa ajili ya walimu wafundishao Kiswahili kuzitumia.

Iyaya, Kobia na Luganda (k.h.j.) waligundua kuwa, sehemu zinazowatatiza wanafunzi katika ushairi ni: istilahi na misamiati migumu inayotumiwa katika ushairi, mbinu za lugha, mtindo na kuandika shairi katika lugha nathari. Katika utafiti wao, ukosefu wa nyenzo za kutosha katika kufundishia somo la ushairi unadhihirika. Ukosefu wa nyenzo za kutosha za kufundishia huathiri ufundishaji wa somo la ushairi. Mapendekezo yao ni kuwa, walimu watumie mbinu zinazohitilafiana wafundishapo ushairi, walimu watilie maanani matumizi ya nyenzo za kufundisha ushairi na panapowezekana walimu wawahusishe wanafunzi wa ushairi kutengeneza

baadhi ya nyenzo hizo kama kazimradi. Utafiti wao ni sawa na utafiti huu kwa sababu tafiti zote zinahusu ufundishaji wa ushairi. Tofauti ni kuwa, utafiti huu unahusu namna ushairi unavyofundishwa katika shule za upili kwa kutumia mbinu kadhaa, mbinu ya ufundishaji wa ushairi kwa kutumia tamthilia ikiwemo.

Yego (2013) amebainisha matumizi ya lugha katika kuwasilisha ujumbe wa waimbaji kwa hadhira. Nyimbo za taarab hutungwa kishairi. Kupitia maudhui, ujumbe wa nyimbo unabainika. Ameonyesha kuwa, wimbo hujengwa kwa mistari ambayo hurudiwarudiwa kwa kutegemea malengo ya watendaji. Vilevile, anaelezea kuwa, kuna mistari ambayo huimbwa na watu mbalimbali na kuna mistari mahususi ambayo huimbwa na kiongozi wa kwa ajili ya kudhibiti hadhira.

Aidha, Yego (k.h.j.) anazidi kueleza kuwa, takriri katika mistari ya nyimbo ndiyo nguzo muhimu katika nyimbo za Kiafrika. Katika wimbo wa *Kibiriti Upele* ambao ameurejelea, anabainisha maudhui ya "nafasi ya mwanamke katika ndoa"; mwanamke anazo juhudi za kupinga ukandamizaji anaotendewa na mwanamume. Ujumbe mwingine ambao unathibitika katika wimbo wa *Kibiriti Upele* ni uadilifu; mwanamke anaonyeshwa kuwa mtu mwadilifu ikilinganishwa na mwanamume ambaye anamletea mkewe ugonjwa wa UKIMWI na hivyo basi, kusababisha kifo cha mkewe na hivyo basi, mwanamume huyo kubakia katika hali ya upweke. Katika wimbo wa *Tupendane Wabaya Waulizane*, ujumbe unaodhihirika ni ule wa mapenzi: inadhihirika kuwa, wanandoa (mume na mke) wanashirikiana kudhibiti ndoa yao. Ujumbe mwingine ambao unabainika ni ule wa majukumu ya mwanamke; mwanamke ameonyeshwa kama mlezi wa jamii, mwimbaji amempa mwanamke ushauri wa kumdhibiti mwanamume kupitia njia kama vile mapishi, maongezi na malezi.

Kulingana na Yego (k.h.j.) kuna matumizi ya lugha ambayo yamebainishwa katika *Kibiriti Upele* na *Tupendane Wabaya Waulizane*: Ameonyesha kuwa, lugha inayotumiwa katika nyimbo hizo mbili ni ya kumdunisha mwanamke; tamathali za usemi zinazotumiwa zinadhihirisha jinsi ambavyo mwanamke alivyodunishwa. Mathalani mwanamke analinganishwa na maua, matunda, ndege na wanyama. Tamathali za usemi ambazo zimedhihirishwa katika nyimbo hizo mbili ni kama vile tashbihi pale ambapo kuna mstari unaoonyesha namna tabia za mwanamume zilivyolinganishwa na mbwa anayezurura sokoni; mwimbaji anachukizwa na tabia za mwanamume ambaye anazurura mitaani akiwatafuta wanawake bila kujali yule aliye naye katika ndoa, hivyo basi, mwanamume huyo anayezurura anafukuzwa na wanawake. Utafiti wake Yego unabaini matumizi ya lugha katika kuwasilisha ujumbe wa waimbaji kwa hadhira ilhali utafiti huu unaeleza namna tamthilia inavyotumiwa kama mbinu ya kufundishia maudhui ya ushairi.

Nzuki (2003) amechunguza kuchangiana kwa vipengele katika kuiumba kazi nzima. Maudhui yanajitokeza na kuonyesha mchango wa vipengele vya kifani katika kuyajenga. Amehakiki namna vipengele mbalimbali vya lugha vinavyotumika katika ukuzaji wa maudhui kadha wa kadha yanayobainika katika diwani za *Mchezo wa Karata na Bara Jingine*. Mathalani ameonyesha kuwa, tashbiha nyingi hutumiwa kufananisha tabia na kukejeli watawala watukufu pamoja na raia maskini. Vilevile, ameonyesha namna taswira inavyobainika katika baadhi ya tungo zinazojitokeza katika diwani hizo mbili. Kwa mfano katika diwani ya *Mchezo wa Karata*, anabainisha taswira ya mtoto aliyepakatwa na mama yake ambayo inazua maudhui ya namna watawala wanavyofaidi kutokana na jasho la watawaliwa. Nzuki (k.h.j.) amelenga mwingiliano wa maudhui na fani katika tamthilia. Utafiti huu umeeleza namna tamthilia inavyotumiwa kufundisha mtindo na maudhui katika ushairi.

Hassan (2013) alichunguza muundo katika ushairi. Kutokana na kazi yake, anasema kuwa, muundo ni mpangilio maalum wa beti za shairi uliopangwa na msanii kwa nia ya kufikisha dhamira na maudhui mbalimbali kwa hadhira iliyokusudiwa. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kuwa, Haji Gora Haji anafuata utaratibu wa kimapokeo kutunga mashairi yake kwa mfano tarbia. Kwa upande mwingine anamwonyesha Euphrase Kezilahabi akitumia miundo ya kisasa katika kuunda mashairi yake; Kezilahabi hatilii maanani kuwa shairi ni lazima liwe na mistari minne namna Haji anavyoshikilia.

Vilevile, Hassan (k.h.j.) anaonyesha kuwa, Haji ambaye ni mshairi wa kimapokeo anajitahidi sana kutumia vina na mizani katika mashairi yake ikilinganishwa na Kezilahabi ambaye hafuati urari wa vina na mizani aandikapo mashairi yake; Kezilahabi anashikilia kuwa, si lazima shairi liandikwe kwa kuzingatia urari wa vina na mizani ndiposa liitwe shairi. Kwa upande mwingine mtafiti huyu anamwonyesha Haji akitumia kibwagizo katika baadhi ya mashairi yake ikilinganishwa na Kezilahabi anayeandika beti za ushairi wake kwa kutoziwekea kibwagizo. Utafiti wake Hassan unalinganisha na kulinganua shairi la arudhi na shairi huru. Utafiti huu unaohusu mbinu zinazotumiwa kufundisha vipengee vya ushairi kama vile muundo.

Ali (2014) alilinganisha nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala kwa ajili ya kubainisha falsafa yao juu ya mwanamke. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kuwa, mwanamke anasawiriwa kama chombo cha starehe na ndiposa mwanamke anatakiwa kumshughulikia mumewe kwa kumpokea atokapo kazini na kumwogesha. Matokeo ya utafiti wake pia yanaonyesha kuwa, mwanamke ni mpole na mnyenyekevu kwa mumewe. Mtafiti huyu aidha, anaonyesha kuwa, Shaaban Robert na Mathias Mnyampala wanamsawiri mwanamke kuwa mtu asiyepaswa hata mara moja kubishana na mumewe kuhusiana na jambo lolote lile katika

ndoa yao. Kinyume cha utafiti ule wa Ali, utafiti huu nao unahusu namna ya kufundisha maudhui ya ushairi kwa kutumia mbinu mahususi.

Indede (2008) anaelezea mwelekeo unaosema kuwa, ulimwengu unabadilika na hivyo basi, utamaduni wa ushairi ni lazima ubadilike kwa kuwa uchumi na siasa za nchi zinaendelea kubadilika. Hivyo basi, washairi wa kisasa wanaeleza kuwa, fasihi hubadilika katika umbo na maudhui na hivyo ushairi wa Kiswahili ni sharti uruhusu mabadiliko yanayotokea katika ushairi huru. Utafiti wake Indede (k.h.j.) umelingana na utafiti huu kwa sababu tafiti zote zinarejelea ushairi. Tofauti iliyoko ni kuwa, utafiti wake umejikita katika umbo la ushairi kwa ujumla ilhali utafiti huu umeshughulikia muundo, mtindo na maudhui kama vipengee vya tamthilia vinavyotumika kufundishia ushairi.

Kwa upande mwingine, Maitaria (k.h.j.) anatathmini matumizi ya methali katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Amezingatia methali katika kuainisha ushairi wa Kiswahili. Methali ni mojawapo ya tamathali za usemi, na hivyo basi, inakuwa na nafasi katika mtindo. Utafiti wake Maitaria (k.h.j.) ni sawa na huu kwa kuwa tafiti zote zinarejelea ushairi kwa ujumla na zinalenga mtindo wa uwasilishaji.  Kinyume cha utafiti wa Maitaria, utafiti huu unahusu namna mtindo katika ushairi unavyofundishwa.

Wangari (2015) alichunguza jinsi watunzi mbalimbali walivyoibuka na mikondo na mitindo mipya ya utunzi. Anarejelea diwani ya *Tunu ya Ushairi* na kutambua kuwa, watunzi wa mashairi ya arudhi hawajafuata ruwaza zilizozoeleka. Vilevile, anatambua kuwa, diwani hiyo inajumlisha mashairi ya arudhi na mashairi huru. Anasema kuwa, diwani hiyo ni changamoto kwa wahakiki kwa sababu ni lazima watathmini upya maelezo yao kuhusu dhana mbalimbali za ushairi. Hivyo basi, diwani hiyo inatoa mipaka ya awali kuhusiana na mashairi pale ambapo ushairi wa arudhi na

ushairi huru zilitenganishwa. Matokeo ya utafiti wake pia yanaonyesha kuwa, mpangilio wa maneno katika diwani hiyo ulizingatiwa; mikondo mingi ya pindu ilidhihirika katika mashairi.

Utafiti wake Wangari (k.h.j.) pia umeangazia dhana ya mpangilio wa mistari; mashairi yanayojitokeza katika diwani ya *Tunu ya Ushairi* ni yale ya mstari mmoja hadi kumi na nne ikilinganishwa na mashairi yaliyozoeleka sana kama vile tathlitha, tarbia na takhmisa. Utafiti wake Wangari (k.h.j.) na utafiti huu ni sawa kwa kuwa tafiti zote mbili zinahusu mitindo na miundo. Tofauti iliyopo ni kuwa utafiti huu unashughulikia namna ya kufundisha mtindo na muundo wa ushairi kwa kutumia mbinu mahususi za ufundishaji.

## 2.5 Namna Tamthilia Inavyoweza Kutumika Kufundisha Ushairi

Tamthilia na ushairi ni tanzu za fasihi ambazo zinafunzwa na kutahiniwa katika shule za upili, kitofauti. Licha ya tanzu hizi kufundishwa na kutahiniwa kitofauti katika shule za upili, kuna uwezekano wa tanzu hizi kutumiwa kwa pamoja kwa ajili ya kurahisisha uelewa wa wanafunzi. Kwa hivyo, sehemu hii inahusu jinsi ambavyo tamthilia inavyoweza kutumika kufundisha ushairi katika shule za upili kwa kurejelea maoni ya watafiti mbalimbali kama ifuatavyo:

Day (2014) anasema kuwa, kufundisha wanafunzi ushairi si rahisi kila mara na ndiyo maana anatumia drama kufundisha ushairi ili wanafunzi wanaopenda masimulizi hasa yanayoigizwa waweze kuelewa ushairi huu wa kimasimulizi. Anazidi kueleza kuwa, shairi la kimasimulizi aliloliteua na kulirejelea kufundishia linaonyesha namna mwanafunzi anavyoweza kuelewa usimulizi wa shairi.

Ufundishaji wa ushairi kwa kutumia drama huwawezesha wanafunzi kushiriki katika mijadala ya darasani, kubuni njia za kufanya kazi ya darasani, kubuni na kuendeleza majukumu yao na kujibu

kwa makini sana maswali kuhusiana na kazi za wengine (Day, k.h.j.). Anaongezea kwa kusema kuwa, inawezekana kutumia drama kufundishia ushairi kwa mara ya kwanza kabisa kwa lengo la kuwawezesha wanafunzi kuelewa ushairi. Wanafunzi wanashauriwa kuwa na ufahamu wa diwani ya ushairi kwanza kabla ya kushiriki uigizaji wa ushairi huo.

Mwalimu anapokuwa darasani anastahili kuwaruhusu wanafunzi kusoma shairi kwa sauti na baadaye kugawa darasa kwa vikundi vya wanafunzi wanne hadi watano (Day, k.h.j.). Baadaye, mwalimu anashauriwa kuwauliza wanafunzi wake kutambua mistari iliyotumiwa katika ushairi na ikawapendeza na vilevile, waeleze ni kwa nini walipendezwa na mistari hiyo. Anaongezea kuwa, mwalimu anafaa kutanguliza uigizaji kwa haraka pasi na kufikiria zaidi na hata bila ya kuelewa shairi linaloigizwa. Aidha, mwalimu awaambie wanafunzi kusimama kwenye duara na iwapo wanafunzi hawatasimama basi waketi kama hadhira na wawe na nafasi ya utendaji mbele yao. Baadaye mwalimu anastahili kuwaambia wanafunzi kuwa, atawasomea sehemu ya kwanza ya ushairi polepole na kila mara anaposoma, mwigizaji anasonga mbele na kuchukua nafasi yake ya uigizaji.

Day (k.h.j.) anaongezea kuwa, baada ya kusoma kila mshororo, mwalimu anastahili kuwaelekeza wanafunzi katika majadiliano kwa lengo la kuhakikisha kuwa wameelewa sehemu ya kwanza ya ushairi.kupitia maigizo. Baada ya majadiliano, mwalimu anastahili kuwaeleza wanafunzi kurejelea usimulizi wa sehemu alizowafundisha kupitia maigizo, na baadaye kuwahimiza wanafunzi kusoma na kuigiza sehemu nyingine za kitabu cha ushairi. Utafiti huu nao unahusu jinsi mwalimu anavyofundisha mtindo, muundo na maudhui katika ushairi kwa kutumia tamthilia.

Feinberg (1979) anasema kwamba, mwelekeo mseto wa ushairi unaseta mbinu za kidrama na vipengee mbalimbali vya kusoma, kuandika, kuchanganua na kukariri ushairi. Anaendelea kusema

kuwa, maendeleo katika uigizaji wa ushairi yalijiri kutokana na kutafuta njia za kuwasaidia wanafunzi wa shule za msingi na za upili kuwa na mtazamo chanya na kuchangamka wanapoambiwa kusoma au kuandika ushairi. Anaongezea kwamba, mbinu hiyo ilifaulu darasani kuanzia gredi ya nne hadi chuoni. Feinberg (k.h.j.) anaongezea kuwa, wanafunzi wanapoandaa uwasilishaji wa kuigiza ushairi katika vikundi, hawatafuti tu na kusoma mashairi bali pia wanachangamkia kuteua mistari na baadaye kuunda shairi la kipekee kwa ajili ya kuwasilisha kwa njia ya maigizo.

Aidha, Feinberg (k.h.j.) anapendekeza hatua zifuatazo katika uigizaji wa ushairi: Kwanza kabisa kuna hatua ya darasa, pale ambapo darasa linawekwa katika vikundi vya wanafunzi watano au sita kwa ajili ya kufanya maandalizi ya kusoma kwa kikundi. Katika hatua hii, uwasilishaji wa shairi kwa kutumia sauti mbalimbali na tafsiri za kimaigizo huangaziwa. Hatua ya pili ni ya kujadili maudhui yanayoweza kujitokeza katika uwasilishaji wa uigizaji wa ushairi, kupitia vitabu vya ushairi na marejeleo mengine kwa ajili ya kupata mada.

Kuhusiana na hatua ya vikundi katika ushairi unaoigizwa, Feinberg (k.h.j.) anasema kwamba, ni muhimu maudhui ya kikundi yakiteuliwa, kisha baadaye mashairi matano au sita yateuliwe kutoka kwa vitabu vya ushairi kwa ajili ya kukipa kila kikundi. Anaongezea kwamba, katika yale mashairi yaliyoteuliwa, mistari, fungu la maneno au maneno yahusishwe katika uwasilishaji. Vilevile, mwalimu anashauriwa kuseta mashairi kadhaa na kuongeza mistari ya awali kwa ajili ya kuunda shairi jipya la kikundi.

Kwa upande mwingine, Feinberg (k.h.j.) anaeleza kuwa, ni muhimu marejeleo yakiandikwa na uamuzi wa mwisho wa mpangilio wa shairi ambalo kikundi kinaliunda ufanywe. Anazidi kushauri kwamba, kila kikundi cha wanafunzi kipewe mistari mahususi. Anaongezea kuwa, uamuzi wa

miondoko ifaayo, ishara, sauti na viwango ufanywe kwa ajili ya kuwa na uwasilishaji mzuri wa uigizaji wa ushairi. Hatua inayofuatia ni ile ya wanafunzi kufanya mazoezi hadi kuwa na ujasiri wa kuwasilisha ushairi wa kuigiza. Anaongezea kwamba, hatua ya mwisho ni ile ya wanafunzi kusoma shairi la kikundi darasani na kusoma kwa kikundi katika vikundi vyao ndiposa waigize ushairi. Utafiti huu nao, unahusu jinsi ya kufundisha mtindo, muundo na maudhui katika ushairi wa Kiswahili kwa kutumia tamthilia.

Miaka ya hivi karibuni, mfumo wa elimu ya Uyunani umeendelea kuangazia elimu tendi kuliko elimu ya kinadharia tu (Tsiaras, 2016). Anazidi kueleza kuwa, mtalaa unaotambua umuhimu wa hisia, mwili na roho pamoja na akili ni wa maana sana. Kwa sababu hiyo, wataalam wengi wanatambua uwezo wa ubadilishaji wa ushairi kama mbinu ya kuendeleza utamaduni kwa kusisitiza kwamba, watoto wanastahili kufurahia kazi za fasihi ambazo zimezingatiwa pakubwa kuwa muhimu katika lugha safi. Vilevile, anasema kwamba, ushairi ulioandikwa unasaidia kuvukisha uwili wa mwili na akili na bila shaka kukuza uhai wa kiroho wa mtoto pamoja na hulka zake. Kuongezea kwa hili, anasema kuwa, miongo mingi iliyopita, wataalam wa elimu wamependelea sana michezo ya kuigiza kwa sababu husaidia watoto kukua vizuri na pia ni mbinu ya kuwamotisha watoto kukuza ishara, usanii na tabia za kiubunifu. Tsiaras (k.h.j.) anaendelea kusema kuwa, ufundishaji wa ushairi kwa kutumia drama ni muhimu kwa lengo la kukuza utendaji na uelewa na vilevile hisia na uerevu wa wanafunzi.

Matokeo ya utafiti wake Tsiaras (k.h.j.), yalionyesha kuwa, asilimia 85% ya walimu waliosailiwa walitumia mara kwa mara michezo ya kuigiza na drama za kielimu kufundisha ushairi. Anaendelea kusema kuwa, walimu wote waliosailiwa walitoa maoni chanya kuhusiana na thamani ya michezo ya kuigiza kama mbinu ya kufundishia ushairi katika elimu ya msingi. Vilevile, anasema kuwa,

darasani, uandishi wa insha hutoa nafasi kwa wanafunzi kuandika mashairi kupitia drama kama shajara za kila siku au miundo kadhaa ya uandishi.

Tsiaras (k.h.j.) aligundua kuwa, asilimia 77% ya walimu waliosailiwa waliwahimiza wanafunzi wao kuandika mashairi kwa kutumia sifa za kidrama. Aidha, anazidi kueleza kuwa, asilimia 70% ya watafitiwa wake walitumia drama kufundisha masuala kadha wa kadha kuhusiana na ushairi kwa lengo la kuwapa wanafunzi nafasi ya kukuza viwango vya juu kuhusiana na uelewa wao kuhusu majibu yao, hisia zao, ubunifu wao na uerevu wao kuhusu matini ya kidhania. Anazidi kuesema kuwa, ufundishaji wa ushairi kwa kutumia drama, uliwawezesha wanafunzi kuelewa ushairi kwa maana ilikuwa mbinu mwafaka ya ufundishaji. Vilevile, anaongezea kuwa, asilimia 70% ya wanafunzi waliotafitiwa walieleza kuwa, mbinu hiyo ilikuwa bora zaidi kwa sababu ilihusu ujifunzaji wa wanafunzi. Kinyume cha utafiti wake, huu unahusu namna ya kufundisha vipengee vya ushairi ambavyo ni mtindo, muundo na maudhui kwa kutumia tamthilia.

Ufundishaji na ujifunzaji wa ushairi wakati mwingine huwa na changamoto na hata hutamausha (Ferguson, 2014). Vilevile, anasema kwamba, kwa wanafunzi wengine, mashairi huwa na ujumbe uliofichwa ambao ni mgumu kwao kuufichua. Anaendelea kusema kuwa, itakuwa bora wanafunzi kufurahia ushairi kwa kufahamu matendo, maana na hisia za mshairi. Aidha, anasema kuwa, hilo litawezekana tu iwapo mkakati wa kutumia drama utatumiwa. Drama ni mkakati mmojawapo katika utafiti ambao unakuza uelewa wa ushairi miongoni mwa wanafunzi na huwaruhusu wanafunzi kutumia mkakati wa ufahamu.

Ferguson (k.h.j.), anatoa mikakati ifuatayo kuhusiana na uigizaji wa ushairi: Kwanza anasema kuwa, kuigiza mashairi ambayo huwa mafupi ikilinganishwa na hadithi inahitaji kutoa misamiati na jazanda kwa wingi na pia kufaragua. Mikakati hiyo ambayo walimu wanaweza kutumia kuigiza

matini ni kama vile kusoma kwa kuigiza, kusoma kwa kikundi, uigizaji wa vidole, kuhadithia na kutembea. Vilevile, anazidi kusema kuwa, teknolojia inaweza pia kutumika pale ambapo wanafunzi wanaweza kufaragua matini kwa kuongezea picha, video na sauti kwa lengo la kubuni ufasiri mpya wa mashairi kwa kutumia drama.

Usomaji wa kikundi na usomaji wa kuigiza ulitumika katika gredi ya sita mara nyingi (Ferguson, k.h.j.). Kwa kuzingatia usomaji wa kikundi, alitathmini iwapo wanafunzi kwa pamoja walisoma matini kwa sauti, aidha, katika vikundi au darasa lote. Anapendekeza kuwa, shairi liwe katika sehemu: kila mwanafunzi awe na mshororo wa kusoma au kila kikundi cha wanafunzi kiwe na ubeti wa kusoma. Anaongezea kuwa, wanafunzi wasome mara kadhaa mishororo au beti walizogawiwa. Wanafunzi wanaposoma, wasome kwa zamu mishororo waliyopewa na hata vikundi visome kwa zamu mishororo ili kuwapa wanafunzi fursa ya kuigiza sehemu mbalimbali za shairi.

Kuhusiana na usomaji wa kuigiza, Ferguson (k.h.j.) anasema kuwa, walimu wazingatie mashairi ya ngonjera kwa kuwa mashairi hayo ni rahisi kufaraguliwa kwa mchezo wa kuigizwa ambao umeandikwa. Anapendekeza kuwa, walimu wabuni au wawaalike wanafunzi kubuni mchezo wa kuigiza unaotoa muhtasari wa shairi. Vilevile, anapendekeza kuwa, walimu wawaelekeze wanafunzi kuangazia usomaji unaojieleza kwa kutumia maelezo, kiimbo na ufasaha wanapofanya mazoezi ya kuigiza na hata wanapofanya maigizo yenyewe. Anazidi kusema kuwa, kuigiza shairi kwa kutumia usomaji wa kikundi na usomaji wa kuigiza unaweza kusaidia kuongeza uelewa kwa sababu vipengee vya usimulizi kama vile sauti, uradidi na toni huweza kuathiri na kuumba uelewa wa msikilizaji anaposikiliza shairi. Kinyume cha utafiti wake, utafiti huu unahusu namna ya kufundisha mtindo, muundo na maudhui katika ushairi kwa kutumia tamthilia.

Elting na Firkins (2006) wanasema kwamba, ushairi ni rasilimali muhimu inayopatikana kwa mwanafunzi wa lugha ya Kiingereza na hivyo basi, wanashadidia kwamba, kusoma, kutafsiri na kuigiza ushairi inafaa kuwa mbinu kuu ya ufundishaji wa sifa za kipindi cha Kiingereza. Wanaongezea kwamba, hata kama ni muhimu kutambua kuwa ufahamu wa kimsingi ni muhimu katika uelewa wa ushairi, kuigiza shairi pia inaweza kuwa mbinu bunifu na ya kuchangamkiwa pale ambapo wanafunzi wa lugha ya Kiingereza wanaweza wakakuza mapokezi ya shairi.

Elting na Firkins (k.h.j.) wanahoji kwamba, katika uigizaji wa ushairi ambao una ukwasi wa lugha na viwango vingi vya maana, unaweza kutoa nafasi kwa wanafunzi wa lugha ya Kiingereza kuwa mawakala katika utunzi wa maana. Wanaongezea kwamba, hilo huwezekana vizuri ushairi ukiigizwa. Aidha, wanasema kuwa, uigizaji wa ushairi unamaanisha kukariri shairi, yaani ni uigizaji simulizi. Vilevile, wanatambua kwamba, uigizaji wa mashairi umekita mizizi Marekani, pale ambapo huwa kuna mashindano kwa ajili ya kupongeza wanaoibuka washindi. Wanasisitiza kwamba, katika mwelekeo wao wa kuigiza shairi, lengo ni kumwezesha mwanafunzi kufahamu na kutafsiri maana ya ushairi kwa njia bunifu.

Elting na Firkins (k.h.j.) wanaeleza kuwa, shairi huigizwa kwa kufuata hatua zifuatazo: Kwanza ni uteuzi wa mashairi kwa kuzingatia umilisi wa lugha ya Kiingereza wa wanafunzi. Mashairi yanayofahamika miongoni mwa wanafunzi kwa misingi ya utamaduni na mazingira wanamoishi wanafunzi yateuliwe kwa ajili ya kuigizwa. Hatua ya pili ni ya usomaji wa ushairi. Katika hatua hii, wanasema kwamba, walimu wasome ushairi kwa sauti ili kuwasaidia wanafunzi kuhusisha kinachosomwa na ulimwengu wao, na hivyo basi, kupata maana ya shairi kulingana na tajriba zao.

Hatua ya tatu ni ile ya kuunda vikundi vya uigizaji (Elting na Firkins k.h.j.). Wanaendelea kusema kwamba, katika uigizaji wa ushairi, ujifunzaji wa kijumla hushuhudiwa, na huwa kuna mtagusano

wa uso kwa uso, na ujifunzaji mzuri hutokea katika kikundi cha wanafunzi kati ya wawili na wanne. Kufaragua huwa ni hatua ya nne pale ambapo wanafunzi wanaoigiza wanaliweka shairi katika sehemu za kuigizwa (shairi liwe na wahusika na wasimulizi). Wanaongezea kwamba, wanaoigiza wanafaa kuzingatia yafuatayo: usuli, mandhari, maudhui na wahusika. Aidha, wanaeleza kuwa, hatua ya mwisho ni mazoezi na uigizaji pale ambapo waigizaji wanaunganisha mawazo yao vyema katika uigizaji. Mabadiliko ya hapa na pale kuhusiana na sauti inayostahili, ishara za uso na mwili hufanywa wakati wa mazoezi ya kuigiza ndiposa baadaye uigizaji rasmi wa ushairi utendeke. Kinyume na utafiti wao, utafiti huu unahusu jinsi ambavyo vipengee vya mtindo, muundo na maudhui katika ushairi vinavyoweza kufundishwa kwa kutumia tamthilia.

Drama na ushairi ni tukio la kusisimua katika ufundishaji wa lugha (Gasparro na Falletta, 1994). Wanaendelea kuhoji kuwa, mbinu hii ya ufundishaji huhusu mwelekeo wa uwingi hisia katika upataji wa lugha kwa kuhusisha wanafunzi wa lugha ya pili kimatendo na kihisia katika mchakato wa ujifunzaji lugha. Wanaendelea kueleza kuwa, matumizi ya ushairi kama drama katika Kiingereza kama lugha ya pili darasani huwawezesha wanafunzi kutalii isimu na vipengee vya dhana za matini yaliyoandikwa bila ya kumakinikia muundo wa lugha.

Gasparro na Falletta (k.h.j.) wanaendelea kusema kuwa, wanafunzi hutumia lugha lengwa kwa malengo mahususi ya mawasiliano. Wanazidi kueleza kuwa, wanafunzi hujaribia vipengee vya mawasiliano yasiyosimuliwa katika vipengee vya lugha ambavyo ni lugha ya mwili, kuashiria na ishara za uso pamoja na vipengee vya usimulizi ambavyo ni: kiimbo, urari wa vina, uradidi pamoja na tamathali za usemi wakati wakifasiri mashairi. Kwa kuongezea, wanasema kuwa, wanafunzi huanza kumilisi lugha na kupata ujasiri wa kutagusana nje ya darasa kwa kutumia lugha lengwa. Aidha, wanaendelea kusema kuwa, baadhi ya mashairi ni drama ndogo, na mara nyingi huandikwa

kwa njia ya dayolojia. Mashairi hayo huwa muhimu kwa kuigizwa kwa sababu ni mafupi na huwa na maudhui mepesi lakini ambayo huwa muhimu sana.

Katika kutekeleza ufundishaji wa lugha ya pili kwa kutumia ushairi kidrama, mwalimu anafaa kujengea wanafunzi usuli wa shairi kwa kuwatangulizia misamiati migumu na isiyo ya kawaida (Gasparro na Falletta, k.h.j.). Wanaongezea kwamba, baadaye mwalimu huwasomea wanafunzi shairi kwa sauti ya juu. Baada ya shairi kusomwa kwa sauti, darasa hujadili kwa pamoja. Vilevile, wanafunzi wanafaa kumsikiliza tena mwalimu anaposoma shairi. Wanaongezea kuwa, hatua inayofuata, wanafunzi husoma shairi kwa kikundi na baadaye mwanafunzi baada ya mwingine husoma shairi kwa zamu. Hatua inayofuata, huwa ya wanafunzi kujiandaa kuigiza shairi kwa kuchagua wahusika wa kuigiza na kujadili miktadha, mwangaza na maleba. Vilevile, wanasema kuwa, wanafunzi wanafaa kufanya mazoezi ya kuigiza shairi na baadaye kufaragua uigizaji wa shairi. Aidha, wanazidi kueleza kuwa, hatua inayofuata huwa ni ya wanafunzi kujaribia mitagusano ya wahusika na dayolojia, na kuwa darasa hujadili ufaraguzi huo.

Gasparro na Falletta (k.h.j.) wanapendekeza kwamba, mwalimu anayefundisha Kiingereza kama lugha ya pili anastahili kuwa na faili la ushairi ambalo lina bahari mbalimbali ya mashairi yaliyoteuliwa kwa makini sana hasa kwa kuzingatia uelewa wa lugha ya wanafunzi kwa kiwango chao cha umri na ilhamu yao. Utafiti huu nao unahusu namna ya kufundisha vipengee vya ushairi ambavyo ni mtindo, muundo na maudhui kwa kutumia tamthilia.

Vodickova (2009) anasema kuwa, mashairi ya kimasimulizi ambayo yana mgogoro ama mada ya upweke, kukataliwa ama uhusiano tata ni muhimu sana kwa sababu yanawezesha wanafunzi kuwa katika hali ambazo ni lazima watatue migogoro na kuwazia mahusiano ya watu. Anaendelea

kueleza kuwa, hayo huwezekana tu iwapo michezo ya kidrama itawezesha kujihusisha na wahusika na kuigiza kama hao na hivyo basi, hii huleta mawasiliano yaliyo ya kweli.

Wakati mwalimu anapofasiri ushairi anafaa kubadilisha kwanza mitazamo hasi ya wanafunzi kuhusiana na ushairi; kwamba ushairi ni somo ambalo linafaa kufurahiwa kwa kuzingatia hisia zinazobainika (Vodickova, k.h.j.). Anaongezea kusema kuwa, kupita kwa drama wanafunzi huwa na uhuru wa kujieleza kwa kutoa maoni yao kwa kutumia lugha ya kigeni na hivyo basi, ule 'ugumu' wa ushairi huondolewa. Anatoa mfano wa shairi ambalo linaweza kuigizwa. Shairi hilo ni: *Ni Nini Kimemtendekea Lulu?* Mwandishi wa shairi hilo ni Charles Cawley. Anasema kuwa, shairi hilo ni sahili na linaelezea hadithi ya msichana mchanga aitwaye Lulu aliyeondoka nyumbani kwao kisiri wakati wa usiku. Katika shairi hilo, mnenaji ni aidha kakake au dadake mdogo wa Lulu asiyeelewa hali hiyo lakini mamake Lulu anakataa kuelezea chochote. Haya yote yanatendeka kwa sababu ugomvi kati ya Lulu na mamake. Usiku huo, Lulu alinyakuliwa na mpenziye, na akawa amepotea. Mamake Lulu ameshindwa cha kufanya na ndiyo sababu ya kujaribu kumkinga dadake/kakake Lulu kutokana na ufahamu huo.

Kutokana na mfano wa shairi alilolitoa (Vodickova, k.h.j.), anasema kwamba, shairi hilo halikusomwa na kujadiliwa tu (jambo ambalo hutendwa mara kwa mara katika vipindi vya fasihi), lakini, kwa sababu mada hiyo inawahitaji wanafunzi kushiriki kihisia, iliigizwa kwa kuzingatia vipengee vya kidrama. Anaendelea kusema kuwa, wakati wa kufundisha shairi kwa kutumia drama, yafuatayo ni muhimu: Kusoma kimyakimya; wanafunzi wasome shairi kivyao kisha misamiati isiyoeleweka ielezwe baadaye. Vilevile, anasema kuwa, wanafunzi waulizwe maswali ya kuwasaidia kuchanganua hoja kuhusiana na wahusika na hali. Wanafunzi pia wanafaa kujua ni akina nani wanaozungumza katika shairi na watambue wahusika pamoja na matatizo yao.

Kwa mujibu wa (Vodickova, k.h.j.), uigizaji wa majukumu ni muhimu katika ushairi unaoigizwa. Akitoa mfano wa shairi lililoteuliwa kwa ajili ya kuigizwa, anasema kuwa, uigizaji wa majukumu ulifanywa katika jozi pale ambapo Afisa wa Polisi alizungumza na mamake Lulu. Anafafanua kuwa, huo ulikuwa ni uigizaji wa majukumu kwa sababu mamake Lulu alikuwa katika kituo cha polisi akielezea jinsi Lulu alivyopotea. Kwa upande mwingine, Afisa wa Polisi aliuliza maswali ambayo yalijibiwa na mamake Lulu. Vilevile, askari alimpa mamake Lulu fomu ya kujaza kuhusiana na kupotea kwake Lulu. Tofauti na utafiti wake, utafiti huu unahusu jinsi ambavyo vipengele vya mtindo, muundo na maudhui katika ushairi vinavyoweza kufundishwa kwa kutumia tamthilia.

## 2.6 Mchango wa Tamthilia Katika Ufundishaji wa Ushairi

Tamthilia ni utanzu wa fasihi ambao hufundishwa kitofauti na kutahiniwa kitofauti katika mitihani ya kitaifa ya shule za upili. Hii ni sawia na ushairi ambao hufundishwa kitofauti na kutahiniwa kitofauti katika mitihani ya kitaifa katika shule za upili. Utafiti huu unahusu jinsi ambavyo tamthilia inavyotoa mchango katika ufundishaji wa ushairi. Maoni ya watafiti wafuatao yamezingatiwa kwa lengo la kuonyesha jinsi ambavyo tamthilia imechangia ufundishaji wa ushairi katika shule za upili.

Wanyela (k.h.j.) amechunguza umuhimu wa ushairi katika kuendeleza utanzu wa tamthilia ya Kiswahili. Ameonyesha kuwa, ushairi ni mbinu mojawapo inayotumiwa na watunzi wa tamthilia kama mbinu ya kimtindo. Akichunguza tamthilia za *Amezidi*, *Mama Ee* na *Kilio cha Haki*, anaeleza kuwa, tamthilia hizo zimefuata muundo wa kuwepo na utangulizi ambao unafuata mtindo wa kishairi. Anaendelea kueleza kuwa, tamthilia hizo zina vimalizio vya kishairi. Kwa mfano, tamthilia ya *Amezidi*, ina wimbo wa mtoto asiyezaliwa, tamthilia ya *Mama Ee*, ina ngonjera na tamthilia ya *Kilio cha Haki*, ina ushairi wa Lanina. Kutokana na utambuzi huo, anaongezea kuwa,

muziki wa ushairi katika tamthilia huleta hisia za papo kwa papo lakini zaidi husisitiza na kusaidia kueleza maana ya maneno yaliyopangwa.

Kimaudhui, waandishi hutumia utanzu wa ushairi kutilia mkazo ujumbe waliokusudia (Wanyela, k.h.j.). Kuhusiana na hili, anabainisha maudhui hayo katika nyimbo za wafanyikazi katika tamthilia ya *Kilio cha Haki* na wimbo wa mzee katika tamthilia ya *Amezidi*. Kwa kuangazia lugha, anasema kuwa, tamthilia hutumia lugha ya mazungumzo kwa lengo la kuepuka urasmi ili kukuza ujumbe, kuzua hisia na kusawiri wahusika. Anazidi kueleza kuwa, lugha ilitumika kufanikisha ujumbe katika tamthilia za *Amezidi*, *Mama Ee* na *Kilio cha Haki*. Katika lugha, tamathali za usemi kama vile, tashbihi, kejeli, chuku, jazanda, taswira, urudiaji na usambamba, tashhisi, semi na methali husisitizwa katika ushairi ambao huwa katika tamthilia kwa lengo la kuleta ujumbe

Wanyela, (k.h.j.), katika kuhakiki maudhui ya ushairi katika tamthilia ya *Kilio cha Haki*, anaonyesha kwamba, mwandishi ametumia ujuzi wake wa lugha kudhihirisha maudhui ya dhuluma kwa watu wanyonge. Vilevile, anaonyesha kuwa, mwandishi amezingatia mbinu ya tauria (mchezo wa maneno kwa njia ya kishairi katika tamthilia) kudhihirisha jinsi ambavyo mwandishi husisitiza ujumbe. Anabainisha hili katika tamthilia ya *Amezidi* kwa kutoa mifano ifuatayo: ‘Huu si mwisho’, ‘Huu ni mwanzo’ na ‘mwanzo unaoanza mwisho’ ili kudhihirisha kuwa mbinu hiyo imetumiwa kudhihirisha mwanzo mpya, yaani mwanzo wa matumaini ya kulifufua bara la Afrika.

Kwa upande mwingine, (Wanyela, k.h.j.) anatumia tamtrhilia ya *Mama Ee* kuonyesha jinsi mwandishi alivyotumia ushairi kudhihirisha mapambano ya mwanamke dhidi ya imani na dhuluma za jamii. Aidha, ameonyesha jinsi mwandishi alivyotumia uradidi katika tamthilia ya *Mama Ee* kwa kuonyesha kuwa, kina ‘e’ kilirudiwarudiwa katika mishororo kama vile ‘Mpambanue apumbae’na ‘Amriye sikatae’ katika ubeti mmojawapo wa shairi lipatikanalo katika

tamthilia hiyo ya *Mama Ee*. Utafiti wake Wanyela (k.h.j.) na utafiti huu ni sawa kwa sababu tafiti zote zinahusu ushairi na tamthilia. Tafiti hizi mbili zimetofautiana kwa kuwa utafiti wake umezingatia namna ushairi unavyotumiwa katika tamthilia ilhali utafiti huu unadhihirisha jinsi ambavyo tamthilia imechangia ufundishaji wa ushairi.

Kuigiza diwani nzima ya ushairi si rahisi lakini bahari za mashairi huwa ni fupi na hivyo basi, kuwa za muhimu kwa ajili ya kuigizwa darasani wakati wa kipindi (Giebert, 2014). Anaongezea kuwa, kuigiza mashairi huwasaidia wanafunzi kufanya mazoezi ya matamshi na kiimbo. Anaendelea kuelezea kuwa, uigizaji wa mashairi miongoni mwa wanafunzi huwafanya kuwa na umilisi wa lugha ya mwili na kujieleza kisauti. Vilevile, anafafanua kuwa, uigizaji wa drama huwasaidia wanafunzi kuwa na ujasiri wa ufasaha wakati wa kuzungumza. Uigizaji huo pia hufanya kazi katika vikundi vidogo kuboresha maarifa ya kufanya kazi katika vikundi miongoni mwa wanafunzi. Anaendelea kusema kuwa, wataalam wanaoshabikia ufundishaji wa ushairi kwa kutumia drama hutoa sababu mbili za kufanya hivyo. Kwanza, wao husema kwamba, mashairi huwa mafupi na yanaweza yakapitiwa katika kipindi kimoja darasani. Vilevile, mashairi hayo yanaweza kufikiwa na wanafunzi wanaoogopa matini marefu. Mashairi hayo pia hupatikana katika njia mbalimbali yakielezea fahiwati na hisia.

Giebert (k.h.j.) anataoa sababu ya pili kwa kusema kuwa, mashairi mengi huwa na ukwasi wa maana na huelezea mawazo changamano katika lugha sahili ambayo huwa ni ya kuvutia hasa kwa wanafunzi wakubwa kiumri na wenye upeo wa juu. Vilevile, anajibu swali kwamba, ni kwa nini ushairi uigizwe? Hoja yake ya kwanza kuhusiana na swali hilo ni kuwa, ili ushairi ufurahiwe, unahitaji kusikilizwa na kuzungumzwa na wanafunzi, na wala si kusomwa tu kimyakimya. Hoja yake ya pili ni kuwa, uigizaji unaweza kufanya ushairi kufurahiwa zaidi. Anaendelea kusema

kuwa, wanafunzi wengi huwa hawapendezwi na ushairi kwa kuwa huwa ni rasmi sana. Kwa hivyo, anapendekeza kuwa, ushairi uigizwe ili wanafunzi waone kuwa ushairi unaweza kufurahiwa.

Giebert (k.h.j.) anatoa mfano wa mchezo wa kuigiza wa Shakespeare ambao una drama na ushairi, na hivyo basi, huzingatiwa kuwa mgumu kwa wazungumzaji asilia kwa sababu ya lugha changamano iliyotumika. Anazidi kuelezea kwamba, kule Ujerumani, wanafunzi wa gredi ya 11 (kumi na moja) hutanguliziwa drama na ushairi wa Shakespear katika vipindi vya Kiingereza.

Mwalimu anapofundisha drama na ushairi katika kazi za Shakespeare, anafaa kuwauliza wanafunzi waandike wanachokifahamu kuhusiana na 'penzi' au 'chuki' katika kazi ya Shakespear kwa hoja tano hadi kumi (5-10) kisha wajadili na wenzao katika vikundi vinginevyo (Giebert, k.h.j.). Anaendelea kueleza kuwa, baadaye wanafunzi wanafaa kuwekwa katika jozi mbalimbali na kuigiza dayolojia ya 'Ninakupenda'/ 'Ninakujua' katika kiimbo na lugha ya mwili kuonyesha upendo, kuachana, kukataliwa kwa mpenzi na mpenzi asiye mwaminifu kuomba msamaha. Aidha, anazidi kuelezea kwamba, maudhui ya shairi ndiyo huangaziwa sana wakati ushairi unapoigizwa. Kinyume cha utafiti wake, utafiti huu nao unahusu jinsi ambavyo tamthilia imechangia ufundishaji wa ushairi.

Taylor (1994) anaeleza kwamba, walimu huwa na changamoto wanapofundisha ushairi, na changamoto hizo hutokana na hisia ambazo walimu huwa nazo baada ya kusoma shairi. Anaongezea kwamba, changamoto za kufundisha ushairi zinaweza kukabiliwa kwa namna walimu wanavyofafanua ushairi kupitia mikakati kadha wa kadha. Anaendelea kusema kuwa, mwelekeo wa kufundisha ushairi kwa kutumia drama unatolea walimu mbinu ya kuwahusisha wanafunzi na hisia, njia ya kufanya kazi na mashairi ambayo hutumiwa kama msisimko wa kujadili au mikutano.

Taylor (k.h.j.) anatoa mfano wa shairi ambalo mada yake ni *Twaenda Kuwinda Dubu* kama shairi ambalo lina utendi. Katika shairi hilo, familia inatafuta dubu kwa moyo mkunjufu na kurejea kwa hofu wanapopata dubu mmoja. Anafafanua kuwa, shairi kama hilo likiigizwa, wanafunzi wachanga wataanza kuwa na fikra ya kile kilichotendeka. Aidha, anaongezea kwamba, uradidi kwa kuzingatia vina utafanywa kwa miondoko ambayo itawafanya wanafunzi kutambua umuhimu wa ushairi kuashiria maudhui wanapojaribu kuwazia kile kilichotendeka familia ilipokuwa ikiwinda dubu ndiposa ikarejea kwa uoga. Tofauti na utafiti wake Taylor (k.h.j.), utafiti huu unahusu jinsi ambavyo matumizi ya tamthilia yalivyochangia ufundishaji wa ushairi.

Mapunjo (2014) amechunguza dhima ya usawiri wa mhusika ambaye ni mwanamke kama kiongozi katika tamthilia. Ametafiti na kubainisha usawiri wa mhusika ambaye ni mwanamke kama kiongozi na kuonesha suala la uongozi linavyoibua visa na linavyojenga dhamira katika tamthiliya teule. Utafiti wake Mapunja umelingana na utafiti huu kwa kuwa tafiti zote mbili zinarejelea tamthilia kubainisha vipengee vya maudhui. Utafiti wake Mapunjo umetumia tamthilia kuchunguzia mwanamke kama mhusika anayeibua dhamira ya uongozi lakini utafiti huu unatumia tamthilia kama mbinu ya kufundishia vipengee vya maudhui kama vile dhamira katika ushairi.

## 2.7 Hitimisho

Katika sura hii, madhumuni ya utafiti yamebainika kupitia tafiti zilizofanywa na wataalam mbalimbali. Utafiti huu umenufaika kutokana na tafiti zilizofanywa na watafiti waliotangulia. Tafiti hizi ziliwezesha utafiti huu kuweka wazi ufanano na utofauti kati ya utafiti huu na tafiti za hapo awali. Tafiti zote zinarejelea ufundishaji, tamthilia na ushairi kwa kina lakini nyingi hazikurejelea tamthilia kama mbinu ya ufundishaji wa ushairi katika shule za upili nchini Kenya. Sura ya tatu inajadili mbinu za ukusanyaji wa data ambazo zilitumiwa katika utafiti huu. Sehemu zilizoshughulikiwa katika sura ifuatayo ni: muundo wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli na

usampulishaji, njia na mbinu za kukusanya data, uwasilishaji na uchanganuzi wa data, uhalali na uthabiti wa vifaa, maadili katika utafiti pamoja na changamoto za utafiti.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Hii ni sura inayoshughulikia yafuatayo: muundo wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za kukusanya data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data, uhalali na uthabiti wa data na maadili ya kitafiti. Vilevile, mbinu za kukusanya data na uchanganuzi wa data zimeelezwa kwa kina.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulitumia muundo wa kimfano. Kumar (2011), anasema kwamba, katika muundo wa kimfano, 'mfano' unaouteua unakuwa msingi kamilifu, jumla na wa kina wa uvumbuzi wa vipengee unavyotaka kutafitia. Aidha, anaongezea kwamba, ni mwelekeo ambao tukio fulani au mifano michache iliyoteuliwa kwa makini hutafitiwa kwa makini. Utafiti huu ulijikita katika Kaunti Ndogo ya Teso Kaskazini ambayo ina shule thelathini na hivyo basi, kuteua shule tisa zilizotumika kwa utafiti kwa kuzingatia malengo ya utafiti yaliyohusishwa na mihimili ya nadharia kama ifuatavyo :

Utafiti huu ulichunguza namna ushairi unavyofundishwa katika shule za upili. Lengo hili lilifafanuliwa kwa kuzingatia mhimili wa nadharia ya utanzu unaoshikilia kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi sana. Vilevile, utafiti huu ulipambanua namna tamthilia inavyoweza kutumika kufundisha ushairi. Lengo hili lilifafanuliwa kwa kuzingatia mhimili wa utanzu wa nadharia uelezao kuwa, tanzu mbili zilizozoeleka zitumike kwa pamoja kwa sababu ya sifa zenye uhusiano mkubwa. Utafiti huu pia ulieleza mchango wa matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa ushairi. Lengo hili lilifafanuliwa kwa kuzingatia

mhimili wa nadharia ya utanzu uelezao kuwa, matumizi ya utanzu mwingine huwafanya wasomaji au wapokezi kuwa na ilhamu zaidi kuliko kuwapa kila wanachotarajia.

### 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika Kaunti Ndogo ya Teso Kaskazini katika Kaunti ya Busia nchini Kenya. Kaunti ya Busia ina kaunti ndogo saba ambazo ni: Busia, Butula, Nambale, Bunyala, Samia, Teso Kusini na Teso Kaskazini (Rejelea Kiambatisho 4). Kaunti Ndogo ya Teso Kaskazini ina jumla ya shule thelathini (30) za upili ambazo zimegawika katika shule za wavulana, shule za wasichana na shule za mseto. Eneo hili lina shule moja ya wavulana, shule nne za wasichana na shule ishirini na tano (25) za mseto.

Eneo hili lilichaguliwa kwa sababu mtafiti kama mwalimu aliye na tajriba na ambaye alikuwa amefundisha katika eneo hili kwa muda mrefu, alikuwa amegundua kupitia kwa utangamano wake na walimu wenzake wanaofundisha eneo hilo kwamba, wana changamoto na ufundishaji wa ushairi. Aidha, wanafunzi wengi katika eneo hili wanatoka katika jamii ya wateso ambayo huwa imepakana na maeneo kama vile Teso Kusini na nchi jirani ya Uganda. Maeneo hayo yana wakazi ambao wengi wao wanatoka katika jamii ya wateso ambao ni wanilotiki, na hivyo basi, wengi wao huwa na changamoto ya kuzungumza Kiswahili ambayo ni lugha ya wabantu. Hivyo, changamoto hizi huathiri matokeo ya wanafunzi ya Kiswahili katika mitihani yao ya kitaifa.

### 3.4 Sampuli na Usampulishaji

Sehemu hii inahusu umma lengwa, sampuli na usampulishaji. Vipengee hivyo vimeshughulikiwa kikamilifu kama ifuatavyo:

### 3.4.1 Umma Lengwa

Umma lengwa ni kikundi chochote cha taasisi, watu au vitu ambavyo vina sifa zinazofanana (Ogula, 2005). Utafiti huu ulilenga taasisi ambazo ni shule za upili zipatikanazo katika Kaunti Ndogo ya Teso Kaskazini, Busia Kenya. Vilevile, utafiti huu ulishirikisha kidato cha tatu. Aidha, walimu wanaofundisha kidato cha tatu ndio walioshirikishwa katika utafiti huu.

### 3.4.2 Sampuli

Sampuli ni kundi dogo ambalo hupatikana miongoni mwa idadi ya watu (Mugenda na Mugenda, 1999). Aidha, wanaongezea kuwa, kundi hilo dogo huteuliwa kwa makini sana ili liweze kuwa kiwakilishi cha idadi ya watu walio na sifa mwafaka. Vilevile, wanasema kuwa, kila mshiriki katika sampuli hurejelewa kama mtafitiwa. Utafiti huu ulimhusisha mwalimu mmoja wa Kiswahili katika kila shule zilizoteuliwa. Hii ni kwa sababu alikuwa kiwakilishi cha walimu wengine wa Kiswahili kwa maarifa na ujuzi wa ufundishaji wa ushairi. Kidato cha tatu kiliteuliwa kwa sababu ndicho kilichokuwa kimejikita katika ufundishaji wa masomo ya ushairi na tamthilia.

### 3.4.3 Usampulishaji

Usampulishaji ni hatua, mchakato au mbinu ya kuchagua kundi dogo kutoka kwa idadi ya watu kwa lengo la kushiriki katika utafiti (Ogula, k.h.j.). Aidha, anaongezea kwamba, ni mchakato wa kuteua baadhi ya watu katika utafiti kwa njia ambayo waliochaguliwa huwakilisha kundi kubwa lililoteuliwa.

Utafiti huu ulitumia sampuli ya utabakishaji. Kwa mujibu wa Orodho (2004), sampuli ya utabakishaji hugawanya kundi zima linalotafitiwa katika vikundi vidogo vidogo kwa kutegemea sifa bainifu za kila kikundi. Shule zilizoshiriki katika utafiti ziliteuliwa kwa mbinu ya usampulishaji wa kitabaka kwa matabaka yafuatayo: shule za wavulana, shule za wasichana na shule za mseto. Sampuli ya kimakusudi ilitumiwa kuteua walimu kwa sababu hao ndio walio na

mamlaka ya kufundisha. Walimu wanaofundisha kidato cha tatu ndio waliolengwa katika utafiti huu kwa sababu walifundisha kidato ambacho kilikuwa kimejikita katika ufundishaji wa masomo ya ushairi na tamthilia.

Utafiti huu ulimlenga mwalimu mmoja katika kila shule zilizoteuliwa. Kwa mujibu wa Kothari (2004), asilimia thelathini (30%) ya sampuli itakuwa bora katika ukusanyaji wa data ambao una sampuli kubwa. Kaunti Ndogo ya Teso Kaskazini ina shule thelathini (30), hivyo basi, utafiti ulizingatia asilimia thelathini (30%) kwa kuteua shule tisa (9). Kutokana na shule zilizoteuliwa, walimu tisa (9) waliteuliwa kushiriki katika utafiti huu. Hivyo basi, shule moja (1) ya wavulana, shule tatu (3) za wasichana na shule tano (5) za mseto ziliteuliwa katika utafiti huu. Shule moja (1) ya wavulana iliteuliwa kwa sababu hii ndiyo shule ya pekee katika eneo hili kwa hivyo sampuli ya kimakusudi ilitumika kuteua shule hii. Kwa upande mwingine, sampuli ya kinasibu ilitumika kuteua shule tatu (3) za wasichana na shule tano (5) za mseto.

Tamthilia ambazo zilitumiwa katika utafiti huu ni: *Kifo Kisimani* (Mberia, 2001) iliyotahiniwa baina ya mwaka wa 2006 na 2011, *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) iliyotahiniwa baina ya mwaka wa 2012 na 2017 na *Kigogo* (Kea, 2016) ambayo ilianza kutahiniwa mwaka wa 2018 hadi sasa. Tamthilia hizi tatu ziliteuliwa kimakusudi kwa sababu ni miongoni mwa tamthilia za hivi karibuni kutahiniwa katika shule za upili nchini Kenya na zina aina ya data zilizohitajika katika utafiti huu.

### 3.5 Mbinu za Kukusanya Data

Kothari (k.h.j.) anasema kuwa, mbinu za kukusanya data ni mbinu ambazo hutumika katika uteuzi wa vifaa vya utafiti. Anazidi kueleza kuwa, mbinu za kukusanya data husaidia katika uundaji wa vifaa vya uteuzi. Utafiti huu ulikuwa wa maktabani na nyanjani.

### 3.5.1 Utafiti Maktabani

Utafiti huu ulifanywa katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Kibabii na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro. Katika maktaba, vitabu na tasnifu kuhusu mada ya utafiti vilisomwa kwa kina. Kusoma huku kuliwezesha utafiti huu kupata maandishi ya kitaaluma kuhusiana na vipengee vya mtindo, muundo na maudhui katika ushairi na vilevile, kubainisha pengo la utafiti huu. Vilevile, vitabu vitatu viteule vya fasihi katika shule za upili (tamthilia mbili zilizowahi kutahiniwa na tamthilia moja inayotahiniwa) vilizingatiwa katika utafiti huu. Tamthilia mbili zilizowahi kutahiniwa ni: *Kifo Kisimani* (baina ya mwaka wa 2006 na 2011) na *Mstahiki Meya* (baina ya mwaka wa 2012 na 2017). Tamthilia inayotahiniwa kwa sasa ni *Kigogo* (kuanzia 2018). Data kuhusu mtindo, muundo na maudhui katika ushairi zilipatikana kutoka kwa tamthilia hizo tatu kwa ajili ya kuandika sura ya nne.

### 3.5.2 Utafiti Nyanjani

Utafiti huu ulishirikisha watafitiwa ambao walikuwa ni walimu wa kidato cha tatu kwa kuwa walifundisha kidato kilichokuwa kimejikita katika ufundishaji wa masomo ya ushairi na tamthilia. Watafitiwa hawa walishiriki vema katika utafiti huu kwa sababu walijibu maswali ya usaili kikamilifu. Usaili wa watafitiwa uliongozwa na dodoso; maswali ya usaili yaliandaliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti na hivyo basi, kutoa mwelekeo uliohitajika katika utafiti huu. Kando na watafitiwa kukubali kusailiwa, walikubali pia kutoa stakabadhi zao za kitaaluma kwa ajili ya kuchunzwa. Stakabadhi zilizochunzwa ni maazimio ya kazi, maandalizi ya somo na rekodi za kazi. Vilevile, kurekodi usaili kati ya mtafiti na watafitiwa ni mbinu ambayo ilitumika katika utafiti huu kukusanya data.

#### 3.5.2.1 Usaili

Utafiti huu ulitumia mbinu ya usaili. Mtagusano kati ya mtu na mtu, aidha, uso kwa uso ama vinginevyo, kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo mahususi akilini ni usaili (Kumar, k.h.j.). Vilevile, anaongezea kwamba, kuna aina mbili za usaili; usaili wa moja kwa moja ambapo mtafiti huuliza swali na msailiwa hujibu swali hilo. Aina ya pili ni usaili wa simu ambapo mtafiti huuliza msailiwa maswali kupitia kwa simu na hivyo basi, msailiwa huyajibu maswali ya mtafiti kupitia kwa simu. Utafiti ulitumia usaili wa moja kwa moja kuwasaili walimu wanaofundisha Kiswahili katika kidato cha tatu katika eneo la Teso Kaskazini. Utafiti ulitumia mbinu hii kwa sababu iliwezesha kupata data za kutosha kuhusu ufundishaji wa mtindo, muundo na maudhui katika ushairi hususan kwa kutumia tamthilia.

Kurekodi ni mbinu muhimu katika ukusanyaji wa data kwa sababu huhakikisha kwamba, sauti za watafitiwa zinasikika na hivyo basi, data hizo ni thabiti na za kuaminika zaidi (Tesier, 2012). Vilevile, anaongezea kwamba, mbinu ya kurekodi ambayo huhusisha vifaa vya kielektroniki kama vile, kinasa sauti au video ni muhimu kwa sababu humruhusu mtafiti kusikiliza kiimbo cha watafitiwa na pia anaweza kusitisha usikilizaji wa yale yaliyorekodiwa wakati wa kuandika data. Kinasa sauti kilitumika kurekodi usaili baina ya mtafiti na watafitiwa. Usaili uliorekodiwa ulihusu jinsi ambavyo ushairi unavyofundishwa katika shule za upili, namna tamthilia inavyoweza kutumika kufundisha ushairi na mchango wa tamthilia katika ufundishaji wa ushairi. Watafitiwa walijuzwa kuwa, wanarekodiwa kwa kutumia kinasa sauti kabla ya kurekodiwa kufanyika.

#### 3.5.2.2 Uchunzaji

Kwa mujibu wa Kumar (k.h.j.) mbinu ya uchunzaji ni njia mojawapo ya kukusanya data za kimsingi. Aidha, anaendelea kuhoji kwamba, uchunzaji ni njia ya kimakusudi, kitaratibu na kichaguzi ya kutazama na kusikiliza mtagusano au tukio namna linavyotendeka. Utafiti huu

ulitumia mbinu hii kuchunza stakabadhi za walimu kama vile maazimio ya kazi, maandalizi ya somo na rekodi za kazi zilizokuwa na ithibati ya mbinu za ufundishaji wa ushairi katika eneo la Teso Kaskazini.

### 3.6 Vifaa vya Ukusanyaji Data

Kothari (k.h.j.) anaeleza kuwa, vifaa vya utafiti vinatokana na mbinu. Vifaa vilivyotumiwa kukusanya data ni dodoso, mwongozo wa kuchunza vipindi na kinasa sauti kama ifuatavyo:

#### 3.6.1. Dodoso

Dodoso ni orodha ya maswali yaliyoandikwa ambayo ni wazi au funge, maswali haya huandaliwa na msaili kwa matumizi katika mtagusano wa mtu na mtu; mtagusano huu huweza kuwa wa uso kwa uso, wa simu au wa vyombo vya kielektroniki (Kumar, k.h.j.). Katika utafiti huu, data kuhusu namna vipengee vya mtindo, muundo na maudhui katika ushairi vinavyofundishwa katika shule za upili, zilikusanywa kwa kutumia dodoso. Vilevile, dodoso ilitumika kukusanya data kuhusiana na namna tamthilia inavyoweza kutumika kufundisha vipengee vya mtindo, muundo na maudhui katika ushairi. Aidha, dodoso ilitumika kukusanya data kuhusiana na mchango wa tamthilia katika ufundishaji wa vipengele vya ushairi ambavyo ni mtindo, muundo na maudhui (Rejelea Kiambatisho 1).

#### 3.6.2 Mwongozo wa Kuchunza Vipindi

Mwongozo wa uchunzaji hutumiwa kutoa vipimo vya vipengee mahususi vya mawasiliano ya kijamii na mtagusano (Pasco, Gordon, Howlin and Charman, 2008). Vilevile, wanaongezea kwamba, hatua zinazohusiana na mwongozo wa uchunzaji huundwa kwa njia maalum ili kutumiwa pakubwa katika mandhari asili lakini yasiyokuwa na mpangilio maalum. Hii ina maana kuwa, mwongozo wa kuchunza vipindi ni mpangilio maalum wa vipengee mahususi ambavyo humwongoza mtafiti hatua kwa hatua wakati wa uchunzaji wa vipindi. Katika utafiti huu,

mwongozo wa kuchunza vipindi ulitumiwa kukusanya data kuhusiana na jinsi ushairi ulivyofundishwa kwa kuzingatia vipengee vya mtindo, muundo na maudhui (Rejelea Kiambatisho 2).

### 3.6.3 Kinasa Sauti

Umuhimu mkuu wa matumizi ya kinasa sauti katika kurekodi data ni kuwa, kinasa sauti kina kasi ya juu ikilinganishwa na jinsi mtafiti anavyoandika tu data wakati wa usaili (Tessier, k.h.j.). Data kuhusu namna vipengee vya mtindo, muundo na maudhui katika ushairi vinavyofundishwa katika shule za upili, zilikusanywa kwa kutumia kinasa sauti. Vilevile, kinasa sauti kilitumika kukusanya data kuhusiana na namna tamthilia inavyoweza kutumika kufundisha vipengee vya mtindo, muundo na maudhui katika ushairi. Aidha, kinasa sauti kilitumika kukusanya data kuhusiana na mchango wa tamthilia katika ufundishaji wa vipengele vya ushairi ambavyo ni mtindo, muundo na maudhui.

## 3.7 Utafiti Mwigo

Utafiti mwigo ni utafiti mdogo kwa ajili ya kujaribu itifaki za utafiti, vifaa vya ukusanyaji wa data, mikakati ya kuteua sampuli, na vifaa vingine vya utafiti kwa maandalizi mapana ya utafiti (Hassan, Schattner na Mazza, 2006). Aidha, wanaongezea kwamba, utafiti mwigo ni hatua mojawapo muhimu katika utafiti na hufanywa kwa ajili ya kutambua changamoto zinazonuiwa, udhaifu katika vifaa vya utafiti na itifaki kabla ya utekelezaji kamili wa utafiti.

Utafiti mwigo ulifanywa katika Shule ya Upili ya Askofu King’oo Okuleu. Sababu ya kuiteua shule hii kwa utafiti mwigo ni kuwa, inapatikana katika eneo la utafiti lililoteuliwa. Utafiti ulifanywa katika Shule ya Upili ya Askofu King’oo Okuleu kwa lengo la kupima maswali yaliyotungwa. Mwalimu mmoja alitumika kupima vifaa vya utafiti. Upimaji ulifanywa ili

kuhakikisha kuwa, data ambayo ingekusanywa ingekuwa ya manufaa kwa utafiti na ingekuwa ya kutegemewa.

Utafiti mwigo pia ulitumika kupima mbinu za kukusanya data. Mathalani, maswali katika dodoso na mwongozo wa kuchunza vipindi ambayo yalionekana kutowezesha kupata data iliyokusudiwa yalirekebishwa.

### 3.8 Uwasilishaji na Uchanganuzi wa Data

Data ilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usaili na uchunzaji. Data iliainishwa kwa misingi ya malengo ya utafiti. Data zilizopatikana kwa kutumia mbinu ya usaili na uchunzaji na ambazo zilikuwa ni za kimaelezo, zilichanganuliwa kwa kutumia maelezo na mifano; utafiti huu ulieleza namna data hizo zilivyopatikana na vilevile, kuambatisha mifano katika maelezo kuhusu data zilizokusanywa kutoka kwa watafitiwa. Data ghafi zilizopatikana zilichanganuliwa kwa kukokoteza na kisha kuwasilishwa kwa njia ya majedwali.

### 3.9 Uhalali na Uthabiti wa Vifaa

Sehemu hii inahusu uhalali wa vifaa na uthabiti wa vifaa. Vipengee hivyo vimeeelezwa kikamilifu jinsi ifuatavyo:

#### 3.9.1 Uhalali wa Vifaa

Uhalali ni usahihi na umaana wa maelekezo ambayo hujengwa kwa misingi ya matokeo ya utafiti (Mugenda na Mugenda, k.h.j.). Aidha, wanaongezea kuwa, uhalali ni kiwango ambacho matokeo yaliyopatikana kutokana na uchanganuzi wa data huwakilisha vipengee vya utafiti. Vilevile, wanaeleza kuwa, vifaa vya utafiti huhalalishwa na yaliyomo. Utafiti huu uliwashirikisha watafiti wenye ujuzi na tajriba katika Chuo Kikuu cha Kibabii hasa katika idara ya Kiswahili kwa ajili ya

kufanya marekebisho yaliyostahili na vilevile, kuhakikisha kuwa, vifaa vilivyotumiwa vilisaidia katika ukusanyaji wa data iliyokusudiwa.

### 3.9.2 Uthabiti wa Vifaa

Uthabiti ni kiwango ambacho matokeo huwa thabiti na sahihi kwa kuzingatia uwakilishaji wa idadi ya watu kijumla baada ya muda fulani, na ikiwa matokeo ya utafiti yatapatikana katika mbinu ile ile, basi vifaa vya utafiti huzingatiwa kuwa thabiti (Bashir, Afzal na Azeem, 2008). Vilevile, wanazidi kuelezea maana ya uthabiti kuwa, ni kitu kinachotegemewa kuwa kitafanya kazi siku za usoni kama kilivyofanya kazi siku zilizopita. Aidha, wanaongezea kuwa, majaribio thabiti hupima kitu kimoja mara nyingi na hutoa matokeo yale yale. Kwa hivyo, uthabiti hujengwa kwa misingi ya matokeo.

Kwa kuzingatia maelezo haya, utafiti huu ulipima maswali ya usaili kwa mtafitiwa kutoka Shule ya Upili ya Askofu King'oo Okuleu ambaye si mlengwa wa utafiti huu lakini anafanana katika viwango vya elimu na tajriba na watafitiwa wa utafiti huu, kabla ya data za utafiti kukusanywa. Dodoso iliandaliwa na baadaye kujaribiwa kwa watu waliokuwa na viwango sawa na watafitiwa kabla ya kuelekeza dodoso hiyo kwa watafitiwa halisi. Lengo la kupima dodoso lilikuwa ni kujua iwapo maswali yalifahamika kwa watafitiwa.

Vilevile, utafiti ulipima dodoso kwa sababu ya kutaka kujua iwapo taarifa zilizohitajika zingepatikana kulingana na maswali yaliyoandaliwa. Hivyo, baada ya kupima dodoso, marekebisho zaidi yalifanyiwa dodoso kabla ya kuwapa watafitiwa waliolengwa kwa ajili ya kukusanya taarifa za utafiti. Mathalani katika dodoso ya awali, maswali ya utafiti yalikuwa:

1. Unatumia mbinu gani kufundisha ushairi?
2. Ni mbinu gani nyingine unayotumia kufundishia ushairi kando na zile zilizopendekezwa?

3. Tafadhali eleza umuhimu wa mbinu uliyoipendekeza.

Maswali ya hapo juu hayangeweza kutoa data zilizohitajika kwa sababu hayakuhusisha malengo ya utafiti huu kikamilifu. Maswali hayo pia hayakuhusisha vipengele vya mtindo, muundo na maudhui namna vinavyobainika katika ushairi. Maswali hayo, kwa mfano swali la 2 na la 3, hayakudokeza tamthilia moja kwa moja kama mbinu inayoweza kutumika kufundishia ushairi. Hivyo basi, maswali hayo yalifanyiwa marekebisho kwa lengo la kuwa na dodoso faafu jinsi inavyobainika katika Kiambatisho 1.

### 3.10 Maadili Katika Utafiti

Creswell (2007) anasema kuwa, mtafiti hukumbana na masuala mengi ya kimaadili ambayo huibuka wakati wa ukusanyaji data nyanjani na wakati wa uchanganuzi na usambazaji wa ripoti. Anaendelea kusema kuwa, masuala ya kimaadili huweza kuwa katika vikundi kama vile, idhini kuhusu michakato ya utafiti. Anazidi kuhoji kuwa, upashaji wa taarifa zisizo za kweli kutoka kwa watafitiwa na usiri wa washiriki, pia huwa suala la kimaadili katika utafiti. Aidha, anaongezea kuwa, wadhamini na wafanyakazi wenza wa mtafiti; manufaa ya utafiti kwa washiriki iwapo watakumbana na hatari na maombi ya watafitiwa ambayo huzidi ukawaida wa jamii ni masuala ya kimaadili ambayo mtafiti hukumbana nayo nyanjani wakati wa utafiti.

Vilevile, Creswell (k.h.j.) anaendelea kueleza kuwa, mtafiti hukinga utambulisho wa watafitiwa (hawatambulishi) kwa mfano kwa kuwatambulisha kwa nambari au majina yasiyokuwa yao. Mtafiti hutoa mifano ambayo huashiria picha ya kijumla wala si picha halisi. Iwapo mtafiti atataka kupata uungwaji mkono kutoka kwa watafitiwa, huwa anawajuza kuwa wanashiriki katika utafiti kwa kuwaeleza malengo ya utafiti na hivyo basi kutohusika katika uongo anapofanya utafiti.

Kwa upande mwingine, Creswell (2014) anahoji kwamba, watafiti wanapaswa kukuza uaminifu wa watafitiwa na kukuza maadili katika utafiti. Aidha, anasema kwamba, mtafiti anapaswa kukinga taarifa kuhusiana na utovu wa nidhamu ambao unaweza kuibuka katika taasisi ambazo anafanyia utafiti. Mtaalam huyu pia anaongezea kuwa, mtafiti anapaswa kuvumilia changamoto zinazoweza kutukia wakati wa utafiti. Vilevile, mtafiti anashauriwa kutilia maanani maadili ya utafiti anapokusanya taarifa za kibinafsi; uhalali na uthabiti wa ripoti ya utafiti; jukumu la watafiti katika miktadha ya tamaduni nyingi na masuala ya kibinafsi hasa kupitia ukusanyaji data wa mtandao.

Utafiti huu ulizingatia michakato ya kimaadili kama ifuatavyo: Baada ya kupata barua ya idhini kutoka chuoni, barua hiyo ilitumiwa kupata kibali na barua ya idhini kutoka kwa Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi. Baada ya idhini na barua ya utafiti kutoka kwa Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi, barua ya utafiti kutoka kwa Kamishna wa Kaunti ya Busia na Mkurugenzi wa Elimu wa Kaunti ya Busia zilipatikana (Rejelea Viambatisho 15, 16, 17,18 na 19). Barua za idhini kutoka kwa Kamishna na Mkurugenzi wa Elimu katika Kaunti ya Busia zilisaidia katika utafiti huu kwa sababu zilitumiwa kufikia Walimu Wakuu wa shule zilizoteuliwa ambao waliwajuza Wakuu wa Idara na walimu wanaofundisha somo la Kiswahili katika shule za Kaunti Ndogo ya Teso Kaskazini.

Mtafiti vilevile aliondoa data ya shule yake ambayo alikuwa ameiweka hapo awali. Badala yake, aliteua shule nyingine na kuitafitia. Alifanya hivi kama njia mojawapo ya kuzingatia maadili; kutohusisha shule aliyofundisha katika utafiti wake.

Aidha, malengo ya utafiti yaliwekwa wazi kwa watafitiwa, kisha watafitiwa walijuzwa kuhusiana na haki ya hiari ya kushiriki utafiti huu. Watafitiwa walikuwa na uhuru wa kushiriki kwa hiari bila ya kulazimishwa kwa vyovyote vile. Watafitiwa walielezwa manufaa na hasara ya kushiriki na

kutoshiriki katika utafiti. Washiriki wa utafiti huu pia walisisitiziwa kuwa, hawangetambulishwa kwa majina yao halisi wakati wa kuandikwa ripoti ya utafiti. Vilevile, washiriki wa utafiti huu walihakikishiwa kuwa data zilizokusanywa zingehifadhiwa kwa siri. Watafitiwa walihakikishiwa kuwa, matokeo ya utafiti huu yangetumika tu kwa utafiti huu peke yake na wala si kwa sababu nyinginezo. Watafitiwa walifahamishwa kuwa, hakuna athari chanya au hasi ambayo ingewapata iwapo wangeamua kushiriki katika utafiti huu. Aidha, watafitiwa walijuzwa suala la utafiti, malengo ya utafiti na umuhimu wa utafiti huu.

## 3.11 Changamoto za Utafiti

Utafiti huu ulikumbana na changamoto ya usafiri; katika eneo la utafiti, barabara zilikuwa zikisakafiwa kwa hivyo mara kwa mara kulikuwa na vumbi kutoka kwa mabuldoza yaliyokuwa yakichimbua mchanga kwa ajili ya kulainisha barabara. Utafiti huu pia ulikumbana na tatizo la kutowapata watafitiwa kwa wakati ufaao; kila mara watafitiwa walikuwa wamejitahidi sana aidha kukamilisha silabasi kwa wakati ufaao au kushughulikia masuala ya michezo na tamasha za muziki. Hivyo basi, mara nyingi watafitiwa walipanga siku nyingine tofauti ya usaili.

Vilevile, utafiti huu ulikumbana na changamoto ya kurekodi data zilizopatikana, kwa mfano kinasa sauti kilichotumiwa kurekodi data kilisumbua mara kwa mara: data hazikurekodiwa inavyostahili kwa kutumia kifaa hiki. Hata hivyo, upungufu huu ulifidiwa na data zilizorekodiwa kwa kutumia kalamu na karatasi.

## 3.12 Hitimisho

Sura hii imeangazia mbinu za utafiti kwa kina. Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo. Utafiti huu ulifanywa katika Kaunti Ndogo ya Teso Kaskazini katika Kaunti ya Busia nchini Kenya na hivyo basi, kuwahusisha walimu wa Kiswahili wanaofundisha kidato cha tatu kwa sababu kidato cha tatu ndicho kilichokuwa kimejikita katika ufundishaji wa ushairi na tamthilia. Utafiti huu

ulitumia mbinu ya utabakishaji katika usampulishaji pale ambapo shule ziliteuliwa kwa misingi ya shule za wavulana, shule za wasichana na shule za mseto.

Katika ukusanyaji wa data, utafiti huu ulitumia njia ya maktabani na nyanjani kukusanya data; utafiti huu ulitumia dodoso na mwongozo wa kuchunza vipindi kukusanya data zilizotokana na mbinu ya usaili na uchunzaji mtawalia. Data za kimaelezo zilizokusanywa zilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa kutumia maelezo na mifano ilhali data za kitakwimu zilizokusanywa zilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa majedwali na asilimia.

Utafiti huu uliwashirikisha watafiti wenye ujuzi na tajriba chuoni kupima maswali ya usaili kabla ya utafiti halisi. Maadili ya utafiti yalizingatiwa kwa sababu watafitiwa waliwafahamishwa kuwa, data zilizokusanywa kwao zingehifadhiwa kwa siri. Aidha, idhini ya kufanya utafiti kwa watafitiwa ilipatikana kwanza kabla ya utafiti kufanywa. Changamoto zilizoshuhudiwa katika utafiti huu zilikuwa kama vile, matatizo ya usafiri, watafitiwa kutopatikana kwa urahisi na vilevile, tatizo la kurekodi data. Sura inayofuata inawasilisha na kuichanganua data.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Utafiti huu ulichunguza namna tamthilia inavyotumika kufundisha ushairi katika shule za upili nchini Kenya. Ushairi ni utanzu mmojawapo wa fasihi ambao unafundishwa katika shule za upili nchini Kenya kwa kutumia mbinu tofauti tofauti. Kwa hivyo, utafiti huu ulikuwa wa maktabani na nyanjani.

Utafiti ulichunguza namna ushairi ulivyofundishwa katika shule za upili, hivyo basi, watafitiwa tisa walisailiwa kuhusiana na namna tamthilia inavyoweza kutumiwa kufundisha ushairi na mchango ambao tamthilia imetoa katika ufundishaji wa ushairi. Utafiti huu ulitumia tamthilia tatu kwa ajili ya kutoa maelezo na mifano kudhihirisha kuwa tamthilia ilikuwa mbinu muhimu katika kufanikisha ufundishaji wa ushairi kwa shule za upili nchini Kenya. Tamthilia hizo zilikuwa ni: *Kifo Kisimani*, *Mstahiki Meya* na *Kigogo*.

Watafitiwa walielezea mbinu tofauti tofauti walizozitumia kufanikisha ufundishaji wa ushairi, na waliposailiwa iwapo tamthilia ingefanikisha ufundishaji wa ushairi walitoa majibu tofauti tofauti kuashiria kuwa, tamthilia ingefanikisha ufundishaji wa ushairi namna ambavyo imewasilishwa katika sura hii.

Utafiti ulitumia maelezo, mifano, majedwali na asilimia kuwasilisha data kutoka maktabani na nyanjani. Utafiti ulizingatia mada zifuatazo katika uchanganuzi na uwasilishaji wa data zilizokusanywa: namna ushairi unavyofundishwa katika shule za upili, namna tamthilia inavyoweza kutumika kufundisha ushairi na mchango wa matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa ushairi.

### 4.2 Namna Ushairi Unavyofundishwa Katika Shule za Upili

Ushairi hufundishwa kwa kurejelea vipengele maalum kama vile mtindo, muundo na maudhui.

#### 4.2.1 Mtindo

Watafitiwa tofautitofauti walieleza namna ambavyo walifundisha utanzu wa ushairi kwa kuzingatia kipengee cha mtindo. Mbinu kadha wa kadha zilidhihirika katika ufundishaji wa mtindo jinsi ilivyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

##### 4.2.1.1 Namna mtindo wa ushairi unavyofundishwa katika shule za upili

| **Namna ya ufundishaji** | **Idadi ya watafitiwa** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Maigizo | 8 | 89% |
| Maswali na majibu | 6 | 67% |
| Kazimradi | 6 | 67% |
| Majadiliano | 5 | 56% |
| Vikundi vya majadiliano | 7 | 78% |
| Kanda au santuri | 4 | 44% |
| Kukariri | 7 | 78% |
| Kinuruweo | 2 | 22% |
| Maelezo | 6 | 67% |
| **Jumla ya walimu** | **9** | **100%** |

Utafiti huu ulibaini kuwa, asilimia kubwa ya watafitiwa (89%); watafitiwa wanane (8) kati ya tisa (9) walitumia maigizo kufundisha mtindo wa ushairi (Rejelea Kiambatisho 11 na Kiambatisho 14). Watafitiwa hawa walitumia maigizo hasa kufundisha mtindo wa shairi la ngonjera. Watafitiwa

hawa walitumia wanafunzi kuigiza shairi la ngonjera pale ambapo wanafunzi waliwekwa katika makundi mawili ya kuigiza. Kando na kutumia maigizo katika kufundishia bahari ya ngonjera, maigizo pia yalitumiwa kufundishia tanzu zingine za ushairi kama vile nyimbo, mashairi huru na bahari za mashairi ya arudhi.

Katika mtindo, watafitiwa walisema kuwa, maigizo yalifaa kwa sababu wanafunzi wanapata wanachofundishwa kwa urahisi kwa sababu waliigiza na hivyo basi, kubakia akilini mwao. Tamathali ya usemi kama vile, takriri ambayo ilirejelewa sana na watafitiwa ilieleweka kwa urahisi sana kupitia maigizo darasani. Wanafunzi wanapoigiza, baadhi ya maneno, mishororo pamoja na vina hurudiwarudiwa na hivyo basi, wao huvihifadhi akilini na hivyo basi, kuelewa utanzu wa ushairi ipasavyo ikilinganishwa na kusoma tu utanzu huu.

Taswira ambayo ni picha inayojengeka akilini wakati wa kusoma kazi fulani ya fasihi au kuona kazi fulani ya fasihi ikiigizwa, ilifanikishwa na maigizo. Watafitiwa ambao ni walimu walisema kuwa, maigizo yalifanikisha ufundishaji wa ushairi kwa sababu wanafunzi waliweka kile ambacho walikisoma katika maigizo na hivyo basi, ufafanuzi kuhusu taswira kueleweka zaidi.

Matokeo yalionyesha kuwa, stakabadhi za kitaaluma kama vile maandalizi ya somo, maazimio ya kazi na hifadhi za kazi, zilikuwa na maigizo kama mbinu ya ufundishaji. Hii inafungamana na mawazo ya nadharia ya utanzu, mhimili wa kwanza (Bakhtin, k.h.j.) kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi sana. Hii ni kwa sababu kupitia maigizo wanafunzi walielewa kwa urahisi kile ambacho kilikuwa kinafundishwa kwa kutumia mbinu ya maigizo.

Matokeo haya yametofautiana na matokeo yake Nzuki (k.h.j.) anapoonyesha kuwa, vipengele mbalimbali vya lugha vinatumika katika ukuzaji wa maudhui kadha wa kadha. Katika matokeo

yake, tashbiha nyingi zinatumika kwa ajili ya kufananisha tabia na kukejeli watawala watukufu pamoja na raia maskini. Matokeo hayo hayajahusisha mbinu ya maigizo katika ufundishaji wa vipengee mbalimbali vya lugha vinavyotumika katika ukuzaji wa maudhui.

Asilimia 67% ya watafitiwa (sita) walitumia mbinu ya maswali na majibu kufundisha mtindo katika ushairi (Rejelea Kiambatisho 7). Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, mbinu ya maswali na majibu ilifaa sana katika kufundisha ushairi kwa sababu baada ya utanzu wa ushairi kuwasilishwa darasani kwa njia ya kusoma au kughaniwa, mwalimu aliwauliza wanafunzi maswali kuhusu mtindo kwa lengo la kuthibitisha iwapo wanafunzi walitambua mtindo katika ushairi husika. Mwalimu aliwauliza wanafunzi iwapo walitambua tamathali za usemi kama vile methali, misemo, nahau na tashbihi katika utanzu wa ushairi uliowasilishwa darasani. Wanafunzi wakijibu sawasawa, basi mwalimu alihakikishiwa kuwa, mbinu hiyo ya ufundishaji ilifaulu. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, mbinu ya ufundishaji ambayo ni ya maswali na majibu ilitumika na hivyo basi, kupata matokeo namna inavyodhihirika katika jedwali 4.2.1.1.

Matokeo haya yameoana na nadharia ya utanzu, mhimili wa kwanza (Bakhtin, k.h.j.) unaoeleza kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi sana. Hii ina maana kuwa, kupitia maswali ya mwalimu wanafunzi walielewa kwa urahisi mtindo wa ushairi kwa sababu walimudu kujibu walimu kile ambacho walikuwa wanakifahamu kuhusiana na mtindo wa ushairi. Matokeo haya ya utafiti yamelingana na matokeo yake Yego (k.h.j.) anapobainisha matumizi ya lugha katika kuwasilisha ujumbe wa waimbaji kwa hadhira.

Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, mbinu ya kazimradi ilitumiwa katika ufundishaji wa mtindo katika utanzu wa ushairi (Rejelea Kiambatisho 10). Watafitiwa sita (6) kati ya watafitiwa tisa (9) ambao ni aslimia 67% walitumia mbinu ya kazimradi kufundisha mtindo katika utanzu wa ushairi.

Watafitiwa hawa waliwapa kazi wanafunzi kuhusu mtindo wa ushairi. Kila mwanafunzi alitakiwa kufanya kazi kuhusu mtindo kwa wakati fulani. Kwa mfano, wanafunzi walitarajiwa kuwasilisha kazi zao baada ya wiki moja. Wanafunzi walipewa utanzu mmojawapo wa ushairi kwa mfano bahari ya ukawafi kisha wakaelekezwa aidha kutambua, kueleza ama kujadili matumizi ya lugha yaliyojitokeza katika utanzu huo wa ushairi. Mbinu hii iliwafaa wanafunzi sana kwa sababu iliwasaidia kuelewa zaidi utanzu wa ushairi.

Matokeo haya yanahusiana na nadharia ya utanzu, mhimili wa kwanza (Bakhtin, k.h.j.) kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi sana. Mbinu ya kazimradi iliwafaa wanafunzi sana kwa sababu iliwasaidia sana wanafunzi kuelewa kwa urahisi mtindo wa ushairi kwa sababu wenyewe walitafiti na baadaye kuwasilisha kazi hizo kwa walimu wao kwa ajili ya kutuzwa na kurekebishwa pale ambapo hawakupata.

Hali hii inahusiana na ugunduzi wao Iyaya, Kobia na Luganda (k.h.j.) wanapochunguza kwamba, kazimradi ni mbinu ya ufundishaji iliyotumiwa na walimu kufundisha ushairi. Waligundua kwamba, kazimradi ni mbinu muhimu katika ufundishaji wa ushairi kwa ujumla wake.

Utafiti huu ulibaini kuwa, majadiliano ni mbinu ya ufundishaji wa mtindo katika ushairi (Rejelea Kiambatisho 8). Majadiliano ni mbinu iliyotumiwa na watafitiwa watano (56%) kufundisha mtindo katika ushairi. Watafitiwa hawa walitumia majadiliano katika kipindi cha dakika arubaini darasani kufundisha ushairi. Waliibua mjadala miongoni mwa wanafunzi kuhusu mtindo uliotumiwa na mwandishi kuandika ushairi husika. Mathalani wanafunzi walijadili tamathali za usemi zilizotumiwa na mwandishi wa shairi huru au shairi la arudhi. Tamathali za usemi kama vile istiari, sadfa na tasfida zilitambuliwa na kujadiliwa.

Aidha, wanafunzi walijadili umuhimu wa tamathali za usemi katika utanzu husika wa ushairi kwa maelekezo yake mwalimu. Hii inakubaliana na nadharia ya utanzu, mhimili wa kwanza (Bakhtin, k.h.j.) kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi sana. Kupitia kwa majadiliano kama mbinu ya ufundishaji, wanafunzi wanagundua kuwa, tamathali za usemi ambazo zinapatikana katika utanzu wa semi katika fasihi simulizi zinatumika katika utanzu wa ushairi na hivyo basi, kuwezeshwa kuelewa kwa urahisi mtindo wa ushairi.

Hali hii inaakisi hali yake Maitaria (k.h.j.) anapotathmini matumizi ya methali katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Amezingatia methali katika kuainisha ushairi wa Kiswahili kwa kusema kwamba, methali ni mojawapo ya tamathali za usemi, na hivyo basi, inakuwa na nafasi katika mtindo.

Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, vikundi vya majadiliano vilitumiwa kama mbinu ya ufundishaji wa utanzu wa ushairi (Rejelea Kiambatisho 8). Watafitiwa saba ambao ni asilimia 78% walitumia mbinu ya vikundi vya majadiliano kufundisha mtindo wa utanzu wa ushairi. Kinaya, taswira, balagha, methali, jazanda, nahau na misemo ni tamathali za usemi zilizofundishwa katika ushairi pale ambapo watafitiwa waliwaweka wanafunzi wao katika vikundi vidogo vya majadiliano kwa ajili ya kujadili tamathali za usemi. Walimu waliwaweka wanafunzi katika vikundi vya wanafunzi wasiozidi watano kwa ajili ya kufanikisha majadiliano, kisha waliwapa kazi kuhusu tamathali za usemi ama mbinu za uandishi. Wanafunzi walijadili tamathali hizo namna zinavyojitokeza katika utanzu husika wa ushairi. Baada ya wanafunzi kujadili mbinu za uandishi zilizobainika katika utanzu husika wa ushairi, waliwasilisha kazi zao darasani.

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya utanzu unaoeleza (Bakhtin, k.h.j.) kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi sana, unaoana na maoni ya

watafitiwa. Vikundi vya majadiliano ni mbinu iliyowafaa wanafunzi kwa sababu waliweza kuelewa kwa urahisi sana mtindo katika ushairi wa Kiswahili.

Matokeo haya yanakubaliana na matokeo yake Achillah (k.h.j.) anaposema kuwa, kila mbinu huwa inafaa na hivyo basi, ni jukumu lake mwalimu kuteua mbinu itakayomwezesha kuyafikia malengo ya somo lake. Aidha, hali hii inahusiana na na hali yake Achillah (k.h.j.) anapozungumzia jinsi mwalimu anavyoweza kuteua mbinu fulani kwa ajili ya kufanikisha ufundishaji wake.

Utafiti huu ulibaini kuwa, watafitiwa wanne (44%) walitumia mbinu ya kanda au santuri kufundisha ushairi (Rejelea Viambatisho 7 na 9). Watafitiwa hawa walitumia vifaa hivi vya kielektroniki kufundisha pale ambapo walitumia nyimbo zilizorekodiwa katika vifaa hivi kwa ajili ya kufundisha kipera cha nyimbo kinachopatikana katika utanzu wa ushairi. Baadhi ya watafitiwa hawa walirekodi shairi lilоghaniwa katika kanda au santuri kisha wakaandaa somo la ushairi na kuliwasilisha somo hilo darasani. Mbinu za uandishi na tamathali za usemi zilidhihirika katika nyimbo au mashairi yaliyorekodiwa.

Vilevile, utafiti ulibaini kuwa, nyimbo na mashairi yaliyokuwa na wingi wa tamathali za usemi na mbinu za uandishi yaliteuliwa na hivyo basi, kurekodiwa. Utafiti ulibaini kuwa, mbinu hii ya ufundishaji ilichangamkiwa sana na wanafunzi. Kwa njia hii, ilifanikisha somo la ushairi. Kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya utanzu (Bakhtin, k.h.j.) kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi sana, maoni ya watafitiwa yalizingatiwa kwa sababu kupitia kwa kanda, mbinu za uandishi na tamathali za usemi ambazo hupatikana katika tanzu zingine za fasihi zilitambuliwa katika utanzu wa ushairi. Hivyo basi, wanafunzi walielewa kwa urahisi sana mtindo wa ushairi kupitia kanda za nyimbo

zilizowasilishwa darasani kwa sababu walifurahia kusikiliza nyimbo hizo darasani na hivyo basi, kuweza kutambua mtindo wa ushairi.

Matokeo haya ya utafiti yamekinzana na yake Yego (k.h.j.) anapoangazia namna lugha ilivyotumika kumdunisha mwanamke. Hivyo basi, tamathali za usemi katika nyimbo hizo zimetumika kwa ajili ya kuonyesha namna mwanamke alivyodunishwa katika jamii. Ugunduzi wake kuhusu namna lugha inavyotumika kumdunisha mwanamke katika nyimbo za taarab haujahusisha kanda au santuri kama mbinu ya ufundishaji.

Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kuwa, kukariri ni mbinu ya ufundishaji iliyotumiwa na watafitiwa saba (78%) kufundisha mtindo katika ushairi. Watafitiwa hawa walisema kuwa, walitumia mbinu hii kufundisha kwa kuteua utanzu wa ushairi uliokuwa na wingi wa tamathali za usemi au mbinu nyingi za uandishi. Baadaye waliwaambia wanafunzi wao kukariri utanzu wa ushairi. Wanafunzi walifurahia kukariri utanzu wa ushairi, na walipoulizwa maswali kuhusiana na mtindo katika ushairi walijibu ipasavyo kwa kuwa walikuwa wamekariri utanzu wa ushairi waliopewa na mwalimu wao.

Nadharia ya utanzu, mhimili wa kwanza (Bakhtin, k.h.j.) inaeleza kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi sana. Hii ina maana kuwa, mbinu ya kukariri ilikuwa bora katika ufundishaji kwa sababu wanafunzi wanapofurahia kukariri mashairi darasani inakuwa rahisi sana kwao kuelewa kwa urahisi mtindo wa mashairi wanayoyakariri. Utafiti huu umetofautiana na utafiti waka Indede (k.h.j.) anapoeleza kuwa, ulimwengu unabadilika na hivyo basi, utamaduni wa ushairi ni lazima ubadilike kwa kuwa uchumi na siasa za nchi zinaendelea kubadilika. Kwa hivyo, ushairi wa Kiswahili ni sharti uruhusu mabadiliko; haya yanayotokea katika ushairi huru. Utafiti wake Indede (k.h.j.) umetofautiana na

utafiti huu kwa kuwa hauhusishi ufundishaji wa mtindo katika ushairi kwa kuzingatia mabadiliko ya ushairi yanayotokana na mabadiliko ya kiuchumi na kisiasa.

Utafiti ulionyesha kuwa, watafitiwa wawili (2) ambao ni asilimia 22% walitumia kinuruweo kufundisha mtindo katika ushairi. Watafitiwa hawa walieleza kuwa, kabla ya kuingia darasani waliandaa somo kuhusu mtindo wa ushairi kisha walitumia vipakatakilishi pamoja na kinuruweo kufundisha mtindo katika ushairi. Hii ina maana kuwa, watafitiwa hawa walitumia mashairi yaliyosheni mtindo kabla ya kuyaweka katika vipakatakilishi, baadaye waliyarusha hayo mashairi pamoja na mtindo uliobainishwa kutokana na mashairi hayo ukutani. Wanafunzi walifurahia mbinu hii ya ufundishaji wa ushairi kwa sababu maandishi yaliambatanishwa na sauti. Hii ina maana kuwa, wanafunzi hao walisaidiwa kuelewa zaidi utanzu wa ushairi.

Maoni ya watafitiwa hawa yalikubaliana na nadharia ya utanzu, mhimili wa kwanza (Bakhtin, k.h.j.) kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi sana. Kupitia kwa kinuruweo, wanafunzi waliwasilishiwa tamathali za usemi ambazo zinapatikana katika tanzu zingine za fasihi lakini zimebainika katika utanzu wa ushairi, na hivyo basi, kuwezeshwa kuelewa zaidi mtindo wa mashairi. Ugunduzi wa Omollo, Wanami na Kandagor (k.h.j.) unaonyesha kuwa, walimu wengi walikuwa na mitazamo chanya kuhusiana na jinsi ya kufundisha Kiswahili kwa kutumia TEHAMA. Kinyume na utafiti wao, huu umeonyesha jinsi walimu walivyotumia kinuruweo kufundisha mtindo katika ushairi wa Kiswahili.

Maelezo ni mbinu ya ufundishaji wa mtindo wa ushairi iliyotumiwa na watafitiwa sita (67%) (Rejelea Kiambatisho 9). Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, maelezo yalifaa katika ufundishaji wa tamathali za usemi na mbinu za uandishi kwa sababu mwalimu alieleza maana na umuhimu

wa tamathali za usemi na mbinu za uandishi kama vile takriri, methali, kinaya, tasfida, sadfa, nahau na misemo namna zinavyojitokeza katika tanzu mbalimbali za ushairi.

Matokeo haya ya utafiti yalioana na nadharia ya utanzu, mhimili wa kwanza (Bakhtin, k.h.j.) kwamba, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi sana. Kupitia kwa maelezo kama mbinu ya ufundishaji, tamathali za usemi pamoja na mbinu za uandishi ambazo hupatikana katika tanzu zingine za fasihi, zilibainika katika utanzu wa ushairi, na hivyo basi, kuwawezesha wanafunzi kuelewa kwa urahisi mtindo wa ushairi. Hali hii ni tofauti na hali yake Wangari (k.h.j.) anapoangazia dhana ya mpangilio wa mistari na kubaini jinsi ambavyo diwani ilivyo na upya wa mpangilio wa mistari ikilinganishwa na diwani za awali. Hata hivyo, ugunduzi wake Wangari (k.h.j.) umetofautiana na huu kwa kuwa hauhusishi mbinu ya maelezo katika ufundishaji wa mpangilio wa mistari katika diwani za awali.

### 4.2.2 Muundo

Watafitiwa mbalimbali walieleza namna walivyofundisha muundo wa ushairi kama ilivyowasilishwa katika jedwali lifuatalo:

#### 4.2.2.1 Namna muundo wa ushairi unavyofundishwa katika shule za upili

| **Namna ya ufundishaji** | **Idadi ya watafitiwa** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Kukariri | 5 | 56% |
| Maigizo | 5 | 56% |
| Kazimradi | 4 | 44% |
| Vikundi vya majadiliano | 4 | 44% |
| Majadiliano | 4 | 44% |
| Maswali na majibu | 6 | 67% |

| | | |
|---|---|---|
| Maelezo | 7 | 78% |
| Mhadhara | 3 | 33% |
| Kinuruweo | 2 | 22% |
| **Jumla ya walimu** | **9** | **100%** |

Utafiti ulibaini kuwa, kukariri utanzu wa ushairi ni mbinu iliyotumika kufundishia muundo wa ushairi; hili lilibainika kwa kuwasaili watafitiwa kuhususiana na mbinu ya ufundishaji wa ushairi; wasailiwa watano (56%) waliwaambia wanafunzi wao kukariri shairi na kwa kufanya hivyo, waliweza kutambua muundo wa ushairi. Mizani, vina, mishororo, vipande na beti za shairi zilibainika wakati ambapo wanafunzi walikuwa wanakariri mashairi. Watafitiwa waliwaelekeza wanafunzi kukariri mashairi kisha baadaye wakawaambia kutambua mizani, vina, mishororo, vipande na beti zilizopatikana katika shairi husika.

Nadharia ya utanzu, mhimili wa kwanza (Bakhtin, k.h.j.) unaeleza kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi. Matokeo haya ya utafiti yanaafiki maelezo ya nadharia hii. Hii ni kwa sababu kupitia kukariri kama mbinu ya ufundishaji, muundo wa ushairi ulibainika na kueleweka kwa urahisi miongoni mwa wanafunzi. Matokeo haya yamelingana na yake Indede (k.h.j.) anapoelezea kubadilika kwa mashairi kimaumbo jinsi ulimwengu unavyobadilika kiuchumi na kisiasa.

Maigizo ni mbinu iliyotumiwa na watafitiwa watano kati ya watafitiwa tisa (56%) kufundishia muundo wa shairi (Rejelea Kiambatisho 11). na Kiambatisho 14. Watafitiwa hawa waliteua mashairi ya ngonjera na malumbano kisha waliwaelekeza wanafunzi wao kuigiza mashairi hayo mbele ya darasa. Baada ya kuigiza, watafitiwa ambao ni walimu waliwaambia wanafunzi wote darasani kutambua mizani, vina, beti, vipande na mishororo katika mashairi yaliyoigizwa.

Wanafunzi waliweza kutambua muundo wa shairi husika kwa kuwa waliigiza au waliwatazama wenzao wakiigiza darasani. Utafiti ulibaini kuwa, maigizo ni mbinu ya kufundishia utanzu wa ushairi kwa sababu ilijitokeza katika stakabadhi za kitaaluma kama vile maazimio ya kazi, maandalizi ya somo na hifadhi ya kazi.

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya utanzu (Bakhtin, k.h.j.) unafafanua kwamba, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fashi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi sana. Kwa kuzingatia nadharia hii inagundulika kuwa, mizani, vina, beti, vipande na mishororo vilieleweka kwa urahisi miongoni mwa wanafunzi kwa sababu viliigizwa. Hali hii imelingana na ugunduzi wao Iyaya, Kobia na Luganda (k.h.j.) wanapoeleza kwamba, mbinu ya kidrama inafaa katika kufundishia ushairi wa Kiswahili katika ujumla wake kwa kutumia nyenzo mwafaka.

Kazimradi ni mbinu ya ufundishaji wa ushairi iliyotumiwa na watafitiwa wanne kati ya watafitiwa tisa (44%) waliosailiwa katika kufundisha muundo wa ushairi (Rejelea Kiambatisho 10). Watafitiwa hawa walisema kuwa, waliwaelekeza wanafunzi wao kutambua na kujadili muundo wa utanzu wowote wa ushairi aidha kwa kuteua utanzu huo kimakusudi na kuwaambia waujadili au kwa kuwaambia wanafunzi wao kutafuta utanzu wowote wa ushairi kisha watambue na kujadili beti, mizani, mishororo, vina na vipande vilivyotumika katika utanzu huo wa ushairi. Watafitiwa hawa waliwapa wanafunzi wao makataa ya kufanya kazi hiyo. Kazi hiyo ilifanywa aidha na mwanafunzi binafsi au katika vikundi. Baada ya mwalimu kusahihisha kazi za wanafunzi aliwarejeshea kwa ajili ya kurekebisha pale ambapo wanafunzi hawakuelewa. Wakati mwingine watafitiwa walisema kuwa, kazimradi iliwasilishwa mbele ya darasa aidha katika vikundi au kila mwanafunzi aliwasilisha kazi yake kuhusu muundo wa utanzu wa ushairi darasani.

Matokeo haya ya utafiti yamehusiana na mhimili wa nadharia ya utanzu (Bakhtin, k.h.j.) unaoeleza kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fashi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi. Kupitia kazimradi, wanafunzi waliibua muundo wa ushairi maktabani na kuuelewa kwa urahisi wakiwa pekee na baadaye wakiwa na mwalimu. Matokeo haya yamekinzana na matokeo yake Hassan (k.h.j.) anapoangazia muundo wa ushairi kwa kuzingatia mistari ya waandishi wawili. Mtunzi mmoja ni wa kimapokeo ambaye anazingatia vina na mizani katika mistari anayotunga, na mwingine ni wa kimapinduzi ambaye hazingatii vina na mizani katika mistari anayotunga. Ugunduzi wake Hassan (k.h.j.) ni tofauti na matokeo haya kwa sababu haujahusisha muundo wa ushairi na mbinu ya kazimradi katika ufundishaji.

Vikundi vya majadiliano ni mbinu ya ufundishaji iliyotumiwa na watafitiwa wanne kati ya watafitiwa tisa (44%) kufanikisha ufundishaji wa muundo wa ushairi (Rejelea Kiambatisho 8). Wasailiwa hawa wanne walisema kuwa, waliwaweka wanafunzi katika vikundi vidogo vya majadiliano (wanafunzi watano hadi sita) kisha waliwapa zoezi kuhusiana na muundo wa ushairi. Wanafunzi hao walijadili vipengee vya muundo wa ushairi kama vile vina, mishororo, mizani, beti na vipande. Watafitiwa hawa walisema kuwa, vikundi vya majadiliano vilikuwa bora kwa kuwa kila mwanafunzi alionekana akishiriki kikamilifu katika majadiliano. Baada ya wanafunzi kujadili vipengee vya muundo wa ushairi husika waliwasilisha kazi zao darasani kwa ajili ya kuhakikisha majibu yao; pale ambapo walipata jibu sahihi walipongezwa na pale walipokosea walisahihishwa.

Matokeo hayo ya utafiti yamelingana na nadharia ya utanzu, mhimili wa kwanza (Bakhtin, k.h.j.) unaoshikilia kwamba, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fashi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi. Kupitia vikundi vya majadiliano, watafitiwa waliwaelekeza wanafunzi kuelewa muundo wa ushairi kwa urahisi kwa sababu wanafunzi wenyewe waligundua vipengee kadha wa kadha kupitia vikundi vya majadiliano. Matokeo haya ya utafiti yanakubaliana na matokeo yake

Wangari (k.h.j.) anapoonyesha kuwa, mpangilio wa maneno katika diwani hiyo ulizingatiwa; mikondo mingi ya pindu ilidhihirika katika mashairi. Mikondo hiyo ya mashairi ilikuwa na miundo mbalimbali.

Utafiti ulibaini kuwa, watafitiwa wanne kati ya watafitiwa tisa (44%) walitumia majadiliano darasani kama mbinu ya kufundishia muundo wa ushairi (Rejelea Kiambatisho 8). Watafitiwa waliandaa mashairi mahususi yaliyokuwa na muundo wa ushairi kwa kuzingatia vipengee kama vile idadi ya mishororo, vina vya ndani na vina vya nje, mizani, vipande na beti kisha walizua mjadala darasani ili wanafunzi wajadili umuhimu wa vipengee vya muundo darasani. Wanafunzi walijadili vipengee vya muundo darasani kwa kuelekezwa na walimu wao ambao ni watafitiwa katika utafiti huu. Wanafunzi walitambua na kujadili muundo wa ushairi husika kwa maelekezo yake mwalimu. Mbinu hii ya ufundishaji ilikuwa muhimu sana kwa sababu wanafunzi waligundua wenyewe namna utanzu wa ushairi unavyotungwa na watunzi mbalimbali kwa njia ya kujadili.

Nadharia ya utanzu, mhimili wa kwanza (Bakhtin, k.h.j.), unashikilia kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi sana ilioana na matokeo haya. Mhimili wa nadharia hii ya utanzu ulizingatiwa kwa sababu muundo wa ushairi uliibuliwa darasani miongoni mwa wanafunzi waliokuwa wakijadili na hivyo basi, kusaidiwa na walimu wao kuuelewa muundo huo wa ushairi kwa urahisi. Hali hii imetofautiana na hali katika matokeo yake Wangari (k.h.j.) anayetambua kuwa, mshororo au mishororo huunda beti za ushairi. Hii ni tofauti na utafiti huu unaohusu muundo kuonyesha namna muundo huo unavyofundishwa.

Asilimia 67%, watafitiwa sita kati ya watafitiwa tisa walitumia mbinu ya maswali na majibu kufundisha muundo wa utanzu husika wa ushairi (Rejelea Kiambatisho 7). Watafitiwa walipokuwa darasani walikuwa wamejiandaa kufundisha utanzu wa ushairi kwa kuteua tungo zilizohusiana na

utanzu huo. Watafitiwa hawa walisema kuwa, baada ya kuwawasilishia wanafunzi utanzu wa ushairi, waliwauliza wanafunzi kutambua na kujadili beti, mizani, mishororo, vina, vibwagizo, vimalizio na vipande, kisha wanafunzi waliwajibu namna walivyoelewa. Wanafunzi vilevile, waliwauliza walimu wao kuwafafanulia vipengee hivyo vya muundo wa ushairi. Mbinu hii ilikuwa kama kipimo cha kutambua iwapo wanafunzi walielewa muundo wa utanzu wa ushairi; ni mbinu iliyofaa sana katika kipindi cha dakika arubaini darasani.

Matokeo haya yameafikiana na nadharia ya utanzu, mhimili wa kwanza (Bakhtin, k.h.j.) kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fashi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi. Kupitia kwa walimu kuwauliza wanafunzi wao maswali kuhusiana na muundo wa ushairi, ilikuwa ni mbinu ya kupima iwapo wanafunzi walielewa kigezo cha muundo. Wanafunzi walipojibu sahihi basi lilikuwa dhihirisho kuwa, walielewa muundo wa ushairi. Hii ina maana kwamba, matumizi ya maswali na majibu ilikuwa ni mbinu nzuri ya kuwasaidia wanafunzi kuelewa muundo wa ushairi kwa urahisi. Matokeo haya ya utafiti yamelingana na ugunduzi wake Hassan (k.h.j.) anapomsawiri Haji kama mwandishi anayefuata kanuni za utunzi kuumba muundo wa mashairi yake ikilinganishwa na Kezilahabi asiyefuata kanuni za kimapokeo kuumba muundo wa mashairi.yake.

Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, watafitiwa saba kati ya watafitiwa tisa (78%) walitumia mbinu ya maelezo kufundishia muundo wa ushairi (Rejelea Kiambatisho 6). Watafitiwa walieleza maana ya istilahi kama vile muundo, beti, vina (vina vya ndani na vya nje), mishororo, mizani, vipande, kibwagizo, na kimalizio. Baadaye waliwawasilishia wanafunzi wao mashairi yaliyokuwa na vipengee vya muundo. Watafitiwa hawa pia walisema kuwa, waliwaruhusu wanafunzi wao kueleza kile ambacho walikielewa kuhusiana na muundo wa ushairi; wale walioeleza sahihi walipongezwa na wale ambao walipotoka walirekebishwa na kuhimizwa kuendelea kujaribu

kueleza istilahi nyingine zilizohusiana na muundo wa ushairi. Watafitiwa pia walisema kuwa, waliandaa maswali yaliyohitaji majibu ya kueleza kimakusudi tu ili wanafunzi waweze kueleza na hivyo basi, kuelewa sawa sawa muundo wa ushairi.

Matokeo haya ya utafiti yameoana na nadharia ya utanzu, mhimili wa kwanza (Bakhtin, k.h.j.) unaoeleza kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fashi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi. Kupitia maelezo kama mbinu ya ufundishaji, muundo wa ushairi ulieleweka sawasawa miongoni mwa wanafunzi kwa sababu istilahi muhimu katika muundo wa ushairi zilielezwa kwa undani. Hali hii imekinzana na hali yake Indede (k.h.j.) anaposema kwamba, namna maumbo yanavyobadilika, ndivyo miundo hubadilika. Hii ni kwa sababu hakuhusisha mbinu ya maelezo katika utafiti wake.

Mhadhara kama mbinu ya ufundishaji, ilitumiwa na watafitiwa watatu kati ya watafitiwa tisa (33%) kufundishia muundo wa ushairi (Rejelea Kiambatisho 7). Watafitiwa (hawa watatu waliposailiwa na mtafiti) walisema kuwa, walifundisha vipengee vya muundo kama vile vina, mizani, beti, mishororo, vipande, vibwagizo na vimalizio kwa kuhadhiri. Watafitiwa walihadhiri huku wanafunzi wakiandika nukuzi kutokana na mhadhara uliotolewa na mwalimu. Watafitiwa hawa walisema kuwa, mbinu hii ya ufundishaji iliwafaa kwa sababu iliwawezesha kukamilisha silabasi kwa muda ufaao na pia iliwafanya wanafunzi kumakinika darasani wakati mwalimu akifundisha. Watafitiwa hawa pia walisema kuwa, mbinu hii iliwafanya wanafunzi kutafiti zaidi kuhusiana na kile ambacho mwalimu alifundisha darasani kuhusiana na muundo.

Nadharia ya utanzu, mhimili wa kwanza (Bakhtin, k.h.j.), inayofafanua kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fashi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi inakubaliana na matokeo haya. Mhadhara kama mbinu ya kufundishia muundo wa ushairi ilikuwa mwafaka

kuwasaidia wanafunzi kufahamu muundo wa ushairi kwa urahisi kwa sababu walikuwa makini kuandika nukuzi za mwalimu aliyekuwa akiwaeleza kwa undani kuhusiana na vipengee vya muundo wa ushairi. Hali hii imetofautiana na hali katika utafiti wake Yego (k.h.j.) anapoonyesha kuwa, mistari huchangia kuundwa kwake muundo wa shairi. Hii ni kwa sababu hajahusisha mhadhara kama mbinu ya ufundishaji wa mistari ambayo huchangia kuundwa kwake muundo wa shairi.

Utafiti ulibaini kuwa, asilimia 22% ya watafitiwa ambao ni sawa na watafitiwa wawili kati ya watafitiwa tisa walitumia kinuruweo kufundishia muundo wa ushairi. Watafitiwa hawa waliandaa somo la ushairi mapema kwa kutumia kipakatakilishi ambacho kiliunganishwa kwa kinuruweo kisha kurusha somo lililoandaliwa ukutani. Somo lililoandaliwa lilihusu vipengee vifuatavyo vya muundo: beti, vina, mizani, mishororo, vibwagizo na vimalizio. Vipengee hivi vya muundo vilitokana na tanzu mbalimbali za ushairi zilizoandaliwa kwenye kipakatakilishi na kisha kurushwa ukutani. Wasailiwa hawa walisema kuwa, somo lililoandaliwa kupitia kinuruweo liliwavutia sana wanafunzi, na hivyo basi, vipengee vya muundo wa ushairi vilifundishika vema zaidi.

Kulingana na nadharia ya utanzu, mhimili wa kwanza (Bakhtin, k.h.j.), tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fashi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi. Matokeo haya ya utafiti yanalingana na nadharia hiyo. Hii ni kwa sababu, kupitia kinuruweo kama mbinu ya ufundishaji, muundo wa ushairi ulieleweka miongoni mwa wanafunzi kwa urahisi kwa sababu kinuruweo kilikuwa kifaa cha kielektroniki kilichochangamkiwa na wanafunzi darasani ambacho kilionyesha muundo wa ushairi ulioandaliwa na walimu wao sawasawa. Matokeo haya yamelingana na ugunduzi wao Chepkemoi na Wanyonyi (k.h.j.) wanapoeleza kwamba, matumizi ya TEHAMA

katika ufundishaji ni muhimu kwa sababu huwafanya wanafunzi kufurahia somo la Kiswahili hasa wanapofundishwa tamthilia.

### 4.2.3 Maudhui

Matokeo ya utafiti kuhusiana na namna maudhui katika ushairi yalivyofundishwa yaliwasilishwa katika jedwali lifuatalo:

#### 4.2.3.1 Namna maudhui katika ushairi yanavyofundishwa katika shule za upili

| **Namna ya ufundishaji** | **Idadi ya watafitiwa** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Maelezo | 7 | 78% |
| Mhadhara | 7 | 78% |
| Kazimradi | 3 | 33% |
| Vikundi vya majadiliano | 4 | 44% |
| Majadiliano | 5 | 56% |
| Maigizo | 5 | 56% |
| Maswali na majibu | 7 | 78% |
| Kinuruweo | 1 | 11% |
| **Jumla ya walimu** | **9** | **100%** |

Utafiti ulibaini kuwa, watafitiwa saba kati ya watafitiwa tisa (78%) walitumia mbinu ya maelezo kufundisha vipengele vya maudhui katika ushairi kama vile dhamira, falsafa ya mwandishi, msimamo wa mwandishi, mgogoro na funzo. Vipengee hivi vya maudhui havikubainishwa sana bali vilitokea kwa jumla tu kama maudhui. Watafitiwa walieleza maudhui namna yalivyobainika katika utanzu wa ushairi. Vilevile, watafitiwa walitambua maudhui katika mashairi teule na

kuwahimiza wanafunzi wao kueleza kwa kina kulingana na uelewa wao. Mbinu hii ya ufundishaji ilipendelewa na watafitiwa kwa sababu iliwasaidia kuafikia malengo ya ufundishaji katika kipindi cha dakika arubaini jinsi ilivyoratibiwa katika shule zao husika. Vilevile, mbinu hii ilikuwa bora kwa watafitiwa kufafanua vipengele vya maudhui kwa urahisi; maana na sababu za mtunzi kudokeza vipengee vya maudhui katika kazi yake ya ushairi zilieleweka kwa urahisi miongoni mwa wanafunzi.

Kwa mujibu wa nadharia ya utanzu, mhimili wa kwanza (Bakhtin, k.h.j.), tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi sana. Kupitia mbinu ya maelezo, wanafunzi walielezwa vipengee vya maudhui na hivyo basi, kusaidiwa kuelewa kwa urahisi maudhui yaliyobainika katika mashairi kwa urahisi sana. Hali hii imeafikiana na ugunduzi wake Nzuki (k.h.j.) anapodhihirisha jinsi vipengee vya maudhui na fani vinavyochangiana, hasa namna maudhui yanavyojengwa kwa kuzingatia vipengee vya fani.

Wasailiwa saba kati ya tisa (78%) walitumia mbinu ya mhadhara kufundishia maudhui katika utanzu wa ushairi. Vipengee vya maudhui vilifundishwa kwa njia ya kuhadhiri. Watafitiwa waliteua bahari mbalimbali za mashairi ambazo walizitumia kuelezea namna maudhui yalivyojitokeza. Mbinu hii ya ufundishaji ilipendelewa na watafitiwa kwa sababu iliwasaidia kuafikia malengo ya ufundishaji katika kipindi cha dakika arubaini. Vilevile, mbinu hii iliwasaidia watafitiwa kukamilisha silabasi kwa wakati ufaao kulingana na maazimio ya kazi. Mbinu hii ya ufundishaji pia iliwafanya wanafunzi kuwa makini darasani mwalimu alipokuwa akiwafundisha na hivyo basi, kuwachochea kusoma zaidi kuhusiana na maudhui katika utanzu wa ushairi na pia kuhakikisha kuwa, istilahi zilizotajwa zilielezwa na mwalimu wakati wa kuhadhiri.

Matokeo haya ya utafiti yamelingana na nadharia ya utanzu, mhimili wa kwanza (Bakhtin, k.h.j.) kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi sana. Mbinu ya mhadhara iliwafanya wanafunzi kuwa makini darasani na hivyo basi, kutafiti zaidi kuhusiana na istilahi ambazo hawakuwa wanazielewa wakati wa mhadhara. Hii iliwawezesha wanafunzi kuelewa kwa urahisi sana maudhui katika ushairi kwa sababu walikuwa makini darasani na baadaye kutafiti istilahi zile ambazo hawakuwa wanazielewa. Matokeo haya yamekinzana na ugunduzi wake Nzuki (k.h.j.) anapoonyesha jinsi vipengele mbalimbali vya lugha vilivyotumika katika ukuzaji wa maudhui kadha wa kadha. Hii ni kwa sababu hajahusisha mhadhara kama mbinu ya ufundishaji na vipengee vya lugha vilivyotumika katika ukuzaji wa maudhui kadha wa kadha jinsi utafiti huu unavyofanya.

Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, kazimradi ni mbinu ya ufundishaji iliyotumika kufundisha maudhui katika tanzu mbalimbali za ushairi. Watafitiwa watatu kati ya tisa (33%) waliwapa wanafunzi wao mashairi teule yakiambatana na maswali kuhusiana na namna maudhui yalivyodokezwa na watunzi wa mashairi hayo. Watafitiwa hawa waliwapa wanafunzi wao makataa ya kuwasilisha kazi zao. Watafitiwa walizisahihisha kazi za wanafunzi wao kisha walizirejesha darasani kwa ajili ya kuwarekebisha wanafunzi waliopotoka. Mbinu hii ya ufundishaji iliwafaa watafitiwa kwa sababu iliwasaidia kubainisha uelewa wa wanafunzi kuhusu maudhui katika tanzu mbalimbali za ushairi.

Matokeo haya yanakubaliana na nadharia ya utanzu, mhimili wa kwanza (Bakhtin, k.h.j.) unaoeleza kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi sana. Kupitia kazimradi, wanafunzi walifanya utafiti wa kina maktabani kuhusiana na maudhui yanayopatikana katika mashairi mbalimbali na hivyo basi, kuwezeshwa kuyaelewa kwa

urahisi sana. Hali hii imefanana na matokeo yake Ali (k.h.j.) anapotathmini maudhui ya nafasi ya mwanamke katika diwani za Shaaban Robert na Mathias Mnyampala.

Utafiti ulibaini kuwa, vikundi vya majadiliano ilikuwa mbinu iliyofaa kufundishia maudhui katika utanzu wa ushairi. Wasailiwa wanne kati ya wasailiwa tisa (44%) walitumia vikundi vya majadiliano kufundishia maudhui katika ushairi. Wasailiwa hawa waliwaweka wanafunzi katika vikundi (kila kikundi kilikuwa na wanafunzi wanne au watano) kwa ajili ya kujadili maudhui yaliyokuwa katika mashairi yaliyoteuliwa na mwalimu. Baada ya kujadili wanafunzi waliwasilisha kazi zao darasani kwa ajili ya kuthibitishwa na mwalimu. Watafitiwa hawa walieleza kuwa, mbinu hii ya utafiti ilifaa kufundishia maudhui katika utanzu wa ushairi kwa sababu wanafunzi walimakinika zaidi walipokuwa wakijadili na hivyo basi, yale yaliyofundishwa kubakia akilini zaidi; hii ina maana kuwa, somo la ushairi lilieleweka zaidi kupitia mbinu hii ya vikundi vya majadiliano.

Kulingana na nadharia ya utanzu, mhimili wa kwanza (Bakhtin, k.h.j.), tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi sana. Kupitia vikundi vya majadiliano, wanafunzi walimakinika kwa ajili ya kufahamu maudhui katika mashairi mbalimbali na hivyo basi, hiyo ikawa mbinu mwafaka ya kuwafanya wanafunzi kuelewa kwa urahisi sana maudhui yanayopatikana katika mashairi mbalimbali. Matokeo haya yametofautiana na matokeo yake Yego (k.h.j.) anapodhihirisha jinsi ambavyo aina ya maudhui yanavyodhihirika katika nyimbo za taarab. Hii ni kwa sababu vikundi vya majadiliano kama mbinu ya ufundishaji, haikuhusishwa katika kubainisha maudhui katika nyimbo za taarab jinsi utafiti huu unavyofanya.

Utafiti ulibaini kuwa, majadiliano ni mbinu ya ufundishaji iliyotumiwa na wasailiwa watano kati ya wasailiwa tisa (56%) kufundishia maudhui katika utanzu wa ushairi. Watafitiwa waliandaa

somo la ushairi mapema kuhusu maudhui katika ushairi kisha waliibua mjadala darasani; wanafunzi walitambua maudhui katika utanzu wa ushairi waliopewa kisha walijadili maudhui hayo darasani. Wanafunzi walinolewa makali yao kuhusiana na maudhui katika tanzu mbalimbali za ushairi kupitia majadiliano kama mbinu ya ufundishaji.

Matokeo haya ya utafiti yameoana na nadharia ya utanzu, mhimili wa kwanza (Bakhtin, k.h.j.) kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi sana. Kupitia majadiliano kama mbinu ya ufundishaji, wanafunzi waligundua jinsi ya kubainisha maudhui katika mashairi mbalimbali kwa urahisi sana kwa sababu wanafunzi walijadiliana namna ya kupata maudhui katika mashairi mbalimbali na hivyo basi, kuwa rahisi kwao namna ya kutambua maudhui hayo kwa urahisi, na hivyo basi, kuelewa kwa urahisi mada inayohusu maudhui katika ushairi. Hali hii imeafikiana na ugunduzi wake Ali (k.h.j.) anapobaini maudhui katika diwani.

Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, maigizo ni mbinu ya ufundishaji iliyotumiwa na watafitiwa watano kati ya watafitiwa tisa (56%) kufundishia maudhui katika utanzu wa ushairi. Maigizo yalitumiwa sana kufundishia bahari ya ngonjera na malumbano. Watafitiwa waliwaweka wanafunzi katika makundi mawili ili kuigiza shairi la ngonjera; kila kundi lilijibizana na kundi lingine katika shairi la ngonjera au shairi la malumbano. Maudhui katika mashairi ya malumbano yalidhihirika wakati ambapo wanafunzi walipokuwa wakiigiza; watafitiwa walihakikisha kuwa, maudhui katika ushairi yamedhihirika vyema kwa kuwauliza maswali kuhusiana na kile walichokiigiza.

Matokeo haya yanakubaliana na nadharia ya utanzu, mhimili wa kwanza (Bakhtin, k.h.j.) unaoshikilia kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke

kwa urahisi sana. Kupitia maigizo wanafunzi walielewa kwa urahisi maudhui yaliyokuwa yanafundishwa na walimu wao. Hii ni kwa sababu wanafunzi walitazama wenzao wanavyoigiza au wenyewe wakiigiza na kwa kuigiza huko wakatambua maudhui katika mashairi hayo kwa urahisi sana. Hali hii imekinzana na matokeo yake Nzuki (k.h.j.), anapoonyesha jinsi ambavyo taswira inavyotumika kuzua maudhui. Katika ugunduzi wake, ufundishaji kwa kutumia mbinu ya maigizo haujahusishwa popote.

Utafiti ulibaini kuwa, maswali na majibu ni mbinu ya ufundishaji iliyotumiwa na watafitiwa saba kati ya watafitiwa tisa (78%) kufundishia maudhui katika utanzu wa ushairi. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, baada ya kuandaa somo la ushairi ipasavyo, watafitiwa walielekea darasani kuwafundisha wanafunzi wao maudhui katika tanzu mbalimbali walizoziteua kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu. Watafitiwa hawa waliwauliza wanafunzi kutambua, kueleza na kujadili maudhui yaliyojitokeza katika utanzu husika wa ushairi; wanafunzi walijibu kulingana na uelewa wao huku watafitiwa wakiwapongeza pale ambapo walipata jibu sahihi na kuwakosoa pale ambapo walipotoka.

Kwa upande mwingine wanafunzi pia waliwauliza walimu wao aidha kueleza au kufafanua zaidi maudhui yale ambayo hawakuyaelewa sawasawa. Mbinu hii ilifaa katika ufundishaji na ujifunzaji kwa sababu iliwawezesha walimu kupima uelewa wa wanafunzi kuhusiana na maudhui katika ushairi papo hapo.

Matokeo haya ya utafiti yameoana na nadharia ya utanzu, mhimili wa kwanza (Bakhtin, k.h.j.) unaoeleza kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi sana. Walimu walipokuwa wakiwauliza wanafunzi kuhusiana na maudhui yaliyobainishwa katika mashairi mbalimbali, waliwafanya wanafunzi kuwa makini na hivyo basi, wanafunzi hao kujitahidi kutoa majibu sahihi na kwa kufanya hivyo, wanafunzi walielewa kwa urahisi sana

namna ya kubainisha maudhui katika mashairi tofautitofauti. Hali hii inaakisi hali katika ugunduzi wake Yego (k.h.j.) anapoonyesha namna maudhui yanavyobainika katika nyimbo za taarabu.

Matumizi ya kinuruweo kama mbinu ya ufundishaji yalibainishwa pale ambapo ilidhihirika kuwa, mtafitiwa mmoja kati ya watafitiwa tisa (11%) aliitumia kufundishia maudhui katika utanzu wa ushairi. Mtafitiwa huyu alisema kuwa, aliunganisha kipakatakilishi chake kwa kinuruweo ili kurusha yale aliyokuwa ameyaandaa kuhusiana na somo la ushairi ukutani; yaliyoandaliwa kuhusiana na somo la ushairi yalihusu mashairi teule ambayo yalikuwa na maudhui.

Mtafitiwa huyu aliendelea kueleza kwamba, wanafunzi walitazama mashairi na vilevile, kusikia sauti za kughani au kukariri mashairi hayo teule; baadaye mtafitiwa huyu aliorodhesha maudhui yaliyopatikana kutokana na mashairi hayo yaliyoteuliwa. Mtafitiwa alitumia mbinu hii kwa sababu wanafunzi walichangamkia kinuruweo na hivyo basi, kuwa katika nafasi nzuri ya kuelewa zaidi utanzu wa ushairi.

Mtafitiwa huyu aliongezea kwamba, mbinu hii ya ufundishaji ilimwepushia mwalimu vumbi iliyotokana na chaki. Hii inahusiana na maelezo ya nadharia ya utanzu, mhimili wa kwanza (Bakhtin, k.h.j.) unaoeleza kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi fulani ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi sana. Wanafunzi waliofurahia matumizi ya kinuruweo katika ujifunzaji wao, walielewa kwa urahisi sana namna ya kutambua maudhui tofautitofauti katika mashairi mbalimbali kwa sababu ufundishaji ulikuwa hai zaidi. Matokeo haya ya utafiti yamekubaliana na ugunduzi wake Gilakjani (k.h.j.) anapoonyesha namna wanafunzi humotishwa teknolojia inapotumika kufundishia lugha ya Kiingereza.

Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa ushairi ni nyingi na pia hutumiwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa tanzu nyinginezo za fasihi. Ushairi huweza pia kutumiwa kama mbinu ya uandishi

katika tanzu nyinginezo za fasihi. Isitoshe, vipengele vya muundo na mtindo wa ushairi huweza kujitokeza katika tanzu hizo hususan tamthilia. Hali hii inaifanya tamthilia kuwa na sifa za kuweza kutumika katika ufunzaji na ujifunzaji wa ushairi.

### 4.3 Namna Tamthilia Inavyoweza Kutumika Kufundisha Ushairi

Utafiti huu ulipambanua namna tamthilia inavyoweza kutumika kufundisha ushairi kwa kuzingatia kigezo cha mtindo, muundo na maudhui kama ifuatavyo:

#### 4.3.1 Mtindo

Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, tamthilia iliweza kutumika kufundisha mtindo wa ushairi. Jedwali lifuatalo linaonyesha namna tamthilia inavyoweza kutumika kufundisha mtindo katika ushairi.

**Jedwali 4.3.1.1 Namna tamthilia inavyoweza kufundisha mtindo katika ushairi**

| Utanzu wa ushairi | Idadi ya watafitiwa | Asilimia |
|---|---|---|
| Nyimbo | 7 | 78% |
| Mashairi huru | 9 | 100% |
| Mashairi ya arudhi | 7 | 78% |
| **Jumla ya walimu** | **9** | **100%** |

Watafitiwa saba kati ya watafitiwa tisa (78%) walieleza kuwa, tamthilia ilikuwa na nafasi katika ufundishaji wa mtindo wa ushairi kwa kurejelea nyimbo. Watafitiwa hawa walisema kwamba, ndani mwa tamthilia kulikuwa na nyimbo ambazo zilikuwa na mtindo, hivyo basi, mwalimu anapofundisha mtindo wa tamthilia anakuwa katika nafasi nzuri pia ya kufundisha mtindo wa

ushairi kwa wakati uo huo. Utafiti ulirejelea tamthilia ya Kifo Kisimani na kubaini kuwa, ilikuwa na wimbo ufuatao:

Tanya: [*Anaimba*] Hekima ya Mtemi Bokono
Kamwe haina mfano,
Mapenzi yake kwa watoto
Abadani hayana mwenza,
Ujuzi wake wa uongozi
Unametameta kama nyota,
Na Moyo wake wa ukarimu
Ni kisima kisichokauka.
Azena: [*Anaimba*] Afya yake ni imara
Kuliko boriti ya mkoko,
Hali yake ni kunjufu
Mithili jua la asubuhi,
Basi tumshukuru Mungu
Kwa zawadi yake adimu,
Na tuimbe kwa fahari
Wenye bahati kama mtende.

Wimbo huu uliimbwa na wahusika wawili ambao ni Tanya na Azena kwa kupokezana katika tamthilia ya Kifo Kisimani. Katika wimbo huu, matumizi ya tashbihi yanadhihirika, mathalani katika ubeti unaoimbwa na Tanya kuna matumizi ya tashbihi katika mstari wa sita; Unametameta kama nyota. Ubeti unaoimbwa na Azena una tashbihi ambayo inapatikana katika mshororo wa tatu na wa nne; Hali yake ni kunjufu mithili jua la asubuhi.

Vilevile, mstari wa mwisho katika ubeti ulioimbwa na Azena kuna tashbihi; Wenye bahati ya mtende. Tashbihi ni tamathali ya usemi ambayo ni mtindo na hivyo basi, mwalimu akifundisha mtindo katika tamthilia, atakuwa amefundisha mtindo katika ushairi kwa sababu ushairi huo

ambao ni wimbo unapatikana katika tamthilia. Hivyo basi, mwalimu atakuwa ametumia mwelekeo mseto katika ufundishaji; ushairi utakuwa umefundishika kwa pamoja na tamthilia.

Matokeo haya yameoana na nadharia ya utanzu, mhimili wa pili (Bakhtin, k.h.j.) unaoshikilia kuwa, tanzu mbili zilizozoeleka zitumike kwa pamoja kwa sababu ya sifa zenye uhusiano mkubwa. Kwa hivyo, tanzu nyingi zinapotumika kwa pamoja huchangia pakubwa kueleweka kwa kazi husika ya fasihi; hivyo basi, mtindo wa ushairi utaeleweka vyema ukifundishwa ndani mwa tamthilia.

Hali hii inakubaliana na ugunduzi wake Day (k.h.j.) anapoeleza kuwa, shairi la kimasimulizi linapoteuliwa kwa lengo la kufundishia hasa kupitia kwa drama, wanafunzi wanaopenda masimulizi yanayoigizwa huweza kuelewa zaidi. Vilevile, matokeo haya yamelingana na ugunduzi wake Feinberg (k.h.j.) anaposema kwamba, wanafunzi wanapoandaa uwasilishaji wa uigizaji wa ushairi katika vikundi, hawatafuti tu na kusoma mashairi bali pia wanachangamkia kuteua mistari kutoka kwa mashairi, kuongeza mistari na baadaye kuyaigiza.

Watafitiwa wote tisa (100%) walieleza kuwa, tamthilia ilikuwa na nafasi nzuri ya kufundishia mtindo katika mashairi huru. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, tamthilia ilikuwa na mashairi huru ambayo yalikuwa na mtindo; hii ina maana kuwa, mtindo katika ushairi ungefundishwa wakati mwalimu anapofundisha tamthilia. Utafiti ulirejelea tamthilia ya Mstahiki Meya kuhakikisha iwapo kulikuwa na mtindo katika mashairi huru yaliyojitokeza hapo ndani. Ufuatao ni mfano wa shairi huru lilivyojitokeza katika tamthilia ya Mstahiki Meya:

**Sauti:** Mstahiki Meya tusikie
Sikiliza sauti zetu zinazokulilia
Zikidai haki kufanyiwa.
Maslahi bora ni haki yetu

Malipo bora ni haki ya mfanyakazi
Huduma za afya ni haki yetu
Tumechoka kudhalilishwa
Na daima kupuuzwa
Tunataka kusikilizwa
Na maslahi yetu kuangaliwa.

Katika shairi hili, takriri inajitokeza; neno 'haki' limerudiwarudiwa katika mshororo wa tatu, nne na tano. Aidha, neno 'yetu' limerudiwarudiwa katika mshororo wa nne na sita. Silabi 'zwa' imerudiwarudiwa katika mshororo wa nane na tisa. Vilevile, taswira inajitokeza katika shairi hili; katika shairi hili, picha inayojengeka akilini mwa msomaji ni kuwa, kuna sauti zinazolilia haki; haki amabayo imepuuzwa. Kupitia kwa tamthilia hii ya Mstahiki Meya utafiti ulibaini kuwa, mtindo wa shairi huru ulikuwa katika nafasi nzuri ya kufundishwa kwa kutumia tamthilia.

Nadharia ya utanzu, mhimili wa pili (Bakhtin, k.h.j.), unaoeleza kuwa, tanzu mbili zilizozoeleka zitumike kwa pamoja kwa sababu ya sifa zenye uhusiano mkubwa, unahusiana na matokeo ya utafiti huu. Kupitia tamthilia ya Mstahiki Meya, mtindo wa ushairi huru unaweza kufundishwa. Hii ni kwa sababu tamthilia iliyozoeleka ina ushairi huru ambao pia umezoeleka kwa wanafunzi na hivyo basi, tanzu mbili zinatumiwa kwa pamoja kwa ajili ya kuwaelekeza wanafunzi kuhusiana na mtindo katika ushairi.

Matokeo haya yameafikiana na hali yake Day (k.h.j.) anapopendekeza kuwa, walimu wawaruhusu wanafunzi wasome mashairi kwa sauti na baadaye wawe katika vikundi ili kujadiliana mistari iliyowapendeza na ndiposa waigize shairi kwa kuwa watakuwa na taswira ya kile kinachoigizwa. Vilevile, matokeo haya ya utafiti yamekinzana na ugunduzi wake Ferguson (k.h.j.) anapohoji kwamba, kuna daraja la kiasilia baina ya drama na lugha na kuwa, drama humotisha wanafunzi wengi na huletea lugha uhai. Ushairi hutumia lugha, na unapoigizwa wanafunzi humotishwa.

Utafiti huu umekinzana na utafiti wake Ferguson (k.h.j.) kwa kuwa amechunguza drama katika kufundishia ushairi.

Watafitiwa saba kati ya tisa (78%) walisema kwamba, tamthilia ilikuwa katika nafasi nzuri ya kutumiwa kufundishia mtindo katika mashairi ya arudhi. Ufundishaji wa mtindo katika shairi la arudhi ungefanikishwa kwa kutumia tamthilia. Utafiti ulirejelea tamthilia ya Kigogo kwa ajili ya kupata mfano wa shairi la arudhi lililokuwa na mtindo. Ufuatao ni mfano wa shairi la arudhi katika tamthilia ya Kigogo:

**Majoka:** Sijui kama karogwa, au pengine katumwa.
Laiti angalijua, moyoni ananiua,
Aache kunikondesha, na raha kunikosesha,
Ashua alichanua, moyoni akanitua,
Nami nikamchagua, ua kuchangamkia,
Kisha akanikimbia, aibu kuniachia,
Yana tabu mazoea, penzile lanisongoa.

Utafiti ulibaini kuwa, shairi hili katika tamthilia ya Kigogo lilikuwa na taswira. Taswira inayobainika katika shairi hili ni ya Majoka ambaye anataabika kwa kumkosa Ashua aliyempenda lakini hakumwoa; anateseka kwa kukosa kumwoa Ashua aliyempenda. Hivyo basi, mtindo wa shairi hili la arudhi unafundishwa kupitia tamthilia hii ya Kigogo. Aidha, kuna takriri ya sauti 'a' ambayo inajitokeza katika vina vya ndani na nje katika shairi lote isipokuwa mshororo wa kwanza na tatu.

Kupitia kwa shairi hili ambalo linapatikana katika tamthilia ya Kigogo, mhimili wa pili wa nadharia ya utanzu (Bakhtin, k.h.j.) unaofafanua kwamba, tanzu mbili zilizozoeleka zitumike kwa pamoja kwa sababu ya sifa zenye uhusiano mkubwa unadhihirika. Maelezo yanayojitokeza kuhusu taswira na takriri katika shairi la arudhi yanadhihirika kwa uwazi katika tamthilia hii ya Kigogo.

Hali hii imehusiana na matokeo yake Tsiaras (k.h.j.) anapoeleza kwamba, ni muhimu walimu kutumia mbinu ya drama kufundishia ushairi kwa sababu wanafunzi humotishwa shairi linapoigizwa.

Matokeo haya vilevile, yametofautiana na ugunduzi wao Gasparro na Falletta (k.h.j.) wanapoeleza kuwa, lugha ya mwili pamoja na ishara za uso huhusishwa na vipengee simulizi. Vipengee hivyo ambavyo ni: kiimbo, urari wa vina, uradidi na tamathali za usemi, hudhihirika ushairi unapoigizwa. Hii ni kwa sababu wamezingatia ufundisahaji wa ushairi kwa kutumia drama za Kiingereza.

### 4.3.2 Muundo

Jedwali lifuatalo linaonyesha namna watafitiwa walivyotoa maoni yao kuhusiana na tamthilia kutumika kufundishia muundo katika utanzu wa ushairi:

**Jedwali 4.3.2.1 Namna tamthilia inavyoweza kufundisha muundo katika ushairi**

| **Utanzu wa ushairi** | **Idadi ya watafitiwa** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Nyimbo | 7 | 78% |
| Mashairi huru | 9 | 100% |
| Mashairi ya arudhi | 8 | 89% |
| **Jumla ya walimu** | **9** | **100%** |

Watafitiwa saba (78%) walisema kuwa, nyimbo zilibainika katika tamthilia, hivyo basi, kulikuwa na mtindo wa ushairi katika nyimbo hizo zilizobainika katika tamthilia. Kwa maoni yao watafitiwa hawa saba, mwalimu anapofundisha mtindo katika ushairi anaweza kutumia tamthilia ili kuwabainishia wanafunzi namna muundo ulivyotumika katika utanzu wa ushairi. Katika tamthilia

ya Kigogo, utafiti ulibainisha namna muundo ulivyojitokeza na hivyo basi, mwalimu anaweza kutumia tamthilia hii kuwawasilishia wanafunzi wake muundo katika nyimbo jinsi ifuatavyo:

**Hashima:** (*Anaimba*.) Ndege ruka, ndege ruka, na barua mkononi,
Kifika kamwambie kimbunga usiku mchana,
Kila uchao twasema heri yalopita jana,
Hata nami sasa naja mbuga nami nachana,
Hapa hapataniweka, najua tutaonana.

Katika wimbo huu, muundo wa ushairi unadhihirika. Hashima anapoimba, inabainika kuwa, kuna mizani ambayo imelingana (mizani kumi na sita) katika kila mshororo isipokuwa mshororo wa nne ambao una mizani kumi na mitano. Wimbo huu unaoimbwa na Hashima una vina vilivyofanana (na) katika kila mshororo isipokuwa mshororo wa kwanza ambao una kina tofauti (ni). Utungo huu pia una mistari mitano katika ubeti mmoja ulio na kipande kimoja kimoja katika kila mshororo isipokuwa mshororo wa kwanza na wa mwisho.

Matokeo haya yameoana na nadharia ya utanzu, mhimili wa pili (Bakhtin, k.h.j.) kuwa, tanzu mbili zilizozoeleka zitumike kwa pamoja kwa sababu ya sifa zenye uhusiano mkubwa. Hii ni kwa sababu kupitia tamthilia ya Kigogo, muundo wa ushairi unabainika. Tamthilia ni utanzu ambao umezoeleka kwa wanafunzi, hii ni sawia na ushairi, kwa hivyo, wimbo unaoimbwa na Hashima katika tamthilia unadhihirisha muundo wa ushairi kama utanzu uliozoeleka kwa wanafunzi. Matokeo haya yamehusiana na matokeo yake Tsiaras (k.h.j.) anapogundua kwamba, walimu waliwahimiza wanafunzi wao kuandika mashairi kwa kutumia sifa za kidrama.

Watafitiwa wote tisa (100%) walisema kuwa, mashairi huru yalibainika katika tamthilia za Kiswahili na hivyo basi, mwalimu alikuwa na uwezo wa kutumia tamthilia kufundishia muundo wa mashairi hayo huru. Mizani, vina, mishororo, vipande, vimalizio na beti ni vipengee vya

muundo ambavyo vingebainika katika mashairi huru. Utafiti ulirejelea tamthilia ya Mstahiki Meya kuteua shairi huru lililojitokeza na lililokuwa na muundo ambao ungeweza kuwasilishwa kwa wanafunzi kama ifuatavyo:

**Dida:** Duniani kuna watu na viatu
na Cheneo ina watu na viatu.
Paka na panya
Panya na paka!

Kazi ya askari nzuri
Si kama huku kufagia.
Kufagia hakuna heshima
Bwana anakutusi
na kukudhalilisha.
Askari na bunduki yake mfalme
Hata bwana anajua.

Bunduki inayotema risasi tatu tatu
basi tena uwe umelala chini hivi
Mlio wake
Vitoa machozi
Magari yanayotapika maji.

Wakati wa mauti kama juzi
Kumbe wazee huwashinda mbio vijana!
Roho ya mtu hapendi mtu imponyoke.
kwa bahati mbaya ikiponyoka
Wakubwa hueleza haikutoka.

Kuna roho ya mtu na ya kiatu
na hizi mbili ni tofauti.
Meya anajua hili
Watu wake wana roho za watu
Naye hakusita mbali akazipeleka
Mbali na uvundo na joto la jiji.
Katika salama ya utulivu
Wa mandhari na hali.

Mimi Dida nayatakia nini?
Mradi mameya wawepo
Nizidi zao nyumba kuzinadhifu.
Hata kama mji mzima kwa uvundo unatisha!

Kupitia maneno yake Dida katika tamthilia ya Mstahiki Meya ambapo yanasikika kama shairi huru, sifa za muundo wa shairi huru zinabainika. Katika unukuzi huu, mizani katika mishororo yote katika kila ubeti haifanani, aidha hakuna mtiririko wa vina katika kila mshororo. Vilevile, mishororo hailingani katika kila ubeti; kuna idadi tofauti tofauti ya mishororo katika kila ubeti. Hili ni shairi ambalo lina kipande kimoja tu katika kila ubeti. Shairi hili lina kimalizio katika kila ubeti na lina jumla ya beti sita.

Nadharia ya utanzu, mhimili wa pili (Bakhtin, k.h.j.), inaeleza kuwa, tanzu mbili zilizozoeleka zitumike kwa pamoja kwa sababu ya sifa zenye uhusiano mkubwa unabainika. Hii ni kwa sababu utanzu wa ushairi unabainika katika tamthilia ya Mstahiki Meya. Hali hii inaakisi matokeo yake Tsiaras (k.h.j.) anapogundua kuwa, ufundishaji wa ushairi kwa kutumia drama uliwawezesha wanafunzi kuelewa ushairi kwa kuwa ilikuwa mbinu mwafaka ya ufundishaji.

Wasailiwa wanane kati ya wasailiwa tisa (89%) walieleza kuwa, muundo katika utanzu wa ushairi unaweza kufundishwa kwa kutumia tamthilia. Hii ni kwa sababu tamthilia ilikuwa na mashairi ya arudhi ambayo yalidhihirisha muundo wa ushairi. Jinsi ambavyo mizani, vina, mishororo, vipande, vimalizo, vibwagizo na beti zilivyopangwa katika mashairi ya arudhi, hivyo ndivyo zilivyojitokeza katika mashairi yaliyopatikana katika tamthilia za Kiswahili. Utafiti ulirejelea shairi moja katika tamthilia ya Kigogo kubainisha muundo wa ushairi kama ifuatavyo:

**Majoka:** Nifungue?

**Babu:** Fungua masikio usikie,
Fungua macho uonee,
Fungua pua unusie,
Fungua moyo uhisie,
Nasema.

**Majoka:** Wasema babu?

**Babu:** Nasema nawe kwa tuo,
Nasema ukome tutuo,
Nasema naweka mtuo,
Maisha.

**Majoka:** Maisha?

**Babu:** Maisha ndumakuwili,
Maisha ni ncha mbili,
Kuishi.

**Majoka:** Kuishi?

**Babu:** Kuishi kumbe kuisha,
Kuishi kulivyo ni kama mshumaa,
Unapoanza kuwaka, hukuza miale yake taratibu,
Halafu unashika kasi, kasi sana.

Shairi hili linalojitokeza kama ngonjera, lina wahusika wawili ambao ni Majoka na Babu, na kupitia kwa wahusika hawa, inabainika kuwa, kuna beti nane; beti za Majoka zina mshororo mmoja mmoja ikilinganishwa na beti za Babu. Ubeti wa kwanza wa Babu una mtiririko wa vina (kina cha mwisho ni ‘e’) isipokuwa mshororo wa mwisho ambao una kina cha ‘ma’. Katika ubeti wa pili wa Babu, vina vya mwisho ni ‘o’ isipokuwa mshororo wa mwisho ambao una kina cha ‘sha’. Ubeti wa tatu wa Babu una vina vya mwisho ambavyo ni ‘li’ isipokuwa mshororo wa mwisho ambao una kina cha ‘shi’.

Ubeti wa mwisho wa Babu una vina tofauti tofauti: ‘sha’ katika mshororo wa kwanza, ‘a’ katika mshororo wa pili, ‘bu’ katika mshororo wa tatu na ‘na’ katika mshororo wa mwisho. Kwa upande mwingine, beti za Majoka ambazo zina mshororo mmoja mmoja katika kila ubeti zina vina tofauti tofauti: ‘e’ katika ubeti wa kwanza, ‘bu’ katika ubeti wa pili, ‘sha’ katika ubeti wa tatu na ‘shi’ katika ubeti wa mwisho wa Majoka. Shairi hili lina kipande kimoja kimoja katika kila ubeti. Mizani katika kila mshororo wa kila ubeti hailingani.

Nadharia ya utanzu, mhimili wa pili (Bakhtin, k.h.j.), inaeleza kuwa, tanzu mbili zilizozoeleka zitumike kwa pamoja kwa sababu ya sifa zenye uhusiano mkubwa, inahusiana na matokeo ya utafiti huu. Hii ni kwa sababu muundo wa ushairi unabainika katika tamthilia ya Kigogo.

Matokeo haya yametofautiana na matokeo ya Ferguson (k.h.j.) anapohoji kuwa, shairi ligawiwe wanafunzi mishororo na beti ambazo ni vijenzi vya muundo wa shairi. Ugunduzi wake Ferguson (k.h.j.), umetofautiana na utafiti huu kwa kuwa unahusu ufundishaji wa vijenzi vya ushairi kwa kutumia drama za Kiingereza. Aidha, matokeo haya yamelingana na ugunduzi wao Elting na Firkins (k.h.j.) wanapohoji kwamba, ili kulifaragua shairi la kuigizwa, walimu wawagawie wanafunzi wanaoigiza mistari au beti.

### 4.3.3 Maudhui

Utafiti ulibaini kuwa, tamthilia za Kiswahili zilikuwa na nafasi nzuri ya kutumiwa kufundishia maudhui katika utanzu wa ushairi kwa sababu zilikuwa na tanzu mbalimbali ambazo zilidhihirisha maudhui. Maoni yao wasailiwa hawa yaliwasilishwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 4.3.3.1 Namna tamthilia inavyoweza kufundisha maudhui katika ushairi**

| Utanzu wa ushairi | Idadi ya watafitiwa | Asilimia |
|---|---|---|
| Nyimbo | 8 | 89% |
| Mashairi huru | 9 | 100% |
| Mashairi ya arudhi | 7 | 78% |
| **Jumla ya walimu** | **9** | **100%** |

Watafitiwa wanane kati ya watafitiwa tisa (89%) walisema kwamba, tamthilia inaweza kutumika kufundishia maudhui katika nyimbo. Maudhui yalipatikana katika nyimbo zilizotumiwa katika tamthilia. Watafitiwa hawa walisema kuwa, maudhui yaliyopatikana katika nyimbo za tamthilia yalifungamana na maudhui ya tamthilia yenyewe. Utafiti ulirejelea nyimbo mbili katika tamthilia ya Kigogo kwa ajili ya kubainisha maudhui yaliyopatikana katika nyimbo hizo kama ifuatavyo:

**Ngurumo:** Msichana mrembo kama wewe, ni kitu gani kinakufanya usiolewe?
Elimu unayo ya kutosha, hata ng'ambo ulikwenda ukarudi.
Ukionyesha majivuno kwa vijana, utazeeka ukiwa nyumbani kwenu.
Oooh bebi, miaka yaenda mbio sana, nayo sura yako inachujuka,
Pengine tabia zako ndizo mbaya awali dada ulijivuna.

Wimbo huu wa Daudi Kabaka unaoimbwa na Ngurumo na vilevile, kuitikiwa na Boza pamoja na walevi wengine ni mfupi lakini una ujumbe mzito. Maudhui ya urembo yanajitokeza katika wimbo

huu. Inabainika kuwa, msichana mrembo hataki kuolewa na kuwa akizidi kukaa nyumbani kwao atazidi kuzeeka na hata sura yake itachujuka. Katika tamthilia wimbo huu unamrejelea Tunu ambaye kulingana na akina Ngurumo, Boza pamoja na walevi wengine ni mrembo lakini hataki kuonyesha urembo ule kwa Ngao Junior (mwanawe Majoka) ili amwoe.

Katika wimbo huu inabainika kuwa, maudhui ya ndoa. Msichana wa sura nzuri haoelewi na sababu ya kutoolewa ni kuwa, anaonyesha majivuno kwa vijana wenzake wa kiume ambao wanaweza kumwoa. Kulingana na akina Ngurumo, Tunu ni msichana ambaye hajaolewa hasa kwa Ngao Junior kwa sababu ameonyesha majivuno.

Maudhui ya elimu yanabainika katika wimbo huu wa Daudi Kabaka kwa sababu kuna msichana aliyesomea ng'ambo. Msichana huyo anayo elimu ya kutosha kwa sababu alisomea ng'ambo. Katika tamthilia, Ngurumo, Boza pamoja na walevi wengine wanauimba wimbo huu kwa ajili ya kumrejelea Tunu ambaye alisoma hadi ng'ambo na kupata shahada ya uzamifu katika sheria. Maudhui ya majivuno kwa vijana yanabainika katika wimbo huu. Msichana mrembo anashauriwa kuwa, akionyesha majivuno kwa vijana atazeekea nyumbani; sura yake inachujuka kwa sababu hapo awali alikuwa na tabia mbaya; alijivuna. Katika tamthilia, Ngurumo na wenzake wanauimba wimbo huu kimakusudi ili kumrejelea Tunu ambaye wanadhani ana majivuno kwa vijana wenzake wa kiume na ndiposa hajaolewa.

Aidha, maudhui ya sura kuharibika kwa sababu ya kuchelewa kuolewa yanadhihirika. Msichana mrembo anaambiwa kuwa, miaka huenda mbio sana na hivyo basi akikawia nyumbani kwao atazeeka kwani sura yake itachujuka na hivyo basi, hatakuwa na wa kumwoa. Katika tamthilia walevi wanaimba wimbo huu kimakusudi kwa ajili ya kumrejelea Tunu ambaye wanadhani kuwa, ana sura nzuri lakini hataki kuolewa na yeyote yule.

Matokeo haya ya utafiti yanalingana na nadharia ya utanzu, mhimili wa pili (Bakhtin, k.h.j.) unaoshikilia kwamba, tanzu mbili zilizozoeleka zitumike kwa pamoja kwa sababu ya sifa zenye uhusiano mkubwa. Maudhui ya ushairi yanajitokeza katika tamthilia ya Kigogo na yana uhusiano mkubwa jinsi ilivyoelezwa. Hali hii inaakisi matokeo ya Ferguson (k.h.j.) anapohoji kuwa, matumizi ya matini na drama huzidi ufahamu wa kawaida na huwapa wanafunzi fursa ya kuwakilisha maudhui changamano pamoja na jazanda kupitia uigizaji.

Wimbo wa pili katika tamthilia ya Kigogo ambao umedhihirisha maudhui ni wimbo unaoimbwa na Ashua mwishoni mwa tamthilia kuashiria ushindi wao katika vita dhidi ya Majoka na wafuasi wake kuhusiana na kufunguliwa kwa soko la Chapakazi lilofungwa na Majoka lakini limefunguliwa kwa sababu ya juhudi zao Tunu, Sudi, Ashua na wakazi wengine kama ifuatavyo:

**Ashua:** Soko lafunguliwa bila nyoka (x2),
Soko lafunguliwa bila Chopi. (x2).

Maudhui ya ushindi dhidi ya maovu yanabainika katika wimbo huu. Majoka ambaye alilifunga soko la Chapakazi kwa manufaa yake anakejeliwa kuwa, nguvu zake za uovu, yaani kukandamiza haki za wakazi wengine kwa kushirikiana na vibaraka kama vile Chopi, zimeshindwa. Hii ni kwa sababu akina Ashua, Tunu na Sudi wanashirikiana kukomboa soko la Chapakazi.

Nadharia ya utanzu, mhimili wa pili (Bakhtin, k.h.j.) unaofafanua kuwa, tanzu mbili zilizozoeleka zitumike kwa pamoja kwa sababu ya sifa zenye uhusiano mkubwa inabainika. Maudhui ya ushindi yanabainika katika tamthilia lakini kupitia kwa utanzu wa ushairi. Matokeo haya yameoana na ugunduzi wake Vodickova (k.h.j.) anapohoji kwamba, shairi ambalo linaweza kuigizwa huwa na maudhui. Hivyo basi, mwalimu anapofundisha, awahimize wanafunzi ili waweze kuigiza kwa lengo la kubaini maudhui hayo.

Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, wasailiwa wote tisa (100%) walieleza kuwa, tamthilia inaweza kutumiwa kufundishia maudhui katika mashairi huru yanayobainika katika tamthilia husika. Wasailiwa hawa walisema kuwa, maudhui ya kitamthilia yenyewe yalibainishwa kupitia mashairi huru ambayo mtunzi aliamua kuyaingiza katika tamthilia yake. Utafiti ulirejelea tamthilia ya Mstahiki Meya kubainisha shairi huru lilokuwa na maudhui ndani mwake. Maneno ya Siki katika tamthilia ya Mstahiki Meya yanajitokeza kama shairi huru jinsi ifuatavyo:

**Siki:** Mimi nilimwambia!
Lakini wapi?
Watu wenye uwele
Na njaa vilevile
Wakusikilize wapi!

Njaa ina nguvu
Imeangusha miamba
Wenye mengi maguvu
Matata yatawakumba.
Mwenye tumbo tupu
Hataki ya kuamba
Wala vitendo vichelewevu.

Katika utungo huu, maudhui ya njaa yanadhihirika. Siki anasema kuwa, watu walio na njaa huwa hawasikii kwa sababu njaa huwa na nguvu. Njaa ina nguvu kiasi kwamba, huangusha miamba na watu walio na nguvu nyingi. Siki anazidi kusema kuwa, watu walio na njaa huwa hawana nguvu ya kutenda chochote kile na hivyo basi, changamoto nyingi huwa zinawakumba. Maudhui haya yanabainika katika tamthilia kwa ujumla wake kwa sababu kuna wanacheneo wengi ambao hawana vyakula.

Vilevile, kuna maudhui ya ugonjwa ambayo yanajitokeza katika ushairi huu. Siki anasema kuwa, watu wagonjwa hawawezi kusikia wanachoelezwa kwa sababu huwa hawana nguvu. Maudhui haya yanaafiki yale yaliyomo katika tamthilia kwa sababu kuna wagonjwa ambao huwa wamelazwa zahanatini bila kutibiwa.

Matokeo ya utafiti yanakubaliana na nadharia ya utanzu, mhimili wa pili (Bakhtin, k.h.j.) kuwa, tanzu mbili zilizozoeleka zitumike kwa pamoja kwa sababu ya sifa zenye uhusiano mkubwa. Maudhui yanayobainika katika utanzu wa ushairi yamefungamana katika tamthilia ya Mstahiki Meya na yana uhusiano mkubwa. Utanzu huu wa shairi huru una sifa ya kimaudhui ambayo inajitokeza sawasawa katika tamthilia ya Kigogo; maudhui yanayobainika katika utanzu huu wa ushairi ndiyo yanayosisitizwa katika tamthilia ya Kigogo. Matokeo haya yanalingana na matokeo yake Vodickova (k.h.j.) anapogundua kwamba, wanafunzi wanapoigiza majukumu ya wahusika katika drama, maudhui hubainika.

Utafiti ulibaini kuwa, watafitiwa saba kati ya watafitiwa tisa (78%) walieleza kuwa, maudhui katika mashairi ya arudhi yalipatikana katika tamthilia. Maudhui yaliyopatikana katika mashairi ya arudhi yaliyokuwa ndani mwa tamthilia yangefundishwa kwa pamoja na hivyo basi, kueleweka sawasawa. Utafiti ulirejelea tamthilia ya Kigogo kubainisha maudhui hayo kama ifuatavyo:

**Majoka:** Sijui kama karogwa, au pengine katumwa.
Laiti angalijua, moyoni ananiua,
Aache kunikondesha, na raha kunikosesha,
Ashua alichanua, moyoni akanitua,
Nami nikamchagua, ua kuchangamkia,
Kisha akanikimbia, aibu kuniachia,
Yana tabu mazoea, penzile lanisongoa.

Kulingana na shairi hili la arudhi ambalo linadhihirika katika tamthilia ya Kigogo, maudhui ya mapenzi yanadhihirika. Majoka alimpenda sana Ashua lakini Ashua hakumpenda Majoka hata kidogo. Majoka anahangaika moyoni mwake kwa kumpenda Ashua lakini Ashua aliyechaguliwa na Majoka hakumchangamkia hata kidogo na ndiyo maana penzi lake Majoka kwa Ashua asiyempenda linampa taabu moyoni.

Nadharia ya utanzu, mhimili wa pili (Bakhtin, k.h.j.) unaoeleza kuwa, tanzu mbili zilizozoeleka zitumike kwa pamoja kwa sababu ya sifa zenye uhusiano mkubwa inaafikiana na matokeo ya utafiti. Maudhui ya mapenzi yanayopatikana katika shairi hili ndiyo yanayobainika katika tamthilia pia, hivyo basi, kuna uhusiano wa maudhui haya ya shairi na maudhui ya tamthilia. Matokeo haya yamelingana na ugunduzi wake Vodickova (k.h.j.) anapofafanua kwamba, wanafunzi wanaposhirikishwa katika uigizaji wa ushairi wanafahamu maudhui zaidi kwa sababu wanapoigiza wanayazua. Kila mhusika huzua maudhui.

Matokeo ya utafiti huu kinyume na tafiti za awali yameonyesha ufundishaji wa maudhui katika ushairi unavyotekelezwa kwa kutumia tamthilia. Tafiti za awali zilizingatia ushairi kwa kutumia drama hasa za Kiingereza. Hata hivyo, utafiti huu umeonyesha ubora katika ufundishaji wa maudhui katika ushairi iwapo tamthilia itahusishwa.

### 4.4 Mchango wa Matumizi ya Tamthilia Katika Ufundishaji wa Ushairi

Watafitiwa walikuwa na maoni mbalimbali kuhusiana na mchango wa tamthilia katika ufundishaji wa utanzu wa ushairi jinsi inavyodhihirika katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 4.4.1 Mchango wa tamthilia katika ufundishaji wa ushairi**

| **Mchango** | **Idadi ya watafitiwa** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Ufundishaji wa tamathali za usemi kwa urahisi | 7 | 78% |
| Ufafanuzi bora wa muundo miongoni mwa wanafunzi | 7 | 78% |
| Uelewa wa maudhui kwa urahisi miongoni mwa wanafunzi | 7 | 78% |
| Ukamilishaji wa silabasi mapema miongoni mwa walimu | 4 | 44% |
| Wanafunzi kuchangamkia somo | 6 | 67% |
| Kuibuliwa kwa ilhamu ya kutafiti miongoni mwa wanafunzi | 3 | 33% |
| Umakinifu wa wanafunzi darasani | 5 | 56% |
| **Jumla ya walimu** | **9** | **100%** |

### 4.4.1.1 Ufundishaji wa Tamathali za Usemi kwa Urahisi

Watafitiwa saba kati ya watafitiwa tisa (78%) walisema kuwa, tamthilia ikitumiwa kufundishia utanzu wa ushairi, itachangia kufafanuliwa kwa tamathali za usemi zinazojitokeza katika ushairi husika unaobainika katika tamthilia. Tamathali za usemi kama vile methali, tashbiha, istiari, jazanda, taswira, sadfa na kinaya zilifungamana katika nyimbo, mashairi huru na mashairi ya arudhi yaliyofungamana katika tamthilia za Kiswahili.

Matokeo haya ya utafiti yameoana na nadharia ya utanzu, mhimili wa tatu (Bakhtin, k.h.j.) kuwa, matumizi ya utanzu mwingine huwafanya wasomaji au wapokezi kuwa na ilhamu zaidi kuliko kuwapa kila wanachotarajia. Mwalimu afundishaye tamathali za usemi atawafanya wanafunzi wake kuwa na ilhamu kwa sababu tamathali hizo zinazobainishwa katika mashairi mbalimbali zinafundishwa kwa kutumia tamthilia na hivyo basi, kuwezeshwa kuzielewa kwa urahisi. Hili

litatendeka iwapo wapokezi ambao ni wanafunzi watachukua jukumu la kusoma tamthilia kwa sababu ya ile ilhamu waliyo nayo na hivyo basi, kuwa katika nafasi nzuri ya kubainisha tamathali hizo za usemi.

Hali hii imekinzana na matokeo yake Vannak (k.h.j.) anapoangazia matumizi ya mwelekeo mseto katika ufundishaji wa fasihi ya Kiingereza. Kwa upande mwingine, matokeo haya yameoana na matokeo yake Wanyela (k.h.j.) anaposema kuwa, tamathali za usemi kama vile, tashbihi, kejeli, chuku, jazanda, taswira, urudiaji na usambamba, tashhisi, semi na methali husisitizwa katika ushairi ambao huwa katika tamthilia kwa lengo la kuleta ujumbe.

#### 4.4.1.2 Ufafanuzi Bora wa Muundo Miongoni mwa Wanafunzi

Watafitiwa saba kati ya watafitiwa tisa (78%) walisema kuwa, matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa ushairi yalikuwa bora kwa sababu wanafunzi waliweza kufafanua muundo wa tanzu mbalimbali za ushairi miongoni mwao kwa urahisi. Vipengee vya muundo kama vile mizani, vina, mishororo, vipande, vibwagizo, vimalizio na beti vilieleweka vyema miongoni mwa wanafunzi kwa sababu walisoma mara kwa mara tamthilia ambayo wanatahiniwa na hivyo basi, tanzu kama vile nyimbo, mashairi huru na mashairi ya arudhi zilibainika katika tamthilia inayotahiniwa. Tanzu hizo zilikuwa na vipengee vya muundo ambavyo vilipatikana katika mashairi mengine ambayo hayakuwa katika tamthilia. Hivyo basi, ufundishaji wa utanzu wa ushairi kupitia kwa tamthilia uliwezesha ufafanuzi bora zaidi wa muundo wa ushairi miongoni mwa wanafunzi.

Matokeo haya yamelingana na nadharia ya utanzu, mhimili wa tatu (Bakhtin, k.h.j.) unaofafanua kwamba, matumizi ya utanzu mwingine huwafanya wasomaji au wapokezi kuwa na ilhamu zaidi kuliko kuwapa kila wanachotarajia. Wapokezi ambao ni wanafunzi kupitia kwa walimu wao

huongozwa kuvifahamu vipengee vya muundo wa tanzu husika kupitia tamthilia; ushairi ni utanzu ambao ni tofauti sana na utanzu wa tamthilia katika fasihi lakini tanzu hizi huwa zimeletwa kwa pamoja kutegemea na mtunzi wa tamthilia na hivyo basi, mwanafunzi hufafanuliwa zaidi muundo wa ushairi kupitia utanzu wa tamthilia wakati mwalimu anapofundisha darasani.

Hali hii imetofautiana na matokeo yao Cheruto na Orodho (k.h.j.) wanapoeleza kwamba, japo mbinu ya mwelekeo mseto ni changamano miongoni mwa walimu ni muhimu ikitumika. Hii ni kwa sababu mbinu wanazozitumia Cheruto na Orodho (k.h.j.) hazihusishwi katika ufundishaji. Aidha, matokeo haya yamekubaliana na ugunduzi wake Giebert (k.h.j.) anapohoji kuwa, ushairi unapoigizwa darasani huwasaidia wanafunzi kufanya maoezi ya matamshi na kiimbo. Wanafunzi wanapoigiza ushairi, wataelewa zaidi kwa sababu uigizaji ni wao, na kile ambacho hawakukifahamu mwalimu akiwa darasani, watakifahamu, kupitia drama.

#### 4.4.1.3 Uelewa wa Maudhui kwa Urahisi Miongoni mwa Wanafunzi

Wasailiwa saba kati ya wasiliwa tisa (78%) walieleza kuwa, tamthilia ilikuwa na mchango mkubwa katika ufundishaji wa utanzu wa ushairi katika shule za upili kwa sababu kupitia kwa tamthilia wanafunzi walielewa kwa urahisi maudhui. Hii ni kwa sababu maudhui yaliyopatikana katika nyimbo, mashairi huru na mashairi ya arudhi ndiyo yaliyofungamanishwa katika tamthilia husika na mtunzi wa tamthilia hiyo. Kila utanzu wa ushairi uliobainika katika tamthilia ulikuwa na maudhui na hivyo basi, mwalimu afundishapo maudhui katika ushairi anakuwa na fursa bora ya kutumia tamthilia kwa sababu tamthilia hiyo ina tanzu za ushairi ambazo zina maudhui.

Matokeo haya yamelingana na nadharia ya utanzu, mhimili wa tatu (Bakhtin, k.h.j.) unaoeleza kwamba, matumizi ya utanzu mwingine huwafanya wasomaji au wapokezi kuwa na ilhamu zaidi kuliko kuwapa kila wanachotarajia. Maudhui ya utanzu wa ushairi yanapofundishwa sambamba

na maudhui ya tamthilia, huwafanya wanafunzi ambao ni wapokezi wa kazi hiyo kuielewa kwa urahisi. Hii ni kwa sababu maudhui ya utanzu wa ushairi yanajitokeza katika tamthilia na hivyo basi, kuwafanya wanafunzi kuwa na ile ilhamu ya kusoma tamthilia nyingine tofauti na zile wanazofundishwa kwa ajili ya kutafiti mashairi yaliyo na maudhui kwa ajili ya kuelewa zaidi. Kwa hivyo, wanafunzi watawezeshwa kuelewa namna ya kubainisha maudhui katika ushairi kwa urahisi kwa sababu ya ile ilhamu ya kutaka kusoma zaidi.

Hali hii imetofautiana na matokeo yake Mapunjo (k.h.j.) anapobainisha namna maudhui yanavyojitokeza katika tamthilia. Sababu ni kwamba, Mapunjo (k.h.j.) amebainisha tu maudhui katika tamthilia pasi na kuonyesha namna tamthilia hiyo inavyotoa mchango wake katika ufundishaji wa ushairi. Aidha, matokeo haya yamekubaliana na ugunduzi wake Giebert (k.h.j.) anaposema kuwa, maudhui hubainika mwalimu anapofundisha ushairi na kuwa, umuhimu wake ni kuwaelekeza wanafunzi kuzifahamu dhana zinazotumiwa kitabuni.

#### 4.4.1.4 Ukamilishaji wa Silabasi Mapema Miongoni mwa Walimu

Watafitiwa wanne kati ya watafitiwa tisa (44%) walisema kuwa, kufundisha ushairi kwa kutumia tamthilia hasa inayotahiniwa kwa wakati huo, kulikuwa bora kwa sababu kuliwawezesha walimu kukamilisha silabasi kwa wakati ufaao. Watafitiwa hawa walisema kwamba, mwalimu aliyefundisha vipengee vya mtindo, muundo na maudhui katika tanzu za ushairi zilizojitokeza katika tamthilia, hakuwa na tatizo la kuwafundisha wanafunzi vipengee hivyo kwa upekee wake katika kila utanzu (tamthilia na ushairi) kwa sababu vilibainika waziwazi. Mathalani namna mwalimu anapofundisha maudhui katika ushairi kivyake au maudhui katika tamthilia kivyake ndivyo anavyofundisha maudhui hayo kwa pamoja katika tamthilia iliyo na tanzu za ushairi. Kwa kufanya hivyo, mwalimu anakuwa na nafasi nzuri ya kukamilisha silabasi kwa wakati ufaao kwa sababu vipengee vya maudhui, mtindo na hata muundo huwa tayari vimegusiwa kwa ukamilifu

wake katika tanzu za ushairi zinazojitokeza katika tamthilia husika ikilinganishwa na jinsi mwalimu anavyofundisha vipengee hivyo kwa mipaka ya tanzu hizo za fasihi.

Matokeo haya yanafungamana na nadharia ya utanzu, mhimili wa tatu (Bakhtin, k.h.j.) kwamba, matumizi ya utanzu mwingine huwafanya wasomaji au wapokezi kuwa na ilhamu zaidi kuliko kuwapa kila wanachotarajia. Hivyo basi, wapokezi ambao ni wanafunzi watakuwa na ile ilhamu ya kubainisha vipengee vya mtindo, muundo na maudhui katika mashairi namna vinavyobainika katika tamthilia kwa kusoma tamthilia zilizoteuliwa na zile ambazo si teule lakini zina vipengee hivyo. Wanafunzi wanapochochewa kuwa na ilhamu ya kusoma tamthilia kwa ajili ya kubainisha vipengee vya ushairi katika tamthilia, wanawawezesha walimu wao kuwasaidia kukamilisha silabasi mapema. Matokeo haya yametofautiana na matokeo yake Molenje (k.h.j.) anapoonyesha jinsi walimu wanavyokuwa na changamoto katika kutekeleza silabasi mpya ilhali utafiti huu ulihusu matokeo ya ukamilishaji wa silabasi kwa wakati ufaao miongoni mwa walimu.

#### 4.4.1.5 Wanafunzi Kuchangamkia Somo

Wasailiwa sita kati ya wasailiwa tisa (67%) walisema kuwa, kufundisha utanzu wa ushairi kwa kutumia tamthilia ni muhimu kwa sababu wanafunzi huchangamkia somo. Watafitiwa hawa walisema kuwa, vipengee vya mtindo, maudhui na muundo ambavyo hubainika katika tanzu mbalimbali za ushairi ambazo huwa ndani mwa tamthilia huchangamkiwa na wanafunzi kwa sababu hazijitokezi zikiwa pekee tu bali hujitokeza katika utanzu mwingine. Wakati wanafunzi wanafurahia tamthilia, huwa wanafurahia tanzu za ushairi ambazo hupatikana ndani mwa tamthilia, hivyo basi, mwalimu afundishapo vipengee vya mtindo, muundo na maudhui katika nyimbo, mashairi huru na mashairi ya arudhi kwa kutumia tamthilia, huwachangamsha wanafunzi wake.

Matokeo haya yamelingana na maelezo ya nadharia ya utanzu, mhimili wa tatu (Bakhtin, k.h.j.) unaoshikilia kwamba, matumizi ya utanzu mwingine huwafanya wasomaji au wapokezi kuwa na ilhamu zaidi kuliko kuwapa kila wanachotarajia. Hii ni kwa sababu vipengee vya muundo vinapofafanuliwa, wanafunzi wanachangamka na hivyo basi, kuwa katika nafasi bora ya kuelewa ushairi unaofundishwa kwa kutumia tamthilia. Kwa hivyo, wanafunzi huwa na ilhamu ya kusoma tamthilia zilizo na vipengee vya ushairi kwa ajili ya kupata msisimko huo na hivyo basi, kuwa katika nafasi nzuri ya kuelewa vipengele vya ushairi kama vile mtindo, muundo na maudhui vinavyobainika katika tamthilia walizoziteua kuzisoma.

Hali hii inatofautiana na ugunduzi wake Yimwilai (k.h.j.) anapoonyesha uthabiti wa mwelekeo mseto kama mbinu ya ufundishaji wa somo la Kiingereza. Kulingana naye, mbinu hii hubadilisha mitazamo ya wanafunzi katika usomaji wa fasihi. Kwa upande mwingine matokeo haya yamefanana na matokeo yake Giebert (k.h.j.) anaposema kwamba, uigizaji wa ushairi huwasaidia wanafunzi kuwa na ujasiri na ufasaha wa lugha. Wanafunzi wanapata tu ule ufasaha wa lugha wanapoigiza. Hii ina maana kuwa, wanafunzi huchangamkia somo wanapoigiza ushairi.

**4.4.1.6 Kuibuliwa kwa Ilhamu ya Kutafiti Miongoni mwa Wanafunzi**

Utafiti ulibaini kuwa, watafitiwa watatu kati ya watafitiwa tisa (33%) walieleza kuwa, tamthilia inapotumika kufundishia utanzu wa ushairi, wanafunzi wanakuwa na ilhamu ya kutafiti zaidi kuhusiana na utanzu wa ushairi. Mtindo, muundo na maudhui ni vipengee ambavyo huwa vinajitokeza katika tanzu mbalimbali za ushairi;tanzu hizi huwa zimefungamanishwa katika tamthilia. Hivyo basi, wanafunzi wanapoelekezwa na mwalimu wao kuhusiana na ushairi kwa kutumia tamthilia ambayo pia huwa inafundishwa kwa ajili ya mitihani, ilhamu ya wanafunzi ya kutafiti kuhusiana na utanzu wa ushairi huibuliwa.

Aidha, watafitiwa walieleza kwamba, wanafunzi huenda maktabani kutafiti katika tamthilia ambazo huwa tofauti na zile ambazo huwa zinatahiniwa kuhusiana na vipengee vya mtindo, muundo na maudhui ambavyo hubainika katika tanzu mbalimbali ambazo huwa zimetumika na mtunzi wa tamthilia husika. Maelezo haya kutoka kwa wasailiwa hawa watatu yamelingana na maelezo ya nadharia ya utanzu, mhimili wa tatu (Bakhtin, k.h.j.) unaoshikilia kuwa, matumizi ya utanzu mwingine huwafanya wasomaji au wapokezi kuwa na ilhamu zaidi kuliko kuwapa kila wanachotarajia. Ushairi ni utanzu ambao ni tofauti na utanzu wa tamthilia lakini zote zinapotumika kwa pamoja hasa kwa maelekezo yake mwalimu, wanafunzi ambao wanaelekezwa huwa na ilhamu ya kutaka kujua zaidi umuhimu wa tanzu hizi mbili kutumika kwa pamoja.

Matokeo haya yamehusiana na ugunduzi wake Taylor (k.h.j.) anapoeleza kwamba, mwelekeo wa kufundisha ushairi kwa kutumia drama unatolea walimu mbinu ya kuwahusisha wanafunzi na hisia, njia ya kufanya kazi na mashairi ambayo hutumiwa kama msisimko wa kujadili au mikutano. Vilevile, hali hii imelingana na matokeo yao Chepkemboi, Chemwei na Awino (k.h.j.) wanapodhihirisha kuwa, wanafunzi wakiwa na mitazamo chanya, inakuwa rahisi kwa walimu kutekeleza ufundishaji mseto.

#### 4.4.1.7 Umakinifu wa Wanafunzi Darasani

Maelezo ya watafitiwa watano kati ya watafitiwa tisa (56%) yalionyesha kuwa, wanafunzi walimakinika darasani wakati mwalimu alipokuwa akiwaelekeza kuhusiana na vipengele vya mtindo, muundo na maudhui kwa kutumia tamthilia. Wasailiwa hawa walisema kwamba, tanzu mbalimbali za ushairi zilizobainika katika tamthilia ambayo hasa ilikuwa inatahiniwa, zilikuwa na vipengee muhimu ambavyo hujitokeza katika ushairi na hivyo basi, kuwafanya wanafunzi kuwa makini darasani kwa sababu vipengee vinavyodhihirika katika ushairi unaopatikana katika

tamthilia, ndivyo vinavyopatikana katika utanzu wowote wa ushairi ambao huwa haupo katika tamthilia.

Maelezo ya watafitiwa hawa watano yamekubaliana na nadharia ya utanzu, mhimili wa tatu (Bakhtin, k.h.j.) kuwa, utanzu mmoja unapotumika katika utanzu mwingine unawafanya wanafunzi kuwa na ilhamu ya kutaka kusoma zaidi kuhusiana na tanzu hizo mbili ambazo zinapatikana katika kazi husika ya fasihi.

Matokeo haya yanakubaliana na matokeo yao Suter na Busienei (k.h.j.) wanapohoji kuwa, mikakati ya ujifundishaji bora ni muhimu kwa wanafunzi. Mikakati hiyo huwawezesha wanafunzi kumakinika darasani wanapojifundisha. Vilevile, matokeo haya yameafikiana na matokeo yake Giebert (k.h.j.) anapoeleza kwamba, ili ushairi ufurahiwe, unahitaji kusikilizwa na kuzungumzwa na wanafunzi na kuwa si kusomwa kimyakimya. Kwa kufanya hivyo, wanafunzi huwa makini ushairi unapoigizwa kwa njia ya drama.

Matokeo ya utafiti huu kinyume na tafiti za awali yameonyesha mchango wa tamthilia katika ufundishaji wa ushairi kwa kuzingatia vipengee vya mtindo, muundo na maudhui. Tafiti za awali zilizingatia ushairi kwa kutumia drama hasa za Kiingereza. Hata hivyo, utafiti huu umeonyesha ubora katika ufundishaji wa vipengee vya mtindo, muundo na maudhui katika ushairi iwapo tamthilia itahusishwa.

## 4.5 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti kwa kutumia maelezo, mifano, majedwali na asilimia. Malengo matatu ya utafiti huu ambayo ni: Kuchunguza namna ushairi unavyofundishwa katika shule za upili, kupambanua namna tamthilia inavyoweza kutumika kufundisha ushairi na kueleza mchango wa matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa

ushairi yamechanganuliwa na kuwasilishwa kwa kutumia maelezo yaliyopatikana kwa watafitiwa tisa pamoja na tamthilia ya *Kifo Kisimani*, *Mstahiki Meya* na *Kigogo*.

Katika lengo la kwanza utafiti ulibaini kuwa maigizo, maswali na majibu, kazimradi, majadiliano, vikundi vya majadiliano, kanda au santuri, kukariri, kinuruweo, maelezo na mhadhara zilikuwa ni mbinu zilizotumiwa na watafitiwa kufundishia mtindo, muundo na maudhui katika ushairi. Utafiti ulibaini kuwa, tamthilia iliweza kutumika kufundishia mtindo, muundo na maudhui katika tanzu za ushairi kama vile nyimbo, mashairi huru na mashairi ya arudhi.

Aidha, utafiti ulibaini kuwa, tamthilia ilikuwa na mchango mkubwa katika ufundishaji wa utanzu wa ushairi. Mchango huo ulikuwa: Ufundishaji wa tamathali za usemi kwa urahisi, ufafanuzi bora wa muundo miongoni mwa wanafunzi, uelewa wa maudhui kwa urahisi miongoni mwa wanafunzi, ukamilishaji wa silabasi mapema miongoni mwa walimu, wanafunzi kuchangamkia somo, kuibuliwa kwa ilhamu ya kutafiti miongoni mwa wanafunzi na umakinifu wa wanafunzi darasani. Sura ifuatayo inatoa muhtasari wa tasnifu, hitimisho na mapendekezo.

## SURA YA TANO

## MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Sura hii inahusu muhtasari wa tasnifu, hitimisho na mapendekezo. Muhtasari wa tasnifu umetolewa kwa kuzingatia sura ya kwanza hadi ya tano. Muhtasari wa matokeo ya utafiti kwa kuzingatia malengo ya utafiti pia umeonyeshwa katika sura hii. Vilevile, hitimisho kwa kuzingatia malengo ya utafiti imeangaziwa katika sura hii. Aidha, mapendekezo kutokana na utafiti huu yameorodheshwa. Mwisho, mapendekezo ya tafiti za baadaye pia yameorodheshwa katika sura hii.

### 5.2 Muhtasari wa Tasnifu

Sura ya kwanza ya tasnifu hii iliweka msingi muhimu katika utafiti huu; ni sura iliyoweka lengo kuu la utafiti huu ambalo ni kuchunguza matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa ushairi katika shule za upili nchini Kenya bayana. Sura ilihusu vipengee muhimu vya utafiti huu ambavyo ni: usuli wa mada, suala la utafiti, malengo mahususi ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti na misingi ya nadharia.

Tasnifu hii imechunguza namna ushairi unavyofundishwa katika shule za upili kwa kutumia tamthilia katika Kaunti Ndogo ya Teso Kaskazini, Busia Kenya. Tasnifu hii imerejelea tamthilia tatu ambazo ni *Kifo Kisimani*, *Mstahiki Meya* na *Kigogo* kudhihirisha namna tamthilia inavyofanikisha ufundishaji wa ushairi. Watafitiwa tisa (9) ambao walikuwa ni kiwakilishi cha walimu wanaofundisha Kiswahili katika Kaunti Ndogo ya Teso Kaskazini walishiriki katika utafiti huu. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya utanzu.

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza namna tamthilia inavyotumika kufundisha ushairi katika shule za upili nchini Kenya. Lengo hili liliwekwa katika malengo mahususi ambayo ni: kuchunguza namna ushairi unavyofundishwa katika shule za upili, kupambanua namna tamthilia inavyoweza kutumika kufundisha ushairi na kueleza mchango wa matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa ushairi. Kwa hivyo, sura hii inatoa muhtasari wa tasnifu.

Sura ya pili iliangazia uhakiki wa maandishi mbalimbali. Utafiti ulihakiki maandishi ya wasomi mbalimbali kwa kurejelea malengo ambayo ni: kuchunguza namna ushairi unavyofundishwa katika shule za upili, kupambanua namna tamthilia inavyoweza kutumika kufundisha ushairi na kueleza mchango wa matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa ushairi.

Katika sura ya tatu, muundo wa utafiti huu umeangaziwa. Utafiti ulitumia muundo wa kimaelezo. Utafiti huu ulichunguza namna ushairi unavyofundishwa katika shule za upili kwa kuzingatia mhimili unaoshikilia kuwa, tanzu huibua muundo wa kazi ya fasihi na kufanya kazi hiyo ieleweke kwa urahisi sana. Vilevile, utafiti huu ulipambanua namna tamthilia inavyoweza kutumika kufundisha ushairi kwa kuzingatia mhimili uelezao kuwa, tanzu mbili zilizozoeleka zitumike kwa pamoja kwa sababu ya sifa zenye uhusiano mkubwa. Utafiti huu pia ulieleza mchango wa matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa ushairi kwa kuzingatia mhimili wa nadharia uelezao kuwa, matumizi ya utanzu mwingine huwafanya wasomaji au wapokezi kuwa na ilhamu zaidi kuliko kuwapa kila wanachotarajia. Kaunti Ndogo ya Teso Kaskazini ilichaguliwa kama eneo la utafiti kwa sababu ilikuwa na watafitiwa waliofaa utafiti huu na hivyo basi, kupata data za kutosha kutoka kwao kwa ajili ya utafiti huu.

Vilevile, sura ya tatu ilishughulikia sampuli na usampulishaji, njia za kukusanya data ambapo ni maktabani na nyanjani ambapo mbinu ya usaili na uchunzaji zilitumika. Uchanganuzi na uwasilishaji wa data, uhalali na uthabiti wa vifaa pia ni sehemu zilizoshughulikiwa katika sura ya

tatu ya tasnifu hii. Maadili katika utafiti yaliongoza mchakato mzima wa utafiti huu. Utafiti huu pia umeelezea changamoto zilizopatikana nyanjani.

Sura ya nne ilionyesha namna data zilivyochanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Data zilizokusanywa zilichanganuliwa kwa kuzingatia malengo yafuatayo: Namna ushairi unavyofundishwa katika shule za upili, namna tamthilia inavyoweza kutumika kufundisha ushairi na mchango wa matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa ushairi.

Sura ya tano inahusu muhtasari, hitimisho na mapendekezo. Muhtasari wa matokeo ya utafiti kwa kuzingatia malengo ya utafiti umetolewa. Vilevile, hitimisho ya sura hii hasa kwa kuzingatia malengo ya utafiti imetolewa. Aidha, mapendekezo yanayotokana na utafiti huu yameonyeshwa. Mwisho kabisa, mapendekezo ya tafiti za baadaye yameorodheshwa.

## 5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Sura ya nne iliweka wazi matokeo ya utafiti uliofanyika maktabani na nyanjani. Katika utafiti huu, data zilizopatikana nyanjani na maktabani zimechanganuliwa na kuwasilishwa kwa kuzingatia malengo matatu mahususi ya utafiti. Muhtasari wa matokeo ya utafiti umepangwa kwa kuzingatia vijimada vifuatavyo:

### 5.3.1 Namna Ushairi Unavyofundishwa Katika Shule za Upili

Utafiti ulibaini kuwa, vipengee vya mtindo, muundo na maudhui katika tanzu za ushairi vilifundishwa kwa kutumia mbinu kadha wa kadha. Mbinu zilizotumika kufundisha vipengee hivyo zilikuwa ni: maigizo, maswali na majibu, maelezo, mhadhara, kukariri mashairi, majadiliano, vikundi vya majadiliano, kinuruweo na kazimradi.

### 5.3.2 Namna Tamthilia Inavyoweza Kutumika Kufundisha Ushairi

Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, tamthilia inaweza kutumika kufundisha utanzu wa ushairi kwa kuzingatia tanzu za ushairi kama vile nyimbo, mashairi huru na mashairi ya arudhi. Utafiti ulibaini kuwa, vipengee vya mtindo, muundo na maudhui vilivyopatikana katika tanzu hizo vilibainika katika tamthilia.

### 5.3.3 Mchango wa Matumizi ya Tamthilia Katika Ufundishaji wa Ushairi

Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, ufundishaji wa ushairi kwa kutumia tamthilia ulichangia ufundishaji wa tamathali za usemi kwa urahisi. Utafiti ulionyesha kuwa, tamthilia inapotumika kufundishia utanzu wa ushairi, tamathali zinazobainika katika nyimbo, mashairi huru na mashairi ya arudhi ziliwasilishwa kwa njia iliyo rahisi kwa wanafunzi.

Aidha, utafiti ulibaini kuwa, muundo wa tanzu za ushairi ulifafanuliwa vyema zaidi kwa kuwa ulipatikana katika tamthilia iliyokuwa ikitahiniwa; namna muundo wa tanzu za ushairi ulivyobainika katika tamthilia ndivyo ulivyobainika katika tanzu zingine za ushairi ambazo hazikuwa katika tamthilia. Utafiti pia ulidhihirisha kuwa, matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa ushairi yalichangia uelewa wa maudhui kwa urahisi miongoni mwa wanafunzi; wanafunzi walielewa maudhui ya ushairi kwa urahisi kwa sababu yalifundishwa kutokana na tamthilia iliyoyafungamanisha. Vilevile, utafiti ulibaini kuwa, walimu walikamilisha silabasi kwa wakati ufaao kwa sababu vipengele vya mtindo, muundo na maudhui ambavyo vilibainika katika nyimbo pamoja na mashairi katika tamthilia, ndivyo vilivyobainika katika ushairi ukiwa umejisimamia tu au tamthilia ikiwa imejisimamia tu na hivyo basi, kuwasaidia walimu kukamilisha silabasi kwa wakati ufaao.

Mchango mwingine wa kutumia tamthilia katika kufundishia ushairi ni kuwa, wanafunzi walichangamka darasani; wanafunzi walifurahia namna vipengee vya mtindo, muundo na

maudhui katika tanzu za ushairi vilivyofundishwa kwa kutumia tamthilia. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, ilhamu ya kutafiti iliibuliwa miongoni mwa wanafunzi kwa sababu wanafunzi walitaka kujua iwapo vipengee vya mtindo, muundo na maudhui katika ushairi vilibainika katika tamthilia zingine kando na ile iliyokuwa ikitahiniwa. Matokeo ya utafiti huu pia yalionyesha kuwa, wanafunzi walimakinika darasani kwa sababu ya kutaka kupata maelezo zaidi kuhusiana na namna vipengee vya mtindo, muundo na maudhui katika ushairi vilivyofafanuliwa kwa kutumia tamthilia na namna vilivyobainika katika tamthilia yenyewe.

### 5.4 Hitimisho

Katika sura hii, muhtasari wa tasnifu umetolewa. Vilevile, muhtasari wa matokeo ya utafiti kwa misingi ya malengo umezingatiwa. Matokeo hayo yalihusu namna ushairi unavyofundishwa katika shule za upili kwa kuzingatia vipengee vya mtindo, muundo na maudhui. Mbinu za ufundishaji wa vipengee hivyo zilikuwa ni: maigizo, maswali na majibu, maelezo, mhadhara, kukariri mashairi, majadiliano, vikundi vya majadiliano, kinuruweo na kazimradi. Vilevile, utafiti ulibaini kuwa, tamthilia inaweza kutumika kufundisha ushairi kwa kuzingatia vipengee vya mtindo, muundo na maudhui.

Kwa upande mwingine, matokeo ya utafiti yalionyesha kwamba, ufundishaji wa ushairi kwa kutumia tamthilia ulichangia ufundishaji wa tamathali za usemi kwa urahisi, muundo wa tanzu za ushairi ulifafanuliwa vyema zaidi kwa kuwa ulipatikana katika tamthilia iliyokuwa ikitahiniwa. Utafiti pia ulidhihirisha kuwa, matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa ushairi yalichangia uelewa wa maudhui kwa urahisi miongoni mwa wanafunzi. Vilevile, utafiti ulibaini kuwa, walimu walikamilisha silabasi kwa wakati ufaao. Vilevile, matokeo ya utafiti yalionyesha kwamba, wanafunzi walichangamka darasani. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, ilhamu ya kutafiti

iliibuliwa miongoni mwa wanafunzi. Matokeo ya utafiti huu pia yalionyesha kuwa, wanafunzi walimakinika darasani.

## 5.5 Mapendekezo

Mapendekezo yanayowasilishwa hapa yanatokana na matokeo ya utafiti huu. Mapendekezo haya yanalenga kuchangia katika kuimarisha ufundishaji kwa kutumia mwelekeo mseto. Mapendekezo hayo ni:

i. Walimu watilie maanani mbinu mahususi za ufundishaji wanapofundisha vipengee vya ushairi kama vile mtindo, muundo na maudhui ili kuhakikisha kwamba, wanafunzi wanafurahia utanzu wa ushairi.

ii. Aidha, taasisi ya uundaji mitalaa inapendekezewa kurahisisha ufundishaji na ujifundishaji wa utanzu wa ushairi kwa kusisitiza mbinu ya mwelekeo mseto.

iii. Usetaji katika ufundishaji na ujifunzaji uweze kutiliwa maanani na walimu wanapofunza ushairi wa Kiswahili kwa kusudi la kuondoa uchovu miongoni mwa wanafunzi.

iv. Walimu waboreshe mwelekeo wa ufundishaji mseto kusudi mada zinazofundishwa zieleweke bora zaidi.

v. Walimu wazingatie mchango wa matumizi ya tamthilia katika ufundishaji wa ushairi.

## 5.6 Tafiti za Baadaye

Utafiti huu ulikuwa na matokeo yake yaliyodhihirisha kuwa, tamthilia za Kiswahili ni mbinu mwafaka katika ufundishaji wa ushairi wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za upili nchini Kenya. Utafiti huu unapendekeza yafuatayo kuhusiana na tafiti za baadaye:

i. Tafiti za baadaye zishughulikie namna vijenzi vingine vya ushairi vinavyofundishwa katika shule za upili kando na mtindo, muundo na maudhui.

ii. Kando na tamthilia, tafiti za baadaye zishughulikie namna riwaya au hadithi fupi zinavyochangia ufundishaji wa ushairi.

iii. Tafiti za baadaye zishughulikie mwingiliano wa tanzu zingine za fasihi katika ufundishaji kando na ushairi na tamthilia.

## MAREJELEO


Achillah, A.R. (2010). *Matumizi ya Mbinu ya Kimuktadha Katika Ufundishaji wa Msamiati wa Kiswahili Katika Shule za Upili za Wilaya ya Kakamega*. Tasnifu ya Uzamili, (Haijachapishwa): Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.

Ali, A. E. (2014). *Kutathmini Nafasi ya Mwanamke Katika Mashairi ya Kiswahili: Uchunguzi wa Mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala*. Tasnifu ya Uzamili, (Haijachapishwa): Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Arege, T.M. (2009). *Mstahiki Meya*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.

Bakhtin, M.M. (1981). *The Dialogic Imagination: Four Essays*. Austin and London: University of Texas Press.

Bashir, M., Afzal, M.T & Azeem, M. (2008). Reliability and Validity of Qualitative Operational Research Paradigm. *Pak. j.stat.oper.res.* Vol.IV, No.1, 2008, pp 35-45.

Chepkemboi, C., Chemwei, B. & Awino, J. O. (2018). Challenges Facing Implementation of Integrated Oral Literature Syllabus in Secondary Schools in Nakuru Town East Sub County. *IOSR Journal of Research and Method in Education (IOSR-JRME)-2018.*

Chepkemoi, N. & Wanyonyi, D. (2017). The Use of ICT in Teaching Kiswahili Play in Secondary Schools in Uasingishu County, Kenya. *European Scientific Journal*. Vol. 13.

Cheruto, A. & Orodho, J. A. (2016). Preparedness of Teachers of Kiswahili in Teaching Using Integrated Kiswahili Course in Secondary Schools in Kericho County, Kenya. *IOSR Journal of Research and Methods in Education (IOSR-JRME)*, Volume 6, pp 12-21.

Creswell, J.W.  (2007). *Qualitative Inquiry & Research Design: Choosing Among Five Approaches.* University of Nebraska, Lincoln: Sage Publications.

Creswell, J.W. (2014). *Research Design: Qualitative, Quantitative, and Mixed Methods Approaches (4th Edition)*. University of Nebraska, Lincoln: Sage Publications, Inc.

Day, H. (2014). *The Highwayman: A Narrative Poem Explored Through Drama*. Teaching Drama. Scheme of Work-KS2, summer term 1, w.w.w.teaching drama.co.uk.

Elting, S. & Firkins, A. (2006). Dramatizing Poetry in the Second Language Classroom. English *Teaching: Practice and Critique*, Volume 5. Number 3, pp 127-136.

Feinberg, R.M. (1979). Poetry Theater-Integrating Drama and Poetry. *Workshop Presented at the National Council of Teachers of English CEE/Secondary Section Program*, Pittsburgh, PA.

Ferguson, K. (2014). Performing Poetry: Using Drama to Increase the Comprehension of Poetry. *A Research-into-Practice Series Produced by a Partnership between the Literacy and Numeracy Secretariat and the Ontario Association of Deans of Education.*

Gasparro, M. & Falletta, B. (1994). Creating Drama with Poetry: Teaching English as a Second Language through Dramatizatio and Improvisation. *EPIC Clearinghouse on Languages and Linguistics, Washington, DC*.

Giebert, S. (2014). Shall I Approach Thee Through Improvised Play? Dramatising Poetry. *Scenario*: ISSN 1649-8526, Volume viii, Issue 2.

Gilakjani, A. P. (2017). A Review of the Literature on the Integration of Technology into the Learning and Teaching of English Language Skills. *International Journal of English Linguistics.* Vol. 7, No.5; 2017: Canadian Center of Science and Education.

Haji, A.I., Muhammed, S.A., Hamad, A. K. & Omar, M. M. (1981). *Misingi ya Nadharia ya Fasihi.* Zanzibar: Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni: Wizara ya Elimu.

Hassan, A. M. A. (2013). *Kuchunguza Vipengele vya Fani Katika Mashairi ya Kiswahili: Ulinganishi na Ulinganuzi wa Mashairi ya Euphrase Kezilahabi na Haji Gora Haji*. Tasnifu ya Uzamili, (Haijachapishwa): Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Hassan, Z. A., Schattner, P. & Mazza D. (2006). Doing A Pilot Study: Why Is It Essential? *Malaysian Family Physicians of Malaysia Online Version: http://www.ejournal.afpm.org.my/*

Indede, F. N. (2008). Mabadiliko katika Umbo la Ushairi na Athari zake katika Ushairi wa Kiswahili. *Swahili Forum*, Uk.73-94.

Iyaya, R. M., Kobia, J. M. & Luganda, M. M. (2016). Uchanganuzi wa Mambo Yanayoathiri Ufundishaji wa Ushairi katika Shule za Upili Nchini Kenya. *Mara Research Journal of Kiswahili*. The Premier Research Publishing Hub. Vol. 1, No.1, Uk. 18-36.

Kaur, N. (2019). Integrated Approach in Science Teaching. *Journal of Emerging Technologies and Innovative Research (JETIR)*.

Kea, P. (2016). *Kigogo*. Nairobi: Storymoja.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques (2nd Edition).* New Delhi: New Age International (P) Limited, Publishers.

Kumar, R. (2011). *Research Methodology: A Step-by-step Guide for Beginners (3rd Edition)*. Los Angeles: SAGE Publications Inc.

Maitaria, J. N. (2012). Methali kama Fomula katika Utunzi na Uwasilishaji wa Ushairi: Mfano wa baadhi ya Mashairi ya Abdilatif Abdalla. Makala, (Hayajachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mapunjo, G. C. (2014). *Usawiri wa mwanamke kama kiongozi katika tamthiliya: Uchunguzi wa Kivuli Kinaishi na Nguzo Mama*. Tasnifu ya Uzamili, (Imechapishwa). Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Masebo, J.A. & Nyangwine (2010). *Nadharia ya Lugha: Kiswahili 1: Kidato cha 5 & 6.* Dar-es-Salaam: Nyambari Nyanguine Publishers.

Massamba, D. (1983). *Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili. Fasihi* (Makala za Semina ya Waandishi wa Kiswahili III). Dar-es-Salaam: TUKI.

Matundura, B. (2015). *Matatizo ya Uainishaji wa Tanzu za Kifasihi*. Chuo Kikuu cha Chuka.

Mberia, K.W. (2001). *Kifo Kisimani.* Nairobi: Marimba Publications Ltd.

Mlaga, W. K. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne ya 21*. Dar es Salaam, Tanzania: Heko Publishers Ltd.

Molenje, M. L. (2018). Challenges of Teaching the Revised Kiswahili Syllabus in Secondary Schools, a Case Study of Bungoma West District Kenya. *AJESS*.

Mugenda, O. M. & Mugenda, A.G. (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi: Acts Press.

Njogu, K. & Chimera, R. (2011). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nzuki, P.K. (2003). *Mwingiliano wa fani na maudhui katika Ushairi wa Kithaka wa Mberia*. Tasnifu ya Uzamili, (Imechapishwa): Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ogula, P.A. (2005). *Research Methods*. Nairobi: CUEA Publications.

Omollo, R. W., Wanami, S. & Kandagor, M. (2017). Attitudes of Tutors on ICT Integration in Teaching Kiswahili in Public Primary Teachers' Colleges in Kenya, the Case of Rift Valley Region. *International Journal of New Technology and Research (IJNTR),* Volume 3.

Opunde, S. (h.t). Mwelekeo Mseto Katika Ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili. Makala, (Hayajachapishwa), Kakamega: Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.

Orodho, A. (2004). *Techniques of Writing Research Proposals and Reports in Education and Social Sciences.* Nairobi: Masda Publishers.

Pasco, G., Gordon, R.K., Howlin, P. & Charman, T. (2008). The Classroom Observation Schedule to Measure Intentional Communication (COSMIC): An observational Measure of the Intentional Communication of Children with Autism in an Unstructured Classroom Setting. *Journal of Autism and Developmental Disorders*, 38, 1807-1818.

Shitemi, N. L. (2010). *Ushairi wa Kiswahili Kabla ya Karne ya Ishirini.* Eldoret: Moi University Press.

Suter, E. & Busienei A. J. (2013). Materials and Instructional Approaches Used by Secondary School Teachers of Kiswahili Oral Literature in Marakwet District, Kenya. *Journal of Emerging Trends in Educational Research and Policy Studies*, 4(3), 566-572.

Taasisi ya Elimu ya Kenya (2006). *Kiswahili Sekondari: Mwongozo wa Mwalimu.* Nairobi: KIE.

Taylor, A. (1994). ‘’On the Pulse”. Exploring Poetry through Drama. *Children’s Literature in Education*, 25(1), 17-28.

Tessier, S. (2012). From Field Notes, to Transcripts, to Tape Recordings: Evolution or Combination? *International Journal of Qualitative Methods*, 2012, 11(4).

Tsiaras, A. (2016). Teaching Poetry through Dramatic Play in Greek Primary School: Surveying Teachers’ and Pupils’ Views. *New Zealand Journal of Research in Performing Arts and Education*: Nga mahi a Rehia no Aotearoa.

Vannak, H. (n.d). Comparing Different Approaches Used in Teaching Literature in the ESL Classroom. *BELTEI International University*.

Vodickova, M. (2009). Interpretation of Poetry through Drama Activities. *Journal of NELTA*, vol.14, No.1-2.

Wafula, R.M. (2003). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo yake.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd., Kijabe Street.

Wangari, O. J. (2015). *Changamoto za Mikondo Mipya ya Utunzi wa Mashairi ya Kiswahili:* Tasnifu ya Uzamili, (Haijachapishwa): Mfano wa *Tunu ya Ushairi*. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Wanjala, F. S. & Kavoi, J. M. (2013). *Stadi za Mawasiliano na Mbinu za kufundishia Kiswahili: Kwa Wanafunzi, Walifunzi na Walimu*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) LTD.

Wanyela, S. J. (2007). *Matumizi ya ushairi katika tamthilia ya Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili, (Haijachapishwa): Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Yego, E. K. (2013). *Nafasi ya Mwanamke: Jinsi Inavyotolewa katika Nyimbo za Taarab za Zanzibar*. Tasnifu ya Uzamili, (Haijachapishwa): Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Yimwilai, S. (2015). An Integrated Approach to Teaching Literature in an EFL Classroom. *English Language Teaching*. Vol. 8, No. 2.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho 1: Mwongozo wa Maswali (Dodoso)

1. Unatumia mbinu zipi kufundisha ushairi?
2. Tafadhali fafanua namna unavyozitumia mbinu ulizozitaja ufundishapo ushairi kwa kurejelea:
    a) Mtindo
    b) Muundo
    c) Maudhui
3. Tafadhali elezea ubora wa kila mbinu uliyoitaja ufundishapo wanafunzi kwa kurejelea:
    a) Mtindo
    b) Muundo
    c) Maudhui
4. Ni kwa jinsi gani tamthilia inaweza kutumika kufundisha ushairi kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo:
    a) Mtindo
    b) Muundo
    c) Maudhui
5. Tamthilia ina mchango upi katika ufundishaji wa vipengele vifuatavyo vya ushairi?
    a) Mtindo
    b) Muundo
    c) Maudhui

**Kiambatisho 2: Mwongozo wa Kuchunza Vipindi**

1. Mwalimu anatumia mbinu zipi kufundishia mtindo, muundo, na maudhui katika ushairi?
2. Je, mwalimu anafaulu vipi kutumia mbinu hizo kufundishia mtindo, muundo na maudhui katika ushairi?
3. Ni mbinu ipi inayotawala ufundishaji wa mtindo, muundo na maudhui katika ushairi?
4. Ni mbinu gani ya kufundishia mtindo, muundo na maudhui katika ushairi ambayo mwalimu ameifaragua papo hapo darasani?
5. Je, mwalimu ametumia mbinu alizozipendekeza katika maazimio ya kazi na maandalizi ya somo kufundishia mtindo, muundo na maudhui katika ushairi?

**Kiambatisho 3: Orodha ya Shule**

Orodha ya shule zipatikanazo katika Kaunti Ndogo ya Teso Kaskazini, Kaunti ya Busia, nchini Kenya

1. Bishop Sulumeti Chelelemuk Girls High School
2. Kolanya Girls High School
3. Kolanya Boys High School
4. St. Thomas Amagoro Girls High School
5. Adanya Secondary School
6. Moding Secondary School
7. Albert Ekirapa Secondary School
8. Bishop King'oo Okuleu Secondary School
9. Changara Secondary School
10. Kakamer Secondary School
11. Kekalet Secondary School
12. Kakurikit Secondary School
13. Kabukui Secondary School
14. Oduya Oprong Secondary School
15. Apokor Girls Secondary School
16. Katakwa Secondary School
17. Chamasiri Secondary School
18. Mwari Secondary School
19. Aedomoru Secondary School
20. Kamuriai Secondary School

21. Kocholia Secondary School

22. St. Anthony Akobwait Secondary School

23. Katanyu Secondary School

24. S.A Aboloi Secondary School

25. St. John's Kajei Secondary School

26. Onyunyuri Secondary School


27. St. Teresa Malaba Secondary School

28. Kokare Secondary School

29. St. Augustine Kamolo Secondary School

30. Keng'atunyi Secondary School

## Kiambatisho 4: Ramani ya Utafiti



**Kiambatisho 5: Ratiba ya kazi**

| SHUGHULI | WAKATI | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Juni 2017 | Julai 2017 | Sept 2017 | Okt 2017 | Feb 2018 | Mach 2018 | Mei 2018 | Juni 2018 | Julai 2018 | Agosti 2018 |
| Mapitio ya maandishi | | | | | | | | | | |
| Kuandika pendekezo la utafiti | | | | | | | | | | |
| Kuwasilisha pendekezo la utafiti kwa idara | | | | | | | | | | |
| Kuwasilisha pendekezo la utafiti kwa kitivo | | | | | | | | | | |
| Kuwasilisha pendekezo la utafiti kwa SGS | | | | | | | | | | |
| Utafiti majaribio | | | | | | | | | | |
| Kukusanya data | | | | | | | | | | |
| Uchanganuzi wa data | | | | | | | | | | |
| Kuwasilisha tasnifu | | | | | | | | | | |
| Kuwasilisha rasimu ya tasnifu ya kwanza kwa idara | | | | | | | | | | |
| Kuwasilisha rasimu ya tasnifu kwa Kitivo | | | | | | | | | | |
| Kuwasilisha rasimu ya mwisho ya tasnifu kwa SSJ | | | | | | | | | | |

**Kiambatisho 6: Maazimio ya Kazi**

MAAZIMIO YA KAZI : KDT 3 - 2019

| JUMA | KIPINDI | SOMO | TALIYOMO | LENGO | MBINU | MAREJELEO | NYENZO | MAONI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 7. | 1. | KUSOMA | Mashairi: Bahari kulingana na mpangilio wa maneno | Mwanafunzi aweze kubainisha bahari | Maswali na majibu | Mwanga wa ushairi kwa shule za upili. | Kitabu | |
| | 2. | KUSOMA | Maudhui katika ushairi | Mwanafunzi aweze kubainisha maudhui katika shairi | Maelezo | Kiswahili kitukuzwe 3 | Kitabu. | |
| | 3. | KUANDIKA | Insha ya maelezo | Mwanafunzi aweze kuandika insha nzuri ya maelezo. | -Majadiliano<br>-Maelezo | Chemchemi za Kiswahili-3 | Kitabu. | |
| | 4. | SARUFI | Vitenzi | Mwanafunzi aweze kueleza maana ya vitenzi | -Kuandika<br>-Kueleza | Chemchemi za Kiswahili-3 | Chati | |
| | 5. | FASIHI | Chozi la Heri.<br>Sura ya tatu | Mwanafunzi aweze kuandika muhtasari wa matukio | -Kuchambua<br>-Kusoma<br>-Kueleza. | Assumpta K. Matei, Chozi la Heri | Riwaya | |
| | 6. | FASIHI | Chozi la Heri ~~Sura~~<br>Sura ya nne | Mwanafunzi aweze kuandika muhtasari wa matukio | -Kusoma<br>-Kuchambua<br>-Kueleza | Assumpta K. Matei, Chozi la Heri | Riwaya | |

## Kiambatisho 7: Maazimio ya Kazi

MAAZIMIO YA KAZI: KIDATO CHA 3 – 2019.

| JUMA | KIPINDI | SOMO | TAKWIMU/MADA | LENGO | MBINU | ASILIA | VIFAA | MAONI. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 10 | 1 | Kusikiliza na Kuzungumza | Mjadala | Mwanafunzi aweze kushiriki mjadala ipasavyo. | Majadiliano | Chemichemi za Kiswahili Kidato 3 | Kitabu | Somo lilifunzwa. |
| | 2 | Fasihi | Ushairi: Nyimbo. | Mwanafunzi aweze kueleza sifa na umuhimu wa nyimbo | Mhadhara | Chemichemi za Kiswahili Kidato 3 | Kanda za video | Somo lilikamilika vema. |
| | 3 | Fasihi | Mashairi. uhuru wa kishairi | Mwanafunzi aweze kueleza uhuru wa kishairi. | Kuuliza na kujibu. | Miale ya ushairi | Diwani | somo lilifundishwa, |
| | 4 | Kuandika | Isimujamii: chimbuko la Kiswahili | Mwanafunzi aweze kueleza chimbuko la kiswahili. | Maelezo | Kiswahili kitukuzwe – kdt3 | chati | Wanafunzi walieleza chimbuko la kiswahili. |
| | 5 | Sarufi | Mnyambuliko wa vitenzi vya silabi moja. | Mwanafunzi aweze kutaja vitenzi vya silabi na kuvinyambua | Ungambuzi. Maelezo. | Chemichemi za kiswahili | chati | somo lilifunzwa. |
| | 6 | kuandika | Isimujamii: sifa za lugha | Mwanafunzi aweze kueleza maana na sifa za lugha. | Maelezo kuandika | Fani ya Isimujamii kwa shule za upili. | Kitabu. | Wanafunzi waliandika. |

## Kiambatisho 8: Maandalizi ya Somo

**LESSON PLAN**

SUBJECT: KISWAHILI

TOPIC: MASHAIRI YA KISWAHILI

SUB TOPIC: Mtiririko, Ukara na ukaraguzi.

CLASS: 3B NO. OF STUDENTS: 35

DURATION: 9:30 – 10:10 DATE: 28 – 01 – 19

PREREQUISITE KNOWLEDGE/SKILLS

Awe na Uelewa wa awali kuhusu vina.

OBJECTIVES

Kufikia mwisho wa somo mwanafunzi aweze kubainisha bahari za mashairi

TEACHING AND LEARNING MATERIALS

1. Ubao na chaki
2. Chati

REFERENCE

Mwanga wa ushairi.

| STAGE | T/L ACTIVITIES | LEARNING POINTS | REMARKS |
|---|---|---|---|
| Introduction (5) mins | Kutoa maelezo ya mtiririko, ukara na ukaraguni | Mwanafunzi kuandika. | wanafunzi waliandika. |
| Development (30) mins | 1. Kuwaweka wanafunzi katika vikundi ili wajadiliane<br>2. Kuwapa wanafunzi maswali ili wajadili | 1 wanafunzi kuja dili na kujibu maswali ipasavyo. | wanafunzi walifuata maagizo. |
| Conclusion (5) mins | Kueleza kwa ufupi kuhusiana na mtiririko, ukara na ukaraguni | wanafunzi kunakili hoja muhimu za mwalimu | Wanafunzi waliandika hoja muhimu |

**Kiambatisho 9: Maandalizi ya Somo**

TAREHE 22/01/019.

ANDALIO LA SOMO

SOMO: KISWAHILI
MADA: USHAIRI
MADA NDOGO: NYIMBO
KIDATO CHA TATU: IDADI YA WANAFUNZI: 32.
MADHUMUNI: Kufikia Mwisho wa kipindi mwanafunzi aweze Kueleza Sifa na umuhimu wa nyimbo.

NYENZO:
1. Kanda za nyimbo
2. Wanafunzi wenyewe.

MAREJELEO
1. Kiswahili kitukuzwe — Kidato cha 3.

| HATUA/MUDA | SHUGHULI ZA MWALIMU | SHUGHULI ZA MWANAFUNZI |
|---|---|---|
| 1. DAK 5 | UTANGULIZI<br>Maelezo Kuhusu nyimbo | Kuandika na Kuchangia Kueleza na kujibu maswali |
| 2. DAK 30 | MWENDELEZO<br>Kueleza sifa na umuhimu wa nyimbo | Wanafunzi Kuchangia Kueleza huku wakiandika na kujibu maswali ya mwalimu |
| DAK 5. | HITIMISHO<br>Kutoa Muhtasari kuhusu maana, sifa na umuhimu wa nyimbo | Wanafunzi Kunakili muhtasari |

**Kiambatisho 10: Maandalizi ya Somo**

10/01/19

Andalio la Somo la Kiswahili.

MADA : USHAIRI

MADA NDOGO : Aina za nyimbo

KIDATO : 3

IDADI : Wanafunzi 43

Malengo : Kufikia mwishoni mwa somo mwanafunzi aweze kueleza aina za nyimbo.

NYENZO :

1. Ubao na chaki
2. Chati.

MAREJELEO :

Chemichemi za Kiswahili - Kdt 3

| MUDA | SHUGHULI ZA MWALIMU | SHUGHULI ZA MWANAFUNZI |
|---|---|---|
| DAKIKA 5 | Utangulizi<br>Kushirikisha wanafunzi katika kutaja aina za nyimbo | Wanafunzi kushiriki katika kutaja aina za nyimbo. |
| DAKIKA 15 | Mwendelezo<br>Kikundi cha kwanza kuwasilisha kazi yao kuhusu aina za nyimbo namna mwalimu atakavyowapanga. | Wanafunzi kuwasilisha darasani majibu yao kuhusiana na aina za nyimbo namna ilivyoratibiwa na mwalimu. |
| DAKIKA 15 | Kikundi cha pili kuwasilisha kazi yao kuhusu aina za nyimbo namna ilivyoagizwa na mwalimu. | Kikundi cha pili cha wanafunzi kuwasilisha kazi zao darasani. |
| DAKIKA 5 | Hitimisho.<br>Kueleza kwa kifupi aina za nyimbo. | Wanafunzi kuandika. |

**Kiambatisho 11: Maandalizi ya Somo**

ANDIKO LA SOMO KWA KIDATO CHA 3
TAREHE : 29/01/19
SOMO : KISWAHILI
MADA : BAHARI YA MASHAIRI
MADA NDOGO : NGONJERA
IDADI YA WANAFUNZI : 37
MUDA : SAA 8·00 – 8·40 ASUBUHI

SHABAHA: Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze kuchambua shairi la ngonjera kimtindo, kimuundo na kutambua dhamira ya mwandishi na maudhui yaliyomo.

VIFAA VYA KUFUNDISHA
① Diwani ya mashairi
② Ubao na chaki

MAREJELEO
1. Miale ya Ushairi

| HATUA | SHUGHULI ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI | HOJA MUHIMU ZA UJIFUNZAJI | MAONI |
|---|---|---|---|
| Utangulizi (Dak. 5) | Kueleza maana ya ngonjera | Wanafunzi kuchangia kueleza na kuandika | Wanafunzi waliandika |
| Mwendelezo (Dak. 30) | 1. Wanafunzi kuwekwa katika makundi ili kuigiza ngonjera teule<br>2. Mwalimu kueleza hoja muhimu kuhusu vipengele vya ngonjera | 1. Wanafunzi kuigiza ngonjera<br>2. Wanafunzi kunakili vipengele muhimu kuhusu ngonjera | 1. Wanafunzi waliigiza<br>2. Wanafunzi walinakili |
| Hitimisho (Dak. 5) | Mwalimu kueleza mambo muhimu kuhusu somo na kuwapa wanafunzi zoezi | Wanafunzi kuandika yale yasemwayo na mwalimu | Wanafunzi waliandika zoezi |

## Kiambatisho 12: Hifadhi ya Kazi

Teacher ______ Subject KISWAHILI

Form 3 Term 1 Week 11 Year: 20 19

| DAY | LESSON | WORK COVERED | COMMENTS | SIGNATURE |
|---|---|---|---|---|
| MON | 1 | Isimujamii: Historia na maendeleo ya Kiswahili | Wanafunzi waliandika | |
| TUE | 2 | Fasihi: Simulizi: Misimu | Wanafunzi waliandika kazi ya mwalimu | |
| WED | 3 | Ushairi: Uhuru wa Kushairi | Wanafunzi waliandika | |
| THU | 4 | Kusoma: Uchambuzi wa Kigogo | Somo lilikamilika vema | |
| FRI | 5 na 6 | Kusoma: Uchambuzi wa Kigogo. | Wanafunzi walichambua | |

| | COMMENTS | SIGNATURE |
|---|---|---|
| SUBJECT HEAD | | |
| HEAD OF DEPARTMENT | | |
| PRINCIPAL'S COMMENTS | | |

## Kiambatisho 13: Hifadhi ya Kazi

HIFADHI YA KAZI

JUMA LA 10 : MUHULA WA 1: 2019

| SIKU | KIPINDI | KAZI | MAONI |
|---|---|---|---|
| Jumatatu | 1 | Malumbano ya utani: Sifa | Somo lilikamilika vyema. |
| Jumanne | 2. | Mbinu za uandishi katika mashairi | Somo lilifundishwa |
| Jumatano | 3. | Maudhui katika ushairi | Wanafunzi walinakili kazi ya Mwalimu |
| Alhamisi | 4. | Mazungumzo: Soga. | Wanafunzi walinakili kazi ya Mwalimu |
| | 5. | Mazungumzo: Hotuba | Wanafunzi waliandika |
| Ijumaa | 6 | Kusoma kwa Ufahamu: | Wanafunzi walisoma na kujibu maswali ya ufahamu |

**Kiambatisho 14: Hifadhi ya Kazi**

REKODI YA KAZI

JUMA: 6 MUHULA: 1 MWAKA: 2019

| SIKU | KIPINDI | KAZI | MAONI |
|---|---|---|---|
| JUMATATU | 1 | Vitendawili na Mafumbo | Wanafunzi Waliandika Makala. |
| JUMANNE | 2 | Ukanushi Kulingana na nafsi – LI–NA–TA–ME–HU–NGE–NGALI | Wanafunzi Walifanya Kazi ya Mwalimu |
| JUMATANO | 3 | Ushairi: Shairi la ngonjera na Malumbano | Wanafunzi Waliigiza darasani |
| | 4 | Muundo Wa Shairi na tamathali za Usemi | Wanafunzi Waliandika Kazi ya Mwalimu na Kupewa Kazi ya Kutafiti Kuhusu Muundo na tamathali za Usemi |
| ALHAMISI | 5 | Kusoma kwa Ufahamu; Kitaba: Chemichemi za Kiswahili – kdt 3 | Somo lilifunzwa |
| IJUMAA | 6 | Fasihi: Nizikeni Papa hapa – Tumbo Lisiloshiba na hadithi nyingine | Somo lilifunzwa |

### Kiambatisho 15: Barua ya Idhini Kutoka SGS

KIBABII UNIVERSITY
(Knowledge for Development)

Tel: 020 – 2028660 / 0708 –085934 / 0734 - 831729
P.O. Box 1699 – 50200
Bungoma
Kenya

E-mail: enquiries@kibabiiuniversity.ac.ke /
registrar.adm58@yahoo.com
Website: http://www.kibu.ac.ke

**OFFICE OF THE DEAN**
*SCHOOL OF GRADUATE STUDIES*

**Ref**: KIBU/SGS/CORR.033/VOL.1-2015/133

**Date:** 4th February 2019

Dear Mukoya Hillary Mauka
Reg. No: MED/KIS/008/14

**RE: APPROVAL OF RESEARCH PROPOSAL**

I am pleased to inform you that the Senate of Kibabii University acting on the advice of the Board of the School of Graduate Studies approved your proposal Entitled: **"Ufundishaji wa Ngonjera Katika Shule za Upili kwa Kutumia Tamthilia: Uchunguzi Kifani wa Kaunti ya Busia Kenya"** and appointed the following as supervisors:

1. Dr. Edwin Masinde
2. Dr. Debora Amukowa

You will be required to submit through your supervisor(s) progress reports every three months to the Dean SGS. Reports should be copied to the following: Chairman, FGSC-FESS and Chairman, DGSC-KOAL

It is the policy of the University that you observe a deadline of two years from the date of registration for a Masters thesis. Do not hesitate to consult this office incase of any problem encountered in the course of your work.

Yours Sincerely,

Prof. S. N. Mutsotso
**Dean, SGS**

**Copy to:** Vice Chancellor
Deputy Vice Chancellor (ASA)
Deputy Vice Chancellor (AFD)
Deputy Vice Chancellor (PPRI)
Director PC&QA

**Kibabii University ISO 9001:2015 Certified**
**Knowledge for Development**

**Kiambatisho 16: Barua ya Idhini Kutoka NACOSTI**



NATIONAL COMMISSION FORSCIENCE, TECHNOLOGY ANDINNOVATION

Telephone:+254-20-2213471, 2241349,3310571,2219420
Fax: +254-20-318245,318249
Email: dg@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke
When replying please quote

9thFloor, Utalii House
Uhuru Highway
P.O. Box 30623-00100
NAIROBI-KENYA

Ref: No. **NACOSTI/P/19/62338/28393**

Date: **26th February, 2019**

Hillary Mauka Mukoya
Kibabii University
P.O. Box 1699-50200
**BUNGOMA.**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Following your application for authority to carry out research on ***"Ufundishaji wa Ngonjera katika Shule za Upili kwa kutumia Tamthilia: Kifani wa kaunti ya Busia Kenya"*** I am pleased to inform you that you have been authorized to undertake research in **Busia County** for the period ending **26th February,2020.**

You are advised to report to **the County Commissioner and the County Director of Education, Busia County** before embarking on the research project.

Kindly note that, as an applicant who has been licensed under the Science, Technology and Innovation Act, 2013 to conduct research in Kenya, you shall deposit **a copy** of the final research report to the Commission within **one year** of completion. The soft copy of the same should be submitted through the Online Research Information System.

**GODFREY P. KALERWA MSc., MBA, MKIM**
**FOR: DIRECTOR-GENERAL/CEO**

Copy to:

The County Commissioner
Busia County.

The County Director of Education
Busia County.

National Commission for Science, Technology and Innovation isISO9001:2008 Certified

## Kiambatisho 17: Kibali cha Utafiti Kutoka NACOSTI

Innovation National Commission for Science, Technology and Innovation National Commission for Science, Technology and Innovation National Commission

**THIS IS TO CERTIFY THAT:**
***MR. HILLARY MAUKA MUKOYA***
**of KIBABII UNIVERSITY, 389-50200 BUNGOMA,has been permitted to conduct research in *Busia County***

**on the topic: *UFUNDISHAJI WA NGONJERA KATIKA SHULE ZA UPILI KWA KUTUMIA TAMTHILIA: KIFANI WA KAUNTI YA BUSIA KENYA***

**for the period ending:**
***26th February,2020***

**Permit No : NACOSTI/P/19/62338/28393**
**Date Of Issue : 26th February,2019**
**Fee Recieved :Ksh 1000**



...............................
***Applicant's Signature***

...............................
***Director General***
***National Commission for Science, Technology & Innovation***

**Kiambatisho 18: Barua ya Idhini Kutoka kwa Kamishna wa Kaunti ya Busia**

**REPUBLIC OF KENYA**

**THE PRESIDENCY**
**MINISTRY OF INTERIOR AND CO-ORDINATION OF NATIONAL GOVERNMENT**

**Email: ccbusia@gmail.com**
**Telephone: 055 - 22598**
**Fax No: 055 - 22231**
**When replying please quote**
**REF No. ADM 15/4/ VOL.VI/ (99)**

**COUNTY COMMISSIONER'S OFFICE**
**BUSIA COUNTY**
**P.O. BOX 14-50400**
**BUSIA (K)**

**30th May , 2019**

**All Deputy County Commissioners**
**BUSIA COUNTY**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Following research authorization vide letter Ref.No.NACOSTI/P/19/62338/28393 dated 26th February, 2019 by the National Commission for Science, Technology and Innovation on ***"Ufundishaji wa Ngonjera katika shule za Upili kwa kutumia Tamthilia: Kifani wa kaunti ya Busia Kenya,"*** this is to inform you that **Hillary Mauka Mukoya** has been authorized to carry out research in Busia County for the period ending 26th February, 2020.

Kindly accord him the due co -operation.

Samuel Kimani
For: County Commissioner
**BUSIA COUNTY**

Copy to:

Hillary Mauka Mukoya
Kibabii University
P.O BOX 1699 - 50200
**BUNGOMA**

COUNTY COMMISSIONER'S OFFICE - BUSIA Page 1

**Kiambatisho 19: Barua ya Idhini Kutoka kwa Mkurugenzi wa Elimu katika Kaunti ya Busia**

HARAMBEE

**REPUBLIC OF KENYA**

**MINISTRY OF EDUCATION**
**STATE DEPARTMENT OF EARLY LEARNING AND BASIC EDUCATION**

***Telephone: 055-22152***
***Fax:;055-22152***
***When replying please quote***
Email:cdebusia@gmail.com

COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION
BUSIA COUNTY
P.O. BOX 15 - 50400
BUSIA (K)

**7th June, 2019**

**Ref No. BSA/CDE/ED/9/6/(169)**

Sub-County Director of Education
**TESO NORTH SUB-COUNTY**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

This office is in receipt of letter from Kenya National Commission for Science, Technology and Innovation (NACOSTI) authorizing research on "***Ufundishaji wa Ngonjera katika shule za upili kwa kutumia Tamthilia: Kifani wa kaunti ya Busia, Kenya***" in your sub-counties for the period ending 26th February, 2020.

This is to inform you that Mr. Hillary Mauka Mukoya has been authorized to conduct the research. Kindly accord him the necessary assistance.

**PAMELLA A. AKELLO**
FOR: COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION
**BUSIA COUNTY**

COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION
07 JUN 2019
Sign...
P.O. Box 15 - 50400, BUSIA (K)

**C.C.**

Mr. Hillary Mauka Mukoya
Kibabii University
**BUNGOMA**